Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 19 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne. S. Makinda ) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa fedha 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII - MHE. MARGARET S. SITTA:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE.CHRISTOWAJA G. MTINDA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 258

**Gharama ya Kituo cha Afya cha Kharumwa**

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR** aliuliza:-

Kituo cha afya cha Kharumwa kinazidiwa uwezo kutokana na kupokea wagonjwa wengi kutoka Jimbo la Nyang'hwale na Wilaya za jirani. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa ziara za kampeni Jimboni humo, aliahidi kukipandisha hadhi kituo hicho kuwa hospitali za Wilaya ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa:-

Je, gharama za upanuzi huo zitakuwemo kwenye Bajeti hii ya mwaka 2010/2011?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya cha Kharumwa kinatumika kama Hospitali ya Wilaya mpya ya Nyang'hwale. Mpango wa Serikali ni kukiboresha kituo hicho ili kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi wa eneo hilo. Katika mwaka 2010/2011 Halmashauri ilitumia shilingi 9.8 wa ajili ya kujenga tanuru la kuchomea taka hatarishi (*Incinarator*).

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 Halmashauri imewasilisha maombi maalum Wizara ya Fedha na Uchumi ya shilingi milioni 700 kwa ajili ya upanuzi wa kituo cha Afya cha Kharumwa. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 imetenga shilingi milioni 42.4 kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi(MMAM) kwa ajili ya kuboresha Wodi za wagonjwa na kupanua chumba cha upasuaji wa kituo hicho. Aidha, shilingi milioni 30 zimetengwa katika Bajeti ya Halmashauri kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni kujenga Hospitali ya Wilaya katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale itakayoanzishwa. Eneo la ujenzi wa hospitali hiyo limetengwa katika eneo lililopo Kharumwa kutokana na kituo cha afya Kharumwa kuwa na eneo dogo.

**MHE. HUSSEIN AMAR NASSOR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, pia naipongeza Serikali kwa kukipandisha kituo cha afya na kuwa hospitali ya Wilaya, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa sababu msongamano wa wagonjwa katika kituo hicho cha afya ni mkubwa na mpango huu wa kukiboresha kituo hicho ni wa muda mrefu kidogo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwapeleka Madaktari, Wauguzi na kupeleka madawa kwa haraka ili kuweza kupunguza msongamano huo?

(b) Je, Waziri utakuwa tayari kufanya ziara katika Jimbo la Nyang'hwale katika Kata ya Nyang'hwale ili kuweza kukiangalia kituo cha afya kilichopo ambacho kina

majengo mazuri kilichotelekezwa na kuweza kuangalia matatizo mbalimbali yaliyopo katika zahanati za Jimbo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hiki anachosema Mbunge kwamba kuna msongamano, ni kweli, na mimi mwenyewe nimefika katika Wilaya hii mpya inayozungumzwa hapa. *Population* yao ni laki nne na wana vituo viwili tu vya afya ambavyo vinafanya kazi. Kituo cha afya kwa wastani kinakuwa na watu kama elfu 50 sasa *you can imagine* kama wapo watu laki nne, hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anachosema hapa Mbunge kwamba kituo hiki ambacho Rais aliahidi kwamba kitapanuliwa, kitapanuliwa kama tulivyoeleza kwenye mpango huu unaozungumzwa hapa, na pembeni ya hospitali hapo kuna eneo ambalo tumelipata ambalo ndilo litakalotumika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapanua ile hospitali ya Wilaya ambayo tumeizungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutahadharisha tu kwamba wapo wananchi ambao wanajiingiza katika lile eneo na wanataka kuchukua lile eneo, nimemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe kwamba anapata Hati Miliki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Madaktari na Madawa sisi hatuna tatizo kwa sababu tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya Afya. Kuna kitu kinachoitwa *intergrated logistic system* ambacho kinatusaidia kujua kiasi cha dawa kinachohitajika katika eneo na wakati huo huo kujua Madakatri wanaohitajika katika lile eneo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mbunge tuwasiliane naye ili tuweze kumsaidia kwa sababu nimefika katika eneo lile na kitu anachosema ni kweli. Mimi naomba nimpongeze hapa kwa kazi nzuri anayoifanya. Mbunge huyu tangu amekuja hapa ameshauliza maswali mengi sana yanayohusu maendeleo ya Mkoa huu mpya, kwa hiyo nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hiki kituo anachozungumza cha kutelekezwa hapa, wanaojenga hospitali ni Halmashauri, wanaojenga vituo vya afya ni Halmashauri, wanaojenga zahanati ni Halmashauri wala siyo Wizara ya Afya na ndiyo maana tunajibu maswali haya. Kama kuna kituo ambacho kimetelekezwa hapa maelekezo yangu ni kwamba wakutane na waseme kwamba kituo hiki tunataka kukinyanyua, kifanye kazi ili kiweze kuwasaidia kuwaendeleza wananchi kiafya. *(Makofi)*

**MHE. SAID MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, kituo cha afya cha Kitomanga ni miongoni mwa vituo ambavyo Rais aliahidi kukipandisha hadhi na kuwa hospitali ya Wilaya, na kwa kuwa tayari Halmashauri ya Wilaya ya Lindi Vijijini imetenga fedha shilingi milini 40 kwa ajili za wodi za wagonjwa katika eneo hili.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutekeleza ahadi hiyo kwa kukifanya kituo hicho kuwa hospitali kamili ya Wilaya kwa kukamilisha kazi zilizobaki?

**SPIKA**: Swali ni jipya kabisa, lakini kwa sababu Waziri anazunguka sana basi ajibu swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hili eneo analolizungumzia nimefika, anazungumzia eneo linaloitwa Bamvua, hawa wana matatizo. Mbunge ameomba niende katika Wilaya yake, mimi ninamwahidi kwamba nitakwenda kule na nitazungumza na Waziri Mkuchika akiniruhusu nitakwenda kuangalia kituo hicho ili nione.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya, huyu anashughulika na mambo ya maji anahangaika na watu wake pale. Mimi napenda kuwaambia wananchi wa Mchinga wamefanya kazi nzuri ya kumleta mtu wa namna hii mwenye uzoefu mkubwa amefanya kazi katika Chama. Kwa hiyo tutamsaidia kuona jinsi tutakavyosaidia katika hospitali hii anayoizungumzia hapa. *(Makofi)*

Na. 259

**Hospitali ya Rufaa ya Musoma**

**MHE. VINCENT J. NYERERE** aliuliza:-

Wananchi wa Musoma na Mara walichanga na kujenga hospitali katika eneo la Kwangwa:-

Je, ni lini Serikali itaendeleza ujenzi na kumaliza Hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mara ya Kwangwa bado ipo. Hatua mbalimbali za wananchi ili kuchangia ujenzi huo zilianza mwaka 1985. Hata hivyo, pamoja na michango ya wananchi iliyochangwa wakati ule iliyofikia kiasi cha shilingi 47,408,158 zilitosha kufikisha ujenzi wa hospitali hiyo hapo ilipofikia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Mara, uongozi wa Mkoa wa Mara katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 umewasilisha maombi maalum ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo hadi kiwango ambacho kitawezesha kutumika.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri, ningependa kujua kwakuwa Bajeti tayari imeshapita ni kiasi gani sasa kinatolewa kwa ajili ya hospitali hii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**Mheshimiwa Spika, hospitali hii inayozungumziwa hapa ni hospitali ambayo Waziri wa Afya ameizungumzia kwa muda mrefu sana na majibu alieza hapa kwamba ni kazi gani ambazo zinafanyika pale.

Moja ya vitu ambavyo Waziri wa Afya amelizungumzia ni jinsi ya kuangalia namna ya kuendeleza utaratibu ule ule uliotumika kwa maana ya kuchangisha wananchi, kuhakikisha kwamba hela hizi zinapatikana kwa ajili ya kuweza kumalizia kazi zinazofanyika pale.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Mara kwa kazi yao nzuri iliyofanyika pale na kwa mchango wao mkubwa ambao waliufanya pale ndiyo maana tumetafuta hiki kiasi kilichotamkwa hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi nimemwita *RAS* amekuja ofisini jana, nikamwuliza swali hili ambalo Mbunge analiuliza. Je, Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili suala hili kwa sababu walipeleka maombi maalum, mpaka sasa hivi hatujapata majibu kutoka Hazina kwa sababu maombi maalum siyo maombi yanayokuja tu yanakwenda Hazina na Hazina wanatoa kibali ndiyo wanasema kwamba hiki tumekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niahidi hapa kwamba tutaendelea kufuatilia kwa sababu suala hili lipo kwenye maombi maalum na kama nilivyosema ni shilingi bilioni 13 zilizoombwa pale. Tukipata jibu lile tutampelekea Mbunge ili aweze kujua kiasi kilichotengwa. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:**Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kuniona, kwa kuwa tangu mwaka 1985 ni zaidi ya miaka 26 ambao ni umri wa watu ambao wapo Chuo Kikuu, na kwa kuwa, Naibu Waziri amesema kwamba amemwita Mkuu wa Mkoa Ofisini kwake, na kwa kuwa miaka yote hiyo viongozi mbalimbali walikuwa wakiitwa na wanaelezwa mambo kama hayo lakini mpaka leo hospitali hiyo haijajengwa.

Je, Naibu Waziri anasema nini sasa kwa wananchi wa Mkoa wa Mara ambao wamechoka na maneno na kauli hizi kuonesha kwamba sasa Serikali imeji-*commit* ujenzi wa hospitali uanze?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hospitali inayoulizwa hapa, Wabunge wasije wakafikiri kwamba mimi siifahamu, mimi nimekwenda kwenye hospitali hii, wala usije ukafikiri tu kwamba mimi najibu jibu tu hapa!

Mheshimiwa Spika, hospitali hii tunaifahamu ni hospitali ambayo ni *concern* ya Mkoa mzima wa Mara. Kama nilivyosema hapa kuna kazi kubwa sana ambayo imefanyika pale na ukienda ukiona majengo yale utashangaa kazi ambayo imefanyika pale.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea hapa katikati ni kwamba takwimu zile zilikuwa hazipatikani, bahati nzuri kama nilivyoeleza hapa, wala siyo Mkuu wa Mkoa niliyemwita hapa, niliyemwita hapa ni *Region Admnistrative Sectretary* (Katibu Tawala wa Mkoa) ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali anayekaa pale. Na ninataka Mheshimiwa Lugola uniamini ninapokuambia kwamba sasa tumeanza kazi hiyo.

Kazi iliyofanywa na wananchi wa Mkoa wa Mara hatuwezi tukaiacha ikabaki vile vile, panahitaji *leadership* maana yake ni kwamba kwanza tushirikiane na wananchi ili wananchi waendeleze kwa sababu sasa tumeshajua kiasi ambacho kimechangwa. Pili ni kwamba upande wa Serikali sasa kuanza kujua ni kiasi gani kitatumika.

Mheshimiwa Spika, bilioni 13 mimi naweza nikajibu hapa kwamba kuzipata zote kwa wakati mmoja haiwezekani kwa sababu Bajeti imeshapita hapa, lakini tunachojua ni kwamba tutakwenda kidogo kidogo. Mbunge atuamini kwamba sasa tunaanza kufanya kazi hiyo tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya, kuhakikisha kwamba Hospitali ile kwa mawazo mazuri waliyokuwa nayo wananchi wa Mara inajengwa kwa kiwango hicho ambacho wanatarajia. *(Makofi)*

Na. 260

**Hitaji ya Barabara ya Lami Buchosa**

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA** aliuliza**:-**

Kutokana na shughuli ya uvunaji mbao katika msitu wa Buhindi barabara za Jimbo la Buchosa zinaharibika sana kwani hazina ubora wa kuhimili wingi wa magari yanayosomba mbao kutoka msitu huo wa Serikali.

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu na lazima kujenga barabra inayotoka Kahunda hadi Sengerema kwa kiwango cha lami ili kuhimili uzito wa magari yanayopita?

(b) Kwa nini Serikali isianze mipango ya kujenga barabara hiyo kwa kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka huu?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Tizeba, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa fedha, Serikali kwa sasa haiwezi kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Barabara hii kwa sasa ni moja ya

barabara ambazo zinatengenezwa chini ya mpango maalum wa matengenezo (PMMR) kwa Mkoa wa Mwanza.

Chini ya mpango huu barabara hufanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na kuendelea kufanyiwa matengenezo kwa kipindi cha miaka mitano. Ukarabati ulikamilika mwaka 2010. Hata hivyo Wizara yangu itaendelea kuitengeneza barabara hii, ili iendelee kupitika katika kipindi chote kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara. Aidha, nitafuatilia kwa karibu kwa mujibu wa sheria magari yanayozidisha uzito yakiwemo magari yanayobeba mbao kutoka msitu wa Buhindi.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Pamoja na majibu ya Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa umuhimu wa barabara hii Serikali ilikwishautambua kiasi cha kuiweka katika matengenezo ya muda maalum *PMMR* na Waziri alikwishafika Sengerema na akaelezwa Azimio la Baraza la Madiwani la kumfukuza yule Mkandarasi kwa sababu ameshindwa kukidhi masharti yaliyomo katika mkataba wa matengezo hayo ya muda maalum.

(a) Je, sasa Waziri yupo tayari kumfukuza kwa sababu alimpa mwezi mmoja na umeshapita?

(b) Kwa kuwa, suala la ufinyu wa Bajeti ni suala la kibinadamu kwa maana kwamba Wizara ndizo zinazo-*allocate* fedha na siyo barabara zinazojitengea fedha. Je, Serikali ipo tayari ku-*allocate* fedha kwa ajili ya matengezo haya katika mwaka wa fedha ujao?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilieleza barabara ya Buchosa ambayo iliulizwa na Mheshimiwa Mbunge, iko chini ya mradi wa *PMMR* ambapo kwa mradi mzima ulioko katika eneo hili unahusisha barabara ya Geta – Ikome kilomita 44.9, Nyehunge – Kahunda barabara ya Kamanga – Katunguru- Sengerema,- Katunguru – Nzela, Barabara ya Sengerema – Nyamazugo pamoja na barabara ya Nyamililo hadi Bukokwa zote kwa pamoja zina kilomita 208.3.

Barabara hizi zinatengenezwa kwa mpango maalum uliobuniwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, ambao unatekelezwa katika Mikoa mitatu kwa majaribio, Mkoa wa Rukwa, Tanga pamoja na Mkoa wa Mwanza. Kwa bahati mbaya baada ya mradi huu kuanza Benki ya Dunia, ilijitoa kwa hiyo, ikibidi Wizara kushughulikia miradi hii. Katika jibu la msingi nimeeleza kwamba mkandarasi kwa sasa hivi amemaliza katika kipindi cha miaka miwili kwa ajili ya kufanya *rehabilitation*. Katika kipindi cha miaka mitatu inayobaki ataendelea kutengeneza barabara hii ili iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri barabara hii nimeipita wiki iliyopita na kwa bahati nzuri hata mimi nimetoka kule kuna babu zangu kule Katoma, Nzela kote kule ni maeneo yangu. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba barabara

hii tutaendelea kuitengeneza na hakuna sababu ya kumfukuza Mkandarasi kwa sababu anaendelea kufanyakazi zake.

Mkandarasi hafukuzwi na Madiwani kwa sababu siyo Madiwani waliompa kazi pale. Kufukuzwa Kandarasi anafukuzwa kulingana na mikataba iliyoko kama inakiukwa. Tujiepusha kufukuza fukuza tu makandarasi ni lazima Kandarasi anapovunja sheria yake ndipo afukuzwe. Asipofukuzwa na akatimiza wajibu wake ni vizuri kumuenzi na kuhakikisha kumpa nguvu za kufanya kazi zake. (*Makofi*)

Kuhusu suala lingine la kwamba tutahakikishaje kwamba fedha zitaendelea kutolewa nataka kumthibitishia rafiki yangu Dr. Tizeba kwamba fedha kwa ajili ya barabara hii zenye jumla ya kilomita 208 kama nilivyozitaja zitaendelea kutolewa hata katika bajeti inayokuja zitatolewa ili barabara hii iweze kupitika katika kipindi chote. Tunajua maeneo haya ni ya uzalishaji mkubwa.

**SPIKA:** Wanaotaka maswali ya nyongeza wanasimama baada ya jibu kujibiwa kwa mara ya kwanza maana naona wengine mnahamasika na maswali ya nyongeza mnasimama na mimi nawaona mara moja. Kwa hiyo, Njwayo ndio nimekuona wengine sikuwaona.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la barabara lililoko katika Jimbo la Buchosa linafanana kabisa na tatizo la barabara lililoko kati ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi kwamba linapitika kwa shida sana baada ya kuwa na *tonnage* kubwa za korosho zinazopita kwenye barabara hiyo. Na kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ilisema wazi kwamba itafanya mpango wa barabara hii katika miaka mitano ijayo sasa iwe ya lami.

Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuliambia Bunge hili maandalizi ya utekelezaji wa dhana hiyo ya kuwa na barabara lami umefikia kiwango gani hadi sasa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mtwara – Newala hadi Masasi inahudumiwa na Wizara yangu kupitia *TANROAD*. Lakini ni ukweli pia kutokana na uwezo wa Serikali hatuwezi tukatengeneza barabara zote kwa kiwango cha lami.

Kupanga ni kuchagua kwa sasa hivi tumejikita zaidi katika kutengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Masasi, Tunduru, Namtumbo, Songea hadi *Mbamba Bay* na barabara zingine zikiwemo za Dodoma kwenda Iringa, Dodoma kwenda Babati na sehemu zingine. Tukishamaliza hizi kwa sababu miaka mitano bado haijaisha ndipo tunaweza kuanza kupanga mipango mingine ya kuanza kufanya *feasibility study* na *details design* kwa kiwango cha lami kwa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Na. 261

**Mizani Kubwa Katika Vituo vya Sumbawanga na Makambako**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Mwitikio mzuri wa Kilimo Kwanza kwa wananchi ni pamoja na kuhakikishiwa soko la uhakika lisilokuwa na usumbufu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufunga mizani (*weighbridge*) katika Vituo vya Sumbawanga na Makambako ili kuondoa usumbufu na msururu mrefu wa magari wakati wa ununuzi wa mazao/mahindi na wakati wa usafirishaji wa mahindi?

**WAZIRI WA UJENZI** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Serikali ina mpango wa kujenga mizani (*weighbridges*) katika miradi mitatu inayoendelea ya barabara ya Tunduma – Sumbawanga, Sumbawanga – Mpanda na Sumbawanga – Matai.

Mheshimiwa Spika, kituo cha mizani kwa upande wa Makambako kipo tangu mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990). Nakubaliana sana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa pamoja na kuubadili mizani huu kuwa wa *computer* bado kituo hiki kinakabiliwa na tatizo la msongamano unaosababishwa na ongezeko la magari *(traffic volume)* kwenye barabara hii. Ili kukabiliana na tatizo hili Wizara inatafuta fedha za kujenga mizani nyingine upande wa pili wa barabara.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwanza naomba nishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa ujenzi wa barabara za lami kwa kiwango cha lami kwa Mkoa wa Rukwa. Lakini pia nina maswali maswali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika swali la msingi nilikuwa nauliza jinsi gani ambavyo Serikali itapunguza adha kwa wananchi wakati wa ununuzi wa mahindi na usafirishaji?

Lakini pia kwa kuwa Serikali imepiga marufuku utoaji wa chakula nje ya nchi ambao kwa kiwango kikubwa ilikuwa imeshaanza kupandisha bei kwa wakulima wa mahindi nao wakaona ni kipindi chao cha kupata mavuno kwa maana ya kiwango cha fedha.

Je, Serikali itaanza kununua mahindi kwa kiasi gani kwa maana ya bei?

**SPIKA:** Hilo la kwanza halimhusu huyu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Swali la msingi lilikuwa limelenga katika kupunguza adha ya ununuzi wa mahindi kwa hiyo, lilikuwa linakwenda kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hii *sasa* ni barabara mahindi ni matokeo tu sasa ukimwuliza swali la mahindi Waziri wa Ujenzi, umempa majaribu kabisa. Endelea kuuliza swali. Hatukukuelewa maswali yako yote mawili anza upya. Mwelekeze Waziri wa Ujenzi siyo mahindi.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kujua sasa barabara hizi za kiwango cha lami kutoka Sumbawanga mpaka Tunduma zitakamilika lini, hali kadhalika kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga? Ahsante sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Kandege kwa maswali yake. Ni kweli kabisa kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, yenye jumla kilomita 231 inajengwa kwa kiwango cha lami. Mkandarasi yuko kule chini ya mradi wa *MCC* unaofadhiliwa na Marekani.

Mkataba ni katika kipindi cha miezi 32 na mkandarasi katika hiyo, sehemu ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, anaendelea vizuri amefikia karibu asilimia 20. Katika sehemu ya kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga ambapo ina jumla ya kilomita 112 na hapo kuna Wakandarasi wawili wamegawanywa katika sehemu mbili za kutengeneza kwa kiwango cha lami.

Lakini siyo hilo tu, pia kutoka Sumbawanga kwenda Kibaoni ambapo kuna zaidi ya kilomita 150 napo kuna makandarasi. Nataka kumthibishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Rukwa kwamba barabara ambazo zimeshaanza kujenga katika Mkoa wa Rukwa, zitakamilika kulingana na mkataba na zitakamilika kwa kiwango cha lami.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa umezalisha mahindi mengi na yanahitajika kusafirishwa kupelekwa mahali ambapo kuna matatizo ya chakula nchini. Mahindi mengi yamerundikana Mpanda na usafiri ni reli na barabara. Barabara iko katika hali mbaya.

Je, Serikali sasa iko tayari kufanya matengenezo ya dharura katika maeneo yaliyoharibika katika barabara itokayo Mpanda, Sikonge hadi Tabora?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga kikamilifu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kuanza matengenezo ya barabara zote zilizo chini ya *TANROAD*. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge, kuwa tutatengeneza hizo barabara ikiwa ni pamoja na barabara hiyo ya kwenda Sikonge ili iweze kupitika kikamilifu. Ninachomwomba ajiandae tu vizuri kupitisha Bajeti yangu nitakapoileta kwenye Bunge ili kusudi fedha za Mfuko wa Barabara ziweze kutumika kutengeneza barabara hizo.

Na. 262

**Kupandisha Hadhi Barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Mlingano – Mashena**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Kutokana na umuhimu wa barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Mlingano – Mashena kuunganisha majimbo matato matatu ya Mlalo, Lushoto na Bumbuli na pia kuhudumia wananchi zaidi ya laki moja, Mkoa uliomba barabara hiyo ipandishwe hadhi ili isimamiwe na *TANROADS* kwa sababu Halmashauri haina uwezo wa kuihudumia barabara hiyo:-

(a)Je, ni sababu zipi zilifanya Serikali isiyakubali mapendekezo ya kuipandisha hadhi barabara hiyo ili ihudumiwe na *TANROADS*?

(b)Haja ya kupandisha hadhi barabara hiyo, bado iko palepale. Je, ni lini sasa azma hiyo itatekelezwa?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry D. Shekiffu Mbunge wa Lushoto, lenye kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imeweka vigezo vya kupandisha madaraja barabara zake kwa mujibu wa sheria ya barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009. Kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika sheria hiyo, barabara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Mashena haikukidhi vigezo na hivyo itaendelea kusimamiwa na TAMISEMI kwa kutumia fedha zinazotengwa kwenye Halmashauri husika. Aidha, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa katika Wilaya ya Lushoto Serikali, imepandisha hadhi barabara ya Mlalo – Mng'aro yenye urefu wa kilometa 18 kuwa ya Mkoa ambapo inahudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa barabara (*TANROADS*).

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Katika swali langu la msingi niliuliza ni vigezo gani ambavyo barabara hii haikukidhi ili kupandishwa hadhi. Kwa bahati mbaya vigezo hivyo havikutajwa.

(a) Je, Waziri atakubaliana nami kwamba anaweza kunipa vigezo hivyo angalau hata kwa maandishi ili tutakapoomba tena basi tuvitimize?

(b) Kwa kuwa barabara hii ni muhimu na inahudumia majimbo matatu na inakwenda mpaka Mashewa – inakwenda mpaka Magoma kwenda Tanga na ni njia ya mkato. Je, Waziri atakubaliana nami sasa kwamba tukipeleka maombi ataliangalia suala hili kwa msingi unaostahili na iweze kupata kibali?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwamba vigezo vinavyotumika ni kwa mujibu wa sheria Namba 13 ya mwaka 2007 na *Regulations* zake za mwaka 2009. Nikimaliza Bunge nitampa nakala za vigezo hivyo Mheshimiwa Shekiffu, ili aweze kuvipitia ili kujua ni vigezo gani vinavyotumika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba sasa hivi ikiletwa itakuwa tunaweza tukachukua, katika mwaka uliopita barabara zilizokuwa za Halmashauri ambazo zilipandishwa hadhi zilikuwa zaidi ya kilomita 3000 na kitu na kwa bahati mbaya barabara zote ambazo zilipandishwa hadhi hazikuweza kupata fedha kwa ajili ya matengenezo. Kwa mwaka huu ndio tumeziwekea fedha kwa ajili ya matengenezo. Fedha hazitoshi. Lakini kwa sababu fedha za mfuko wa barabara zinagawanywa kwenye Halmashauri na zingine zinapelekwa *TANROAD.* Sisi tunaamini kabisa kwamba Halmashauri ya Lushoto ikiomba *special fund* kwa ajili ya barabara husika kwa kupitia Mfuko wa *Road Fund* wanaweza wakapelekewa hizo fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo kupitia Halmashauri inayohusika. (*Makofi*)

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya Shelui – Mtoa – Mtekente mpaka Urugu kwenda Kibaya ilishapendekezwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa kwamba ipandishwe hadhi kuwa wakala wa barabara wa Mkoa na ndio barabara ambayo inahudumia zaidi ya robo tatu ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi na inabeba uchumi wa zaidi ya robo tatu wa Iramba.

Je, Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari sasa atakapopandisha barabara zingine kuipandisha na hii ikiwepo na ile ya Tulia ambapo ndiyo kuna uvuvi kwa Jimbo la Iramba Magharibi? (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali jipya sana, lakini kwa sababu ya ujuzi wa Waziri nampa ajibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara zinazohudumiwa na Wizara yangu kwa kupitia *TANROAD* ni zaidi ya kilomita 30,000 katika nchi nzima. Lakini kuna karibu pia kilomita 50,000 ambazo zinahudumiwa na Halmashauri za Wilaya. Ni Bunge hili ndilo lililopanga kwamba fedha kiasi fulani zinapelekwa *TANROAD* na fedha kiasi fulani zinapelekwa Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya kuhudumia mfuko wa barabara.

Sasa ni kweli kwamba Wabunge wengi kwa sababu ya kazi nzuri zinazofanywa na *TANROAD* kila Mbunge anapenda barabara za Halmashauri za Wilaya zihamishwe zipandishwe daraja zikawe za Mkoa. Lakini kupanga ni kuchagua tunapohamisha zile barabara fedha zinabaki kule kule kwa hiyo, napenda kutoa wito kwamba kwa Halmashauri za Wilaya zinazohusika ni vema sasa zikaanza kutumia vizuri fedha zao zinazopangwa kule za *Road Fund* katika kuhakikisha barabara zinazowahusu zinatengenezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Kwa barabara ya Mheshimiwa Mchemba nataka kusema kwa dhati kwamba nao waombe fedha za kutosha kwa kupitia Mfuko wa Barabara, ili barabara hii

inayosimamiwa na Halmashauri iweze kutengenezwa kwa kiwango kinachotakiwa. Halmashauri zisikwepe majukumu yao ya kutengeneza fedha.

Kwa mujibu wa sheria namba 98 *amendment act* namba 2 ya mwaka 1998, fedha za barabara zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya zinatakiwa zitumike kwa ajili ya matengenezo ya barabara tu si kwa kazi zingine.

Kwa hiyo, Halmashauri ziwajibike kuhakikisha barabara zote zinatengenezwa kulingana na sheria ya fedha za Mfuko wa Barabara. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wanaojibu maswali naomba wakae *front bench* hapa kwa sababu mnafanya Spika asielewe nani anayejibu. Wote wanaohusika na maswali wakae *front bench. (Makofi)*

Na. 263

**Ahadi ya Kuchimba Bwawa Chikuyu kwa Umwagiliaji**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2010 Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi kwa wananchi wa Kijiji cha Mbwawa, katika kata ya Chikuyu kuwa atawachimbia bwana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji:-

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa kwa wananchi wa Kijiji cha Mbwasa, katika Kata ya Chikuyu, Wizara yangu iliwatuma wataalam wa umwagiliaji kutoka Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kati, kufanya utafiti wa kitalaam katika eneo hilo kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, watalaam wa umwagiliaji kwa kushirikiana na watalaam wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, wamefanya utafiti wa awali kuhusu uwezekano wa kujenga bwawa la kuvuna na kuhifadhi maji katika Kijiji cha Mbwasa, kwa ajili ya umwagiliaji. Utafiti huo umebainisha kuwa Bonde la Makunguu ambalo lipo umbali wa kilometa 6 kutoka Kijiji cha Mbwasa, linaweza kuhifadhi maji kwa kujenga tuta la bwawa katika eneo linalofahamika kama makazi ya nyani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, imetenga shilingi milioni 25 kupitia *Capital Development Grant* na Mfuko wa *Tanzania Japan Food Aid Counterpart Fund* tayari umetenga shilingi milioni 200 kwa

ajili ya mradi huo. Aidha, Wizara yangu kupitia ofisi ya umwagiliaji Kanda ya Kati, imeandaa hadidu za rejea ambazo zitawasilishwa Wilayani Manyoni, kwa ajili ya itifaki ya kutangaza ili kumpata mtalaam mshauri ambaye atafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa bwawa hilo, hatua ambayo itatupatia gharama halisi ya ujenzi wa bwawa. Aidha, Ofisi ya umwagiliaji ya kanda ya kati, itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, katika kuandaa andiko la kuombea fedha mradi huo kwa ajili ya utekelezaji kutoka Mfuko wa kuendeleza umwagiliaji ngazi ya Wilaya. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameonyesha jitihada za Halmashauri na jitihada za Serikali kwa kutenga fedha.

(a) Je, anaweza akawaambia nini wananchi wa Mbwasa kwamba kazi hii itaanza lini na itakamilika lini? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ameonyesha kwamba bwawa hili ni kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Je, anaweza akatueleza bwawa hilo litaweza kuwa na matumizi mengine kama ya kunyweshea mifugo na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHURIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika labda nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Chilolo, nakumbuka swali hili, nilijibu swali linalofanana na hili ambalo lililetwa na Mheshimiwa Chiligati na nikawahakikishia wananchi wa Mbwasa kwamba baada ya ufuatiliaji wa karibu wa Waheshimiwa Wabunge wote hawa wawili, Serikali tayari imeshachua taratibu za kulijenga bwawa hilo. Kwa hiyo sasa tunachokifanya ni kuandaa *design* na kuandaa makadirio ya gharama.

Kwa hiyo, katika msimu huu tutafanya kazi hiyo na baada ya kupitisha Bajeti hii shughuli hizo zitaanza. Hatua itakayofuata ni ya ujenzi wa bwawa lenyewe. Nina hakika kufikia msimu au mwaka wa fedha unaokuja bwawa litakuwa limekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Chilolo kwamba migogoro mara nyingi inayojitokeza kati ya wakulima na wafugaji ni mikubwa na maji ni sehemu moja wapo. Kwa hiyo, mabwawa yetu tunayoyajenga hivi sasa, tunayajenga ili yaweze kukidhi mahitaji ya kilimo wakati huo huo tunaweka na mabirika ya kunyweshea mifugo na ikiwezekana pia tunaweka na matoleo ya maji ya kunywa ili wananchi hao hao waweze kupata huduma hizo kwa mara moja na kuipunguzia Serikali gharama za kuanzisha miradi ya kila aina wa kuhudumia mtu huyo huyo mmoja mmoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa mafanikio ya kilimo chetu hapa Tanzania kitategemea sana mipango ya kilimo cha umwagiliaji na hiyo ni dhana ya uhakika kabisa.

Je, Serikali imejipanga kwa kiasi gani katika kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinahifadhiwa kwa kiwango kikubwa ili kuhakikisha kwamba mabwawa mengi yanajengwa na kilimo cha umwagiliaji kinakuwa endelevu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Ngoye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kama tutakumbuka mwaka 2009 tulipitisha Sheria Na. 11 ya Rasilimali za Maji, sheria hii ndiyo inayotusaidia kulinda vyanzo vya maji, iwe ya umwagiliaji, maji ya kunywa na hata ya chepechepe.

Kwa hiyo, sheria hiyo ipo tayari, hiyo ni njia moja wapo ambayo imetufanya tujipange kulinda vyanzo vya maji kilichobaki ni kuitekeleza maana kuweka sheria pekee yake bila kuitekeleza, hilo nalo ni tatizo. Lakini pia tatizo lingine liko kwenye ngazi ya chini, tunapokuwa na *by-laws* kwenye ngazi ya vijiji na *by-laws* zile zisiposimamiwa, ni rahisi kabisa kuweza kuharibu vyanzo vya maji.

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba sio Serikali tu kwenye ngazi ya Serikali Kuu, lazima tushirikiane kuanzia kwenye ngazi za chini mpaka juu.

Lakini nimalizie kwa kusema kwamba katika Mpango wa Maendeleo ambao tuliusoma humu ndani hivi karibuni, tukaupitisha, ukiusoma vizuri utaona Serikali imejipanga vizuri kujenga mabwawa 33 hususan katika maeneo haya yenye mvua haba kwa ajili ya kuvuna maji. Hilo ni kwa ajili ya kujipanga vizuri ili tuhakikishe kwamba maji yanapatikana kwa wakati wote na katika maeneo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Na. 264

**Shamba la Mpira la Mang'ula**

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE** aliuliza:-

Shamba la mpira la Mang'ula Kalunga halijaendelezwa kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza shamba hilo?

(b) Je, mmiliki wa shamba hilo ni nani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba la mpira la Kalunga, lililoko Mang'ula katika Wilaya ya Kilombero ni moja kati ya mashamba yalioanzishwa na Serikali mwaka 1978 kupitia kampuni ya *General Tyre East African Limited* kwa lengo la kuzalisha malighafi ya kiwanda hicho. Shamba lingine ni lile la Kihuwi lililoko Muheza. Kwa nyakati tofauti katika ya mwaka 1995 na 2005, mashamba hayo yalikuwa yanalimwa kwa kukodishwa na makampuni ya *Macintyre Flatters Limited* ya Kenya, *Jumamosi L. Ardhi Limited* ya Tanzania ambayo yote yalishindwa kuyaendeleza.

Mwaka 2006 Serikali iliyaweka mashamba hayo katika mchakato wa ubinafsishaji lakini mwisho wa mwaka 2008 Serikali iliamua kusimamisha zoezi la ubinafsishaji kwa mashamba hayo na kuyakabidhi kwa Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC).* Mwaka 2009 *NDC* iliingia mkataba ya kampuni ya *Coast Water Project Limited* hadi Disemba 2011 kwa lengo la kutunza mashamba hayo wakati mkakati mpya wa kuyaendeleza unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mashamba ya mpira hayaendelezwi kama ilivyotarajiwa. Kwa mfano shamba hilo la Kalunga lenye ukubwa wa hekta 752.4 hivi sasa limepandwa mpira. eneo la hekta 170 tu. Maeneo yaliyobaki bila kuendelezwa yamekwisha vamiwa na wananchi ambao nao tayari wameyaendeleza kwa kupanda mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua ili kuhakikisha kwamba mashamba ya mpira na mengine yanaendelezwa na ardhi inatumika kuwanufaisha wananchi kama ilivyo kusudiwa. Aidha Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Shirika la *Consolidated Holdings Cooperation* imefanya mapitio ya mashamba yote na umiliki wake kwa lengo la kumshauri Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kufuta Hati Miliki za ardhi.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri hili jibu lako halifanani na uliyotupa sisi. Kwa hiyo, sina uhakika na Mheshimiwa Rwakatare ana jibu gani.

**MHE. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, aliniletea jibu lingine kwa hivyo nina majibu mawili. (*Kicheko*)

**SPIKA**: Halifanani kabisa, sasa naomba uulize tu vile vile kama unavyojua.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

Majibu ya swali langu amenipa, mimi amenipa jamani hayo aliyosoma amenipa na nimeridhika nayo. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Mchungaji unanisikiliza mimi siyo mtu mwingine yeyote hapa ukumbini, endelea.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa sababu sasa imekwishakudhibitika ya kwamba zao la mpira mahali pale halitaendelezwa tena na huu mlolongo wanaochukua ni mrefu mno utoke *Consolidated Holdings*, uende Wizara ya Ardhi, uende kwa Rais, halafu urudi tena kwa nini wasiachie kazi hii Halmashauri ya Kilombera ili wananchi hawa wapate kugawiwa mashamba haya ili walime zao ambalo litaweza kusaidia dhana aa Kilimo Kwanza kama mpunga au labda miwa mahali pale ni tepetepe panahitaji mazao kama haya?

(ii) Mheshimiwa Spika, akina mama wa Wilaya ya Kilombero wamezuiwa kuokota kuni katika hifadhi ya Oldzungwa na *TANAPA* tangu tarehe 30, Juni, 2011 sasa akina mama hawa wameachwa bila nishati mbadala ya kuweza kupikia ubwawa na vyakula vingine.

Je, Mheshimiwa Waziri ataruhusu akina mama hawa angalau waokote kuni katika shamba hili kabla hawajafanikisha hayo mambo yaliyokuwa kwenye mpango mrefu?

**SPIKA**: Hilo shamba ni hilo hilo la mazao ya mpira au lingine?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwanza kabla ya kujibu naomba radhi na naomba nikuhakikishie kwamba majibu haya niliyosoma nilikwisha wasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge na ndiyo maana ame- *insist* kwamba anayo majibu sahihi niliyosoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza tayari Serikali imekwishapitia hatua hiyo, shamba linapokuwa lina umiliki wa ardhi namna ya kuondoa ule umiliki, huwezi kwenda tu moja kwa moja Halmashauri ikaanza kuondoa ule umiliki. Ndiyo maana tumefuata huo mlolongo mrefu. Tayari vikao vimekwishafuatwa kuanzia ngazi ya kijiji, *ODC* imeshakaa na kadhalika.

Mkoani wamekwishakaa na wamekwisha wasilisha maombi yao kwenye Wizara ya Ardhi na maombi hayo tayari yamekwisha fanyiwa kazi. Sasa huwezi ukabadilisha tu matumizi ya ardhi bila kumhusisha mwenyewe mwenye dhamana, ndiyo maana

nimesema hatua inayofuata sasa inapelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aweze kutoa uamuzi wa kubadilisha Hatimiliki.

Mimi naamini kabisa kwamba hatua tuliyoifikia sasa ni nzuri. Suala hilo litatekelezwa muda sio mrefu kwa sababu ngazi zote zilizokuwa zinafanyia kazi, tayari zimemaliza kazi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, nimelisikiliza vizuri, mimi niseme tu kwamba kwenye mashamba ya mpira kuokota vikonyo vilivyo katika, vimeanguka chini sidhani kama kuna tatizo kama hilo wala sidhani kama kuna mtu anazuiwa kuokota mabaki ya miti ambayo yameanguka, labda kitakachokatazwa ni kukata ile miti ya mipira yenyewe kwa sababu ukifanya hivyo, utakuwa umefanya kosa kwa kukata mazao ambayo tayari yana miliki nyingine.

Mimi sidhani kama akina mama wakiokota tu kuni watazuiliwa, nadhani hilo ni suala ambalo linaweza kuangaliwa katika ngazi ile ya Halmashauri na mamlaka zingine zinazofuata.

Na. 265

**Ugonjwa wa Saratani**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF (K.n.y. ZAHRA ALI HAMAD)**aliuliza:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti na kugundua kuwa ni sababu gani zimesababisha ugonjwa wa saratani kuwakumba zaidi Wanawake?

(b) Je, ni saratani ya aina gani inayosumbua zaidi Wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, nomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa taarifa tulizonazo, wagonjwa wengi wa saratani ni wanawake. Sababu moja kubwa inayochangia wanawake kuwa wengi kuliko wanaume ni kwamba zipo aina za saratani ambazo zinawapata wanawake pekee kutokana na maumbile yao.

Baadhi ya saratani hizo ni saratani ya shingo ya kizazi, nyumba ya uzazi, matiti, kubeba mimba ambazo si timilifu *(Gestation Trophoblastic Diseases)* na kadhalika. Sababu nyingine ni kwamba kwa kawaida wanawake wakiumwa ni wepesi kutafuta ushauri wa Daktari kuliko wanaume.

Kutokana na tabia hiyo, ni rahisi zaidi kupata taarifa za magonjwa ya wanawke ikiwa ni pamoja na saratani. Wanaume wako radhi kuwapeleka wake zao hospitalini wanapoumwa lakini wao wenyewe siyo wepesi wa kutafuta ushauri wa Daktari kama walivyo wanawake.

Kutokana na tabia hiyo, ni rahisi zaidi kupata taarifa za magonjwa ya wanawake ikiwa ni pamoja na saratani. Wanaume wako radhi kuwapeleka wake zao hospitalini wanapouumwa lakini wao wenyewe si wepesi wa kutafuta ushauri wa daktari.

(b) Mheshimiwa Spika, saratasi ya shingo ya kizazi ndiyo saratani inayosumbua sana wengi na wanawake kwa wingi zaidi nchini Tanzania kuliko saratani zingine zote. Tatizo hili ni mara tano zaidi kuliko hata tatizo la saratani ya matiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uzito wa tatizo hili, Serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha mpango wa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi, kuongeza uwezo wa kuitambua mapema, pamoja na kuboresha matibabu yake kwa wale ambao wameshaathirika na ugonjwa huu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina mswali mawili ya nyongeza:-

(i) Katika kukabili saratani ya shingo ya kizazi, Serikali iko katika mchakato wa kuanzisha chanjo. Je namwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, hiyo chanjo itaanza lini? *(Makofi)*

(ii) Katika hospitali ya *Ocean Road* inayohusiana na saratani iko katika hali mbaya sana. Ninaelewa kuwa Serikali imeanzisha ujenzi wa jengo jipya litakalochukua wagonjwa karibu 170. Je, jengo hilo litamalizika lini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumejipanga kwa ajili ya kuanza chanjo ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi na gharama za kufanya hiyo shughuli zinategemeana na wafadhili wawili ambao niliwataja wakati najibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

Mheshimiwa Spika, tumeshaanza kujipanga, tutaanza lini *exactly* siwezi kumweleza Mheshimiwa Mbunge leo hii ila naomba anipemuda niwasiliane na wafadhili kwamba wameshajipanga kwa kiasi gani, pesa zitaingia lini Mheshimiwa Mbunge nitakuletea jibu kwa maandishi. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya malazi ya *Ocean Road*, ni kweli kuko *over crowded* na ni kwa sababu ndiyo hospitali pekee katika Taifa letu hili inayohudimia wagonjwa wa saratani. Maana yake kwa kuwa na matibabu ya mionzi ambayo hayako katika hospitali nyingine yoyote ya rufaa hapa nchini.

Lakini kwa sasa hivi tunajipanga vizuri tu tutaanza matibabu ya saratani katika hospitali ya Bungando, *KCMC* na hospitali ya Mbeya. Tukianza hiyo, nafikiri tutapunguza msongamano, jengo hili litamalizika katika mwaka huu wa fedha ikitegemeana na kwamba hakutakuwepo tena na mwendelezo wa *inflation*.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa ahsante sana kwa kuniona. Swali langu la nyongeza linalenga kuwa wanawake wengi ndiyo waathirika wakuu wa maradhi haya ya saratani hapa nchini.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kutoa elimu hii kwa watoto, na hasa wasichana na wavulana walioko mashuleni na kuweza kuwafikia wanawake wote walioko vijijini, ni jinsi gani ya kutambua dalili za *cancer* na tiba inakopatikana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Pwani kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze kwa sababu ni mwana harakati mkubwa sana wa afya za wanawake na vijana katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ili uweze kupambana na maradhi ya aina yeyote, ni lazima tutoe elimu, naomba nimhakikishie kwamba kama Wizara kupitia kitengo chetu cha kuzuia maradhi cha *prevention*, tumeanza mkakati wa kutengeneza vijarida ili tuweze kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia ya redio pamoja na kuvisambaza.

Lakini kwa sababu chanjo hii inatolewa kwa wasichana ambao wako mashuleni kwenye shule za sekondari na ninaona kwamba itabidi tuteremke kwenye darasa la saba na la sita ili tuweze kuwa-*cover* wanawake walio wengi. Chanjo itakwenda sambamba na elimu kwa sababu huwezi kumchanja mtu bila kumpa elimu.

Wavulana tutawapa elimu ili waone umuhimu kwamba watakapokuja kuwa na wake zao waweze kuwashawishi kwenda kufanyiwa uchunguzi ambao nafikiri kila daktari wa Tanzania ana uwezo wa kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi.

Na. 266

**Umeme Unaotokana na Makaa ya Mawe**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

*TANCOAL* wanatarajia kuanza mradi mkubwa wa kufua umeme kutokanana makaa ya mawe:-

(a) Kwa nini Serikali haiwekezi zaidi katika kampuni hiyo ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo kwa kuzingatia matatizo makubwa ya umeme tuliyonayo nchini?

(b) Kwa kuzingtaia kuwa hakuna kijiji chochote ukiondoa mji wa Mbinga kinachopata umeme.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuielekeza kampuni hiyo kupeleka umeme kwenye vijiji vya Kata za Ruanda, Namizwea, Matiri na Wilaya yote ya Mbinga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *NDC* iliingia ubia na kampuni ya *Pacific Corporation East Africa Ltd.* na kuunda kampuni ya *TANCOAL* ambapo *NDC* inamiliki asilimia 30 na *Pacific Corporation* imaliki asilimia 70.

Kampuni *TANCOAL* imewasilisha maombi ya leseni ya uchimbaji madini (makaa ya mawe) Wizara ya Nishati na Madini tarehe 12 Februari, 2011 kwa lengo la kuanza kutekeleza mradi wa kuchimba madini hayo. Taratibu za kutoa leseni ya uchimbaji madini zinaendelea.

Kinachoendelea hivi sasa ni maandalizi ya mradi yakiwemo matengenezo, kuchonga barabara (*acess road*) zitakazotumika wakati wa utekelezaji wa mradi pamoja

na kukamilisha hatua za kupata kibali cha mazingira kitakachowezesha *TANCOAL* kupata leseni ya uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo aliyoyata Mheshimiwa Mbunge, yamepangiwa kufikishiwa umeme wa gridi kupitia Mradi wa Makambako-Songea, unaohusisha upanuzi wa Gridi ya Taifa kutoka msongo wa kilovoti 132 Makambako hadi Songea umbali wa kilimota 250 na utakwenda Songea lakini pia usambaza umeme katika maeneo ya Wilaya za Ludewa, Namtumbo, Songea pamoja na maeneo hayo ya Wilaya ya Mbinga aliyoyataja. Maandalizi ya umilikishwaji wa maeneo ya ujenzi wa vituo vya kupoozea umeme vya Madaba na Songea, pamoja na kulipa gharama za uthamini kwenye Halmashauri husika yanaendelea. Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa Mradi huo, alipatikana mwezi Juni, 2011 na ataanza kazi mwezi ujao wa Agosti, 2011. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015. Kazi atakazozifanya mwaka huu ni kutayarisha zabuni za kuwapata wakandarasi wengine watakaojenga Mradi katika hatua zingine.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwanza ni masahihisho; mimi ni Mbunge wa Mbinga Mashariki siyo Magharibi. La pili, ninasikitika kusema kwamba, maswali yangu yote (a) na (b) hayajajibiwa. Kwa hiyo, ninasita kuuliza swali la nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hukumsikia vizuri. Ninaomba urudie Mheshimiwa Kayombo, hakukusikia vizuri.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Nimesema kwamba, mimi ni Mbunge wa Mbinga Mashariki, siyo Magharibi na maswali yangu yote (a) na (b) hayakupata majibu ya Serikali. Kwa hiyo, ninasita kuuliza swali la nyongeza.

**SPIKA:** Hajauliza swali la nyongeza tunaendelea. Amekasirika sana hakujibiwa sasa aulize nini cha nyongeza.

Na. 267

**Wawekezaji Katika Madini – Rukwa**

**MHE. ABIA M. NYABAKARI** aliuliza:-

Katika Mkoa wa Rukwa kuna madini mengi ikiwemo *Ruby*, Dhahabu, *Emerald* na kadhalika; Madini ya Rubi (Bama Rubi) yanapatikana huko India lakini yameshachimbwa na kuisha:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuchimba madini hayo yenye thamani kubwa kwa kushirikiana na Wananchi wa Rukwa?

(b) Je, kwa nini Serikali haitafuti wawekezaji katika madini ili washirikiane na Wananchi wa Rukwa kwa lengo la kuwainua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mkoa wa Rukwa una madini mbalimbali katika maeneo mengi ya Mkoa huo. Kulingana na jiolojia ya Mkoa huo na tafiti zilizokwishafanyika muda mrefu hapo nyuma, imebainika kuwepo kwa Madini ya Dhahabu, Shaba, Risasi, Nikeli, Chromite, Ulanga, Manganese, Makaa ya Mawe, *Tungsten* na *Wolfromite.* Uchimbaji wa madini hayo unaweza kufanywa kupitia uchimbaji mdogo na wa kati. Hata hivyo, utafutaji wa kina unahitajika katika maeneo mengi ili kujua kiasi cha mashapo ya madini yaliyopo katika maeneo yenye madini hayo yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Hatua hii ni muhimu kabla ya kufanya uamuzi wa kuwekeza katika Mradi wa Madini hususan uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini ya Mwaka 2009, imeeleza bayana kuwa, Serikali itakuwa ni mhamasishaji, msimamizi na mdhibiti wa shughuli za madini na inaweza kuwekeza kimkakati kwenye baadhi ya Miradi ya Madini kupitia *STAMICO.* Hadi sasa Serikali haina Mradi wowote wa utafutaji madini Mkoani Rukwa kupitia *STAMICO.* Ni vigumu kuanzisha uchimbaji katika eneo lolote bila kulifanyia utafutaji wa kina wa madini husika. Serikali haina mpango wowote wa kuchimba madini katika Mkoa wa Rukwa katika maeneo ambayo *STAMICO* haina leseni, bali itaendelea kuhamasisha wawekezaji binafsi wa ndani hasa kutoka Mkoa wa Rukwa ili waweze kuwekeza kwa kushirikiana na wawekezaji wengine kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, Serikali imeweka mazingira ya kuwavutia wawekezaji binafsi katika Sekta ya Madini ili wawekeze katika utafutaji madini kwa lengo la kugundua madini yanayoweza kuchimbwa kwa faida. Pia Serikali kwa kupitia Shirika la Madini la Taifa la *(STAMICO),* inaweza kuingia ubia na wawekezaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Taifa linanufaika na uchimbaji wa madini katika Miradi hiyo.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, kufuatana na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, inaonekana kabisa kwamba, katika Mkoa wa Rukwa hakuna rubi wala *emerald,* lakini Wananchi hawa wanaendelea kuchimba kila kukicha na wanapata kidogo kidogo.

(i) Je, Serikali ipo tayari kuwaambia kwamba zile ramani zilizotolewa zinazoonesha kwamba hapa ni njia ya ruby na hapa ni njia *emerald* kwamba ni batili?

(ii) Waziri fulani alipita pale akaongea na kile kikundi; kuna kikundi kimoja kipo Sumbawanga Mjini akawaambia kwamba wako tayari kuwasaidia kama Serikali. Kikundi hiki mpaka sasa hakijaweza kupata hata senti tano. Je, Serikali inaingiza siasa na utekelezaji katika mambo ya maendeleo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwenye majibu yangu nimesema kwamba, Serikali inatambua. Kwa sababu utafiti uliofanywa Mkoa wa Rukwa kusema kweli uchimbaji Mkoani Rukwa umeanza miaka ya 1950, lakini ulikuwa uchimbaji wa kati umesimama. Sasa kwenye haya madini mengine niliyokutajia kama nikeli, shaba na makaa ya mawe, yapo. Umenizungumzia vito, rubi, *emerald*, haya madini yapo Tanzania nzima; yapo kwa wingi kule Tunduru kwa Mheshimiwa Abdallah Mtutura; yapo Masasi huku chini kwenda Wilaya ya Newala; na yapo mitaa ya Tanga kule Kilindi. Sasa ninachosema ni kwamba, siyo kwamba, tumehamasisha vikundi kwenye uchimbaji mdogo, lakini tunarajia tuvihudumie kupitia Mfuko wa Wachimbaji Wadogo. Serikali inatoa leseni na inaweka mazingira wezeshi ili watakapokuja wawezeshaji, ambao ni wawekezaji wenye uwezo mkubwa zaidi, tunawapeleka huko na ndivyo tunavyofanya hivyo.

Sasa kama wewe unawafahamu wachimbaji ambao wana leseni hizi na wanahitaji kuingia kwenye ubia, kusema kweli tumejaribu sana kuunganisha watu pale Wizarani na kuna baadhi ya maeneo kama Kilindi na wapi tumewasukuma huko. Hili ni jambo ambalo tunalifanya na tutaendelea kulifanya na kama wapo kwa upande wa Rukwa, mimi ninakuomba tukutane ili tuangalie namna Wizara inavyoweza kukusaidia katika hili.

Hili la pili la kikundi cha uwezeshaji; vikundi hivi vipo vingi. Vipo vikundi ambavyo tumehamasisha vikae katika vikundi vya wachimbaji wadogo ili waweze kufaidika na mikopo midogo midogo na kadhalika. Sasa siyo Serikali yenyewe itakayoingia kusema inatoa pesa kupeleka kwenye kikundi fulani hapana, lakini tunatengeneza mazingira ili vikundi kama hivyo, vikijitengeneza vikawa na leseni, sisi tunaweza kuwaelekeza kwa wawekezaji au tunaweza tukawaelekeza kwenye mabenki waweze kukopa kama wanakopesheka kulingana na ule Mradi wenyewe pale na pia vigezo vitakavyotumika na mabenki.

**SPIKA:** Jamani, maswali yamekwisha na muda pia umepita. Sasa ninaomba niwatangaze wageni.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Au unaniongoza mimi kuhusu nini? Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68, kifungu cha 7 inasema; “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au aruhusiwe kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge.”

**SPIKA:** Jambo gani lilitokea?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, jana wakati Waziri Mkuu, anaongelea suala la Wizara ya Nishati na Madini na kusema kwamba, amesikiliza ushauri wa Wabunge na wameona warejeshe jambo hilo nyuma likafanyiwe upembuzi yakinifu

ili waweze kulileta tena kwa Wabunge; alizungumzia juu ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, ambaye anaonekana amejihusisha kwa namna moja ama nyingine katika vitendo vya rushwa. Ninachotaka nisaidiwe sasa na Serikali ama na wewe ni kwamba; inawezekanaje Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini akapata *confidence* ya kuandika barua ya kuomba rushwa kwenye Idara mbalimbali chini ya Wizara bila Waziri ama Naibu Waziri kuwa na hizo taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba mwongozo wako; je, ni kweli anayepaswa kuwajibika katika suala hilo ni Katibu Mkuu wa Nishati na Madini peke yake ama pamoja na Mawaziri wa Wizara husika? Ninaomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kwa mujibu wa kifungu cha 69(1), mjadala ule tumeweka pembeni; hilo la kwanza; na sisi tukakubali hapa na akaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, hilo lililosemwa ndani ya Bunge hili na Mbunge mmojawapo, anakwenda kuliangalia kwa sababu yeye hana madaraka. Kwa hiyo, suala zima nini kifanyike halikufanyika jana. Kwa hiyo, ninaomba waendelee kufanya kazi wanazostahili *administratively*. Hivyo, ndivyo tunavyosema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na tangazo la wageni; wageni tulionao hapa Bungeni, kwanza, Waheshimiwa Wabunge, ninataka tunyamaze. Kuna familia yake Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, watoto wake wawili walipo hapo wasimame; hapa kuna Mariam na Karim. Halafu tuna Viongozi Wakuu wa Wizara, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Hamisi Dihenga. Ahsante. *(Makofi)*

Yupo Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Celestine Gesimba, ahsante. Tuna Kaimu Kamishna sijui Kamishna wa kitu gani, Ndugu Marystella Wassena. Tunaanza kupata wasiwasi, Kamishna wa kitu gani hapa sasa na ikishakuwa ni akina mama na pengine ndiyo vinaondoka hivyo! Tunaye Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Mheshimiwa Balozi Kuhanga. Ahsante, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Mkude, ahsante. Tunao Watendaji Wakuu 23 wa Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu. Halafu wadau wa elimu tulionao hapa ni Mwenyekiti wa Shirika la Maendeleo la Elimu la Canada, Corey Hatington; Kiongozi wa Elimu USAID Renuka Pillay; Mwenyekiti wa TOMONGSCO, sijui kirefu chake ni nini anaitwa Kanali Mstaafu Ally Mwanakatwe; Mratibu wa TEN/MET, ninafikiri huyu mnamfahamu, Mrs. Helma Mengele; na Katibu Mkuu wa CWT, Ndugu Yahaya Msulwa; yuko wapi? Ahsanteni sana.

Halafu tuna wageni 35 wa Mheshimiwa Philipo Mulugo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Jimboni, wakiongozwa na Mheshimiwa Kapala C. Makelele. Huyu ni Mheshimiwa Diwani na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Chunya. Mheshimiwa Diwani yuko wapi? Ahsante. *(Makofi)*

Tunao wenzetu 42 wenye ulemavu wa Mkoa wa Dodoma; wako wapi? Ahsante sana. Karibuni; ni wenye ulemavu mbalimbali. Karibuni sana, tumefurahi kuwaoneni na mjisikie mpo pamoja na sisi. Tunao wanafunzi 50 na walimu kumi wa Shule ya Sekondari ya Makole Dodoma. Ninaomba wasimame walipo; ahsante sana. Ninyi hapa Bunge liko kwenu, kwa hiyo, mnakaribishwa wakati wote. Halafu tuna wanafunzi 52 na walimu saba wa Shule ya Msingi Dodoma Mlimani. Hawa nao wako wapi? Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha St. John; wako wapi wataalam wetu hawa? Ahsante sana. Jitahidini kusoma mnategemewa. Tuna wanafunzi 50 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Dodoma; hawa wako wapi? Ninadhani wamekosa nafasi baadaye wataingia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Vilevile tuna matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati yake kwamba, leo kutakuwa na kikao kwa ajili ya kujadili mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Kamati hiyo kwa kipindi kijacho. Hicho kikao kitakuwa saa saba mchana katika Ukumbi Na. 231, Jengo la Utawala.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, wao saa 7.30 mchana leo, watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 227. Hawa ni saa 7.30, wale wengine ni saa 7. Halafu tunatangaziwa kwamba, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanawakaribisha Wabunge wote kwenye Maonesho ya Vitabu na Machapisho mbalimbali ya vyuo vyao kwenye Viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa kutembelea Maonesho hayo kuanzia leo tarehe 19. Pia kuna Maonesho ya *Mobile Maabara*, mnaweza kwenda kuona, mkaona kama yanafaa katika shule zilizoko kwenye majimbo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, toka juzi tumewatangazia kuhusu msiba wa Mheshimiwa Naibu Spika, aliyefiwa na bibi yake kwamba, wale watakaokwenda magari yatakuwa nje hapo mara baada ya kuahirisha shughuli hizi saa 4.30. Kwa hiyo, wale wanaotaka kwenda watakwenda, lakini mchana wote watakuwa hapa tayari.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya msiba huu, ninaomba nimwombe Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Mabumba, anipokee nikashiriki kwenye msiba huo.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Massele Mabumba) Alikalia Kiti*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Mwenyekiti. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kwanza nakalia Kiti; mwongozo maana yake nini? Ninaomba Mheshimiwa Waziri tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012**
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha mimi kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na uhai na afya njema.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Ninapenda pia kumpongeza Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kuniteua kuiongoza Wizara hii muhimu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwa ujumla kwamba, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote, kuhakikisha kuwa ninafanikisha malengo ya Wizara hii na yale ya Taifa kwa ujumla. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Bagamoyo, kwa kuendelea kuniamini kwa kunichagua kwa mara ya pili kuwa Mbunge wao. Ninawashukuru pia Wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo, kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili Tukufu, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Ninapenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne katika muhula wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kwake na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano. Hii inadhihirisha jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyo na imani kubwa, juu ya busara za Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo na uzoefu wake katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuungana na wenzangu katika kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Spika, kwa kuondokewa na mama yake

mpendwa. Ninapenda pia kuchukua nafasi hii, kumpa salamu za rambirambi Mheshimiwa Job Ndugai, kwa kuondokewa na bibi yake mpendwa, aliyekuwa mlezi wake. Aidha, ninatoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, waliopatwa na misiba kwa kuondokewa na wapendwa wao katika mwaka huu. Ninamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi; *Amina*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe; Katibu Mkuu Profesa Hamisi Omari Dihenga; Naibu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Muhochi Gesimba, pamoja na Kaimu Kamishna wa Elimu Bi. Marystella M. Wassena; Wakurugenzi; Viongozi wa Wakala, Mashirika, Mabaraza na Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Wizara; Viongozi katika ngazi mbalimbali na Wafanyakazi wote, kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na maandalizi ya bajeti hii. Aidha, shukurani zangu ziwaendee Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Wanataaluma, kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishukuru kwa dhati, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Margret Simwanza Sitta, Mbunge Viti Maalum, kwa kuichambua na kuijadili bajeti hii kwa kina na kisha kuyapitisha makadirio ya Wizara yangu. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itaendelea kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ili kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustapha Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya mipango, uchumi, mapato na matumizi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Ninaomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge hao, yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika sekta mbalimbali, ikiwemo Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninapenda sasa kuchukua fursa hii kufanya mapitio na majukumu ya Wizara ya Kisera na ya Kiutendaji. Aidha, nitaelezea utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na malengo na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu ya kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo; kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi; Elimu ya Sekondari; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Juu, pamoja na kusimania Taasisi na Mabaraza yaliyo chini yake. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa

utoaji wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini. Wizara pia ina wajibu wa kufanya mapitio, kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sera, Mipango, Sheria na Kanuni za Elimu zilizopo, kulingana na mabadiliko ya dhima na dira ya Serikali na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/11 na baadaye nitatoa mwelekeo wa Mapato na Matumizi ya fedha za Wizara kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato ya Mwaka wa Fedha 2010/2011. Katika mwaka wa fedha wa 2010/11, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali Shilingi bilioni 5.048. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, Shilingi bilioni 4.382 zilikuwa zimekusanywa, sawa na 86.7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2010/2011. Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 665.573; kati ya hizo, Shilingi bilioni 525.941 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 139.632 zilikuwa ni za maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, matumizi ya kawaida yalikuwa Shilingi bilioni 503.379 na matumizi ya maendeleo yalikuwa Shilingi bilioni 76.821.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya jumla kuhusu matumizi ya fedha zilizopokelewa Wizarani, ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/11:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kamishna wa Elimu ina majukumu ya kuweka na kudhibiti viwango vya ubora wa elimu na utoaji wa elimu katika ngazi za Awali; Msingi; Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; pamoja na Ukuzaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu. Ofisi ya Kamishna wa Elimu inajumuisha vitengo vya Elimu Maalumu, Elimu kwa Redio, Usajili wa Shule, Ithibati ya Vifaa vya Elimu pamoja na Masuala Mtambuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Ofisi ya Kamishna wa Elimu, pamoja na majukumu mengine, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa vifaa pamoja na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule za Msingi 317, za Sekondari 30 na Vyuo vya Ualimu 7;

(b) Ilichagua wanafunzi wenye ulemavu 356 waliofaulu Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Elimu ya Msingi, kwa ajili ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka wa masomo 2011;

(c) Ilijadili Miswada *(manuscripts)* 236 ya vitabu vya kielimu kupitia Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya Kielimu *(Educational Materials Approval Committee - EMAC),* ambapo Miswada 200 iliidhinishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho na 36 ilikataliwa;

(d) Ilisajili shule 169, ambapo 112 ni shule zisizo za Serikali na 57 ni shule zilizojengwa kwa nguvu za Wananchi;

(e) Iliandaa taarifa ya awali ya Mradi wa 'tafiti kuhusu Ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika *(The Southern and Eastern Africa Consortium for Monitoring Educational Quality - SACMEQ Research Project III)* na kutoa rasimu ya kwanza, ambapo kazi ya kuihariri inaendelea;

(f) Ilichambua maombi 400 ya leseni za kufundishia na kutoa leseni kwa waombaji 170;

(g) Iliandaa na kutangaza vipindi 528 redioni vya masomo ya Shule za Msingi; na

(h) Iliandaa na kutangaza vipindi 52 redioni kuhusu mbinu za ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Msingi iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya MMEM (2007 - 2011) kama ifuatavyo:-

(a) Ilikamilisha hadidu za rejea kwa ajili ya tathmini ya Awamu ya Pili ya MMEM ili kuandaa andiko la Awamu ya Tatu ya Mpango huo;

(b) Iliwezesha kufanyika kwa mafunzo kwa ajili ya walimu 210 wa masomo ya Hisabati, Sayansi, English na Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kutoka Halmashauri 15;

(c) Iliandaa mwongozo wa ufundishaji wa somo la sayansi kwa vitendo ambao tayari umefanyiwa majaribio;

(d) Iliwezesha kufanyika kwa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu ya msingi kwa maafisa elimu 161 kwa kipindi cha mwezi mmoja, katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM)* huko Bagamoyo;

(e) Iliratibu na kufuatilia utekelezaji wa 'Mpango wa Lishe Shuleni' katika Halmashauri 16 zenye ukame na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa utoaji wa huduma ya chakula shuleni. Aidha, iliandaa rasimu ya andiko (Concept Note) la 'Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni', na kuliwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hatua zaidi;

(f) Ilifuatilia uandikishaji wa watoto katika Elimu ya Msingi katika Halmashauri 30 za mikoa kumi, ambapo taarifa za awali zinaonesha kuwa uandikishaji ulikuwa wastani wa asilimia 50. Aidha, iliandaa vipeperushi na mabango ya uhamasishaji juu ya umuhimu na taratibu za uandikishaji wa watoto katika elimu ya awali;

(g) Iliendelea na uandaaji wa miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto na Upimaji wa Utoaji wa Elimu ya Awali.

Aidha, wadau 50 kutoka Halmashauri tano za Bagamoyo, Temeke, Mtwara Vijijini, Magu na Siha, walijengewa uwezo kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto; na

(h) Iliandaa na kuratibu Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV na kufuatilia uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Sekondari ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari, ambayo kimsingi ni kiungo kati ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Juu. Aidha, Idara ya Sekondari inasimamia utoaji bora wa elimu kwa usawa kuanzia Kidato 1– 6; na kuweka viwango na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari itolewayo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Sekondari hutolewa katika ngazi ya kawaida *(O-level),* ambayo huchukua miaka minne na ngazi ya juu *(A-level),* ambayo ni ya miaka miwili. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, jumla ya shule zote za sekondari nchini zilikuwa 4,266. Kati ya hizo, shule 3,397 ni za serikali (3,308 za Wananchi za kutwa, 89 ni shule kongwe za Serikali) na 869 ni shule zisizo za Serikali. Jumla ya wanafunzi katika Shule za Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali nchini ni 1,638,699. Wanafunzi wa Kidato cha 1 – Kidato cha 4 ni 1,566,685 (wasichana 699,951). Wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6 ni 72,014 (wasichana 28,577). Idadi kubwa ya wanafunzi waliopo shuleni ni kielelezo cha juhudi za Wananchi katika kupanua na kuendeleza Elimu ya sekondari Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wameendelea kuona mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), yanayotokana na kuongezeka kwa udahili katika Kidato cha Kwanza. Katika mwaka 2010, wanafunzi waliosajiliwa katika Kidato cha Kwanza katika Shule za Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali walikuwa 438,827 na mwaka 2011 walikuwa 467,155.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kushuka kwa ufaulu katika mitihani ya Kidato cha Nne, idadi kubwa ya wanafunzi waliopata Daraja la I – III katika Mitihani ya Kidato cha Nne, ambao ndiyo wenye sifa za msingi za kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2011, wanatoka Shule za Sekondari za Kutwa za Wananchi. Kati ya watahiniwa 38,781 waliopata Daraja la I-III katika Mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2010, wanafunzi 19,126 wanatoka Shule za Sekondari za Wananchi za Kutwa. Aidha, wanafunzi 3,697 wametoka katika Shule Kongwe za Sekondari za Serikali na 15,958 wanatoka katika Shule za Sekondari zisizo za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la kugatua uendeshaji wa Shule za Sekondari lilitolewa na Mheshimiwa Rais mwezi Februari, 2008. Shughuli mbalimbali za utekelezaji wa tamko hilo zilianza tangu wakati huo na mpaka sasa Serikali inaendelea kukamilisha mchakato wa kugatua usimamizi na uendeshaji wa Shule za Sekondari. Ugatuaji huu ulifanyika kwa malengo yafuatayo:-

(a) Kusogeza usimamizi na uendeshaji wa shule karibu na wadau;

(b) Kusogeza uratibu wa utekelezaji wa kila siku wa mitaala ya masomo karibu na Halmashauri; na

(c) Kutoa nafasi zaidi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusimamia na kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zinazotokana na ugatuaji, huduma kwa walimu na wanafunzi zinafanyika kwa mafanikio zaidi sasa. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuwa na dhamana ya Sekta ya Elimu, yenye wajibu wa kutambua elimu bora kwa nchi yetu na kusimamia upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iligharimia mafunzo kazini kwa walimu 1,000 wa masomo ya sayansi, hisabati na *English;*

(b) Iligharimia mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wawezeshaji 336 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa lengo la kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo hayo;

(c) Ilitoa kompyuta kwa ajili ya shule 30 na kuendesha mafunzo kwa walimu kuhusu namna ya kuzitumia katika kufundisha masomo anuwai kwa kupitia mtandao;

(d) Iliwezesha kuanzishwa kwa vituo vya mafunzo kazini kwa ajili ya walimu wa hisabati na sayansi katika shule za sekondari 25 katika mikoa 21 na kuvipatia vifaa vya maabara (fizikia, kemia na biolojia), kompyuta, printa, fotokopia, skana, mashine ya kurudufia *(duplicator)* na projekta ya *LCD* kwa kila kituo;

(e) Iliendesha kambi za sayansi kwa wanafunzi wa kike 100 kwa lengo la kuwajengea wanafunzi hao uwezo wa kufaulu masomo ya sayansi na hisabati. Aidha, ilitoa mafunzo ya kuendesha kambi hizo kwa walimu 30 wa Shule za Sekondari za Mkoa wa Dar es Salaam;

(f) Iliandaa miongozo ya kuwezesha ufundishaji wa masomo ya sayansi (fizikia, kemia na biolojia) kwa vitendo kwa Kidato 1 - 4, ambapo nakala 5,000 zilichapishwa kwa kila somo;

(g) Ilifanya tathmini na ufuatiliaji wa ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati, hususan kwa walimu waliopata mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kufundisha masomo hayo, katika mikoa kumi ili kubaini manufaa na changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mtaala;

(h) Ilikamilisha utayarishaji wa Awamu ya Pili ya MMES na kuwezesha kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo tarehe 19 Januari, 2011;

(i) Iliandaa Mpango wa Utekelezaji na Mpango wa Ununuzi;

(j) Ilitoa mafunzo kwa watendaji 527 wa Halmashauri, Maafisa Elimu wote wa Mikoa na Wakuu wa Shule 903 ili kuwaelimisha juu ya utekelezaji wa MMES Awamu ya Pili;

(k) Ilitoa vivunge vya sayansi (*Science Micro Kits)* vyenye vifaa vinavyoweza kutumika katika majaribio ya masomo ya fizikia, biolojia na kemia kwa ajili ya Shule za Sekondari 180 katika Mikoa tisa (Kigoma, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Dodoma, Morogoro na Kagera) na kuendesha mafunzo ya namna ya kuvitumia, kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya *UNESCO*; na

(l) Iliratibu mashindano ya uandishi wa insha katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya *SADC*, ambapo Wanafunzi wa Tanzania walishika nafasi ya kwanza katika Afrika Mashariki na nafasi ya tatu katika Nchi za Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ualimu inasimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada. Aidha, Idara huandaa na kupitia miongozo na viwango vya Elimu ya Ualimu na kufuatilia uendeshaji na utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya elimu ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada hutolewa katika Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali na 69 visivyo vya Serikali, vyenye uwezo wa kudahili jumla ya wanachuo 43,098 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuinua ubora wa utoaji wa elimu nchini, Wizara yangu ilizindua Mkakati wa Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Elimu ya Msingi - Ngazi ya Shule (MWAKEM), wenye lengo la kuimarisha uwezo wa walimu wa kufundisha pamoja na kuwajengea umahiri katika kufundisha elimu ya awali na msingi. MWAKEM inatimiza lengo la pili la MMEM, ambalo ni kuinua ubora wa elimu kwa kujenga uwezo wa walimu wa shule za msingi ili kuimarisha utoaji wa elimu bora. Utekelezaji wa MWAKEM, unafanyika kwa mfumo wa moduli kwa njia ya elimu masafa. Utaratibu huu unampa mwalimu nafasi ya kujifunza mambo mapya yaliyomo katika mtaala, kupata dhana, nadharia na mbinu bora za kufundishia na kujifunzia ili kukidhi mabadiliko ya kijamii, sayansi na teknolojia, pamoja na kumwezesha mwalimu kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu. MWAKEM inatekelezwa katika ngazi ya shule na hivyo kumwezesha mwalimu kusoma huku akiendelea kufanya kazi. Aidha, kujiendeleza kwa namna hii humwezesha mwalimu kujifunza kwa kutenda awapo shuleni, badala ya kutegemea nadharia za vitabuni. Mafunzo ya namna hii, yana gharama ndogo ikilinganishwa na yale ya kukaa chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Ualimu ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanachuo 6,379 wa ngazi ya cheti na 4,189 wa ngazi ya Stashahada katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali. Aidha, ilitoa mafunzo kwa walimu 348 katika fani maalumu mbalimbali (kwa mfano, michezo, muziki, sanaa za ufundi na sanaa za maonesho) katika ngazi ya Cheti na Stashahada;

(b) Ilitoa wahitimu 11,196 (5,793 wanawake, 5,403 wanaume) wa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti. Aidha, walimu wanafunzi 7,088 (wanawake 2,410 na wanaume 4,678) walihitimu mafunzo ya ngazi ya Stashahada, ambapo 1,497 ni walimu kazini na 5,591 ni walimu tarajali. Walimu wote wa ngazi ya cheti ni walimu tarajali. Walimu tarajali wa ngazi ya cheti watapangwa kwenda kufundisha shule za msingi na wa ngazi ya stashahada watapangwa kwenda kufundisha shule za sekondari mwezi Julai/Agosti 2011. Walimu kazini watarudi kwenye vituo vyao vya kazi;

(c) Iliwezesha wakufunzi 120 kuhudhuria mafunzo ya jinsi ya kutumia TEHAMA katika kufundisha na kujifunza, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mafunzo haya yalilenga katika kutekeleza Mradi wa TEHAMA katika shule 35 za sekondari na vyuo 7 vya Ualimu kwa majaribio;

(d) Iliwezesha utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Masuala Mtambuko na huduma za afya na kinga dhidi ya VVU na UKIMWI kwa wakufunzi 124;

(e) Iliendesha mafunzo ya mbinu za Ufundishaji Bainifu na Elimu ya UKIMWI kwa wakufunzi 36, Walimu wa Shule za Msingi 275, Wakaguzi wa Shule 12 na waratibu wa vituo vya walimu 9 kutoka katika Wilaya za Mkoa wa Kigoma (Kibondo, Kigoma Vijijini na Kasulu);

(f) Iliendesha mafunzo ya ufundishaji wa somo la French kwa wawezeshaji 36 wa Shule za Sekondari na mafunzo ya jinsi ya kufundisha somo hili katika Shule za Sekondari kwa walimu 156;

(g) Iligharimia mafunzo ya wakufunzi 285 katika Vyuo Vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(h) Iliwezesha mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo, Maafisa na Watendaji 74 kuhusu kuinua ubora wa utendaji kazi katika maeneo ya uongozi na uhasibu katika Taasisi ya ESAMI;

(i) Iliandaa mwongozo wa ufundishaji wa sayansi, *english* na TEHAMA kwa vitendo katika Vyuo vya Ualimu;

(j) Ilikamilisha moduli za masomo ya Hisabati, *English,* pamoja na ujuzi wa kufundisha kwa umahiri kwa ajili ya Programu ya Mafunzo kwa Walimu Kazini kwa

Elimu ya Msingi Ngazi ya Shule ama MWAKEM; na kutoa mafunzo kwa watendaji 2864 wa Programu hiyo; na

(k) Ilitoa mafunzo kwa Watendaji wa Programu ya MWAKEM, 329, walimu mahiri 423, pamoja na kuelimisha Walimu 2,052 wa Shule za Msingi. Aidha, ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji 60 wa ngazi za Halmashauri, Chuo na Shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni kuleta msukumo katika juhudi za Serikali za kukabiliana na ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, Idara ina wajibu wa kutoa fursa ya kujiendeleza kielimu nje ya mfumo rasmi wa shule miongoni mwa vijana na watu wazima na kusimamia vituo vya magazeti ya elimu katika kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliwezesha uandaaji wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia vya wanakisomo; vikiwemo Mwongozo wa Mwezeshaji, Kitabu cha Mwanakisomo, *Scripts* na Filamu za masomo 65 yatakayofundishwa katika Mradi wa Ndiyo Ninaweza;

(b) Iliratibu uandaaji wa Sera na Mwongozo wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(c) Iliandaa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Elimu juu ya Haki za Binadamu na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima – 2011/12 – 2015/16;

(d) Ilifanya ufuatiliaji na tathmini katika wilaya tisa (Ilemela, Dodoma - Manispaa, Songea - Manispaa, Mkuranga, Ngorongoro, Kiteto, Kilindi, Singida - Manispaa na Kigoma (V)) za majaribio ya Programu ya Ndiyo Ninaweza ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza; na

(e) Ilichapa na kusambaza nakala 100,000 za magazeti ya Elimu katika Kanda za Kusini na Ziwa na kuyasambaza katika Wilaya za Kanda hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, ina majukumu ya kubuni, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, pamoja na mambo mengine, ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Iliwezesha kupatikana kwa Mtaalam Elekezi wa kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU);

(b) Iliwezesha kukutana kwa wahadhiri wa vyuo 12 vya Tanzania na 12 vya Canada katika Warsha mbili zilizofanyika Morogoro chini ya uratibu wa Mradi wa *Education for Employment* ili kuandaa na kuanzisha mitaala inayozingatia umahiri *(Competence-Based)* katika Vyuo vya Ufundi nchini; na

(c) Ilifanikisha kuwekeana saini Hati ya Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na *Metsol AB* ya Sweden juu ya kuanzisha mafunzo ya tabia za metali *(Metallurgy)* nchini, ambapo wataalamu kutoka Sweden watakuja nchini kwa ajili ya kuandaa mitaala wakishirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Elimu ya Juu ina majukumu ya kusimamia na kutathmini Sera, Sheria, Taratibu na Miongozo ya Utoaji wa Elimu ya Juu. Aidha, Idara ya Elimu ya Juu, kwa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mamlaka ya Elimu Tanzania na Vyuo vya Elimu ya Juu, inahakikisha kuwa elimu inayotolewa inazingatia ubora kulingana na mahitaji ya soko la ushindani na inawafikia walengwa wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Elimu ya Juu ilitolewa katika Vyuo Vikuu 19 (vya umma 8 na visivyo vya serikali 11 na vyuo vikuu vishiriki 15; vya Umma 3 na visivyo vya Serikali 12). Kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufundisha na kufanya utafiti ambao, pamoja na kuwa sehemu ya taaluma, unalenga katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini miongoni mwa jamii na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iligharimia mafunzo kwa Wanafunzi Madaktari 1,750 wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo katika Vyuo vya *MUHAS, UDOM, HKMU, KCM-College, WBUCHS, IMTU* na *SUA.* Kati ya hao, 84 ni madaktari wa meno na 70 ni madaktari wa tiba ya mifugo;

(b) Ilitekeleza utaratibu wa kubadilishana wanafunzi kati ya Tanzania na Msumbiji na Tanzania na Uganda, ambapo Watanzania 68 wanasoma Uganda na 29 wanasoma Msumbiji. Aidha, wanafunzi 50 Raia wa Msumbiji na 69 Raia wa Uganda wanasoma katika Vyuo Vikuu nchini Tanzania;

(c) Iliwawezesha wanafunzi watano raia wa China kusomea kozi ya muda mfupi ya Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya utaratibu wa skolashipu zinazotolewa na Serikali ya Tanzania kwa Serikali ya China katika kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China;

(d) Ilifanikisha uelimishaji wa wadau kuhusu fursa za Elimu ya Juu nchini na nje ya nchi pamoja na umuhimu wa uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu katika Mikoa ya Rukwa, Kagera, Tabora na Shinyanga. Aidha, uelimishaji ulifanyika kupitia

Maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu nchini yaliyofanyika Dar es Salaam tarehe 27 - 29 Aprili 2011;

(e) Ilidhamini mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa Wahadhiri 18 wanaosoma Ujerumani kupitia skolashipu zinazotokana na mkataba kati ya Tanzania na Ujerumani *(DAAD scholarships);*

(f) Ilipokea na kuratibu nafasi 132 za masomo; kutoka Uingereza (12), China (72), Korea ya Kusini (2), India (20), New-Zealand (2), Urusi (15), Misri (5) na Cuba (4);

(g) Iligharimia mahitaji maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu katika Vyuo Vikuu; *UDSM, SUA, MZUMBE, MUCCoBS* na *DUCE;* na

(h) Iiliratibu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) kwa kukusanya taarifa zinazohusu maeneo ya kipaumbele katika Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi wa Shule ina majukumu ya kuhakikisha kuwa, Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa kwa ufanisi katika ngazi za elimu ya awali, msingi, sekondari, vitengo vya elimu maalum, vituo vya ufundi stadi, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Ukaguzi wa Shule ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilikagua Jumla ya asasi za elimu 7,906 na kutoa ushauri na msaada wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu. Aidha, uhaba wa walimu, miundombinu isiyotosheleza, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilibainika katika shule zilizokaguliwa;

(b) Iliandaa Mwongozo wa Mafunzo *(Training Manual)* kwa ajili ya wasimamizi wa elimu kwa kushirikiana na *UNICEF;* na

(c) Iliteua wakaguzi 214 na kuwapa mafunzo ya ukaguzi wa shule mwezi Agosti, 2010 na kuwapanga katika Wilaya na Kanda husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Sera na Mipango inahusika na utoaji wa utaalamu na huduma katika uandaaji, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, pamoja na uratibu wa maandalizi ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Wizara na Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha ya Umma na Mipango ya Utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliandaa Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo na kuendelea kuisambaza kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni;

(b) Iliandaa michoro na miongozo ya ujenzi wa shule za sekondari chini ya MMES Awamu ya Pili (2010-2015);

(c) Iliendesha mafunzo kuhusu mipango ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya shule kwa watendaji 527 wa Halmashauri katika Kituo cha *ADEM* – Bagamoyo na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wakuu wa Shule za Sekondari 924 katika Vituo vya *ADEM* - Bagamoyo, Njombe na Kahama;

(d) Iliendelea kusimamia ujenzi wa shule ya sekondari ya bweni ya mchepuo wa sayansi kwa ajili ya Kidato cha 5 na 6 Miono - Bagamoyo;

(e) Iliendelea kusimamia ujenzi wa Shule za Msingi za Msoga (kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China);

(f) Iiliendelea kusimamia ujenzi wa Shule ya Arusha Contonment;

(g) Iilifanya tathmini ya hali halisi *(Physical Condition Survey)* ya miundombinu ya vyuo vya ualimu 10 na Maktaba 14 za Mikoa ili kubaini mahitaji halisi ya kuifanyia ukarabati;

(h) Iliimarisha Mfumo wa Takwimu *(Database)* za elimu katika Halmashauri 105 kwa kushirikiana na *UNESCO* kupitia Programu ya *Education Sector Management Information System (ESMIS);*

(i) Iliendesha Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Utendaji katika Sekta ya Elimu *(Joint Education Sector Review)* kwa mwaka 2009/10; na

(j) Ilifanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na kuandaa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi pamoja na Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi. Aidha, inaratibu Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliratibu ajira za watumishi wapya 351 (walimu 340 na watumishi wasio walimu 11), iliidhinisha vibali vya ajira za wataalam wa kigeni 722, ilithibitisha kazini watumishi 85 na kuratibu upandishaji vyeo wa watumishi 1,010 (walimu 812 na watumishi wasio walimu 198);

(b) Ilikamilisha rasimu ya mkataba wa huduma kwa mteja ambapo utekelezaji wake utaanza Mwaka wa Fedha wa 2011/12;

(c) Wizara inaendelea kushughulikia madai ya watumishi kila yanapopokelewa. Kati ya Julai, 2010 na Juni, 2011, Wizara ilihakiki na kuwasilisha Hazina madai mbalimbali ya watumishi 822 yakiwa na thamani ya Sh. 1,269,298,719.60. Kati ya hayo, malimbikizo ya mishahara yalikuwa na thamani ya Sh. 777,918,643.00 na madai mengineyo yalikuwa ya Sh. 491,380,076.60. Aidha, hivi sasa, madai ya watumishi 844, yenye thamani ya Sh. 923,899,277.18 yanashughulikiwa; na

(d) Iliandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za watumishi kwa kutumia TEHAMA ambapo taarifa za watumishi zimeanza kuhakikiwa na kuingizwa katika mfumo huo ili ziweze kutumika rasmi mwaka ujao wa fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano, kina majukumu ya kuratibu na kuandaa utoaji wa habari za Sekta ya Elimu kwenye vyombo vya habari na Wananchi. Aidha, kinashirikiana na wadau wengine wa Sekta ya Elimu katika kuhamasisha Wananchi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kiliratibu na kuandaa utoaji wa habari zinazohusu matukio ya elimu yakiwemo, uzinduzi wa MMES Awamu ya II na Mpango wa Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Walimu wa Shule za Msingi (MWAKEM);

(b) Kilifanikisha kuchapishwa kwa nakala 2,000 za Jarida la *EdSDP* katika Kanda za Elimu na kuzisambaza ili kuhamasisha jamii kuhusu mikakati ya kutekeleza mipango ya elimu;

(c) Kiliandaa vipeperushi 500, kalenda 17,500 na shajara 2,000 kwa ajili ya kuwaelezea wadau juu ya sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya elimu;

(d) Kilijibu hoja 30 za wadau kati ya 35 zilizotolewa katika tovuti ya Wananchi, *(www.Wananchi.go.tz)* na tano bado zinafanyiwa kazi; na

(e) Kilikamilisha rasimu ya kwanza ya Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu, yana wajibu wa kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Mwaka 2010/11, kila Wakala, Baraza na Taasisi zilitekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), ina jukumu la kutoa mafunzo ya elimu ya Watu Wazima na elimu ya kujiendeleza nje ya mfumo rasmi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilitoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi kwa kutumia mfumo unaozingatia umahiri *(Competence Based Education & Training Curriculum - CBET),* kwa walengwa 140 wa ngazi ya Cheti, 300 wa Stashahada, 125 wa Stashahada ya juu na 202 wa Shahada;

(b) Ilitoa mafunzo ya namna ya kufundisha kwa kutumia mfumo unaozingatia umahiri kwa wakufunzi na wahadhiri 53 wa TEWW na Vyuo sita vilivyo chini ya *NACTE* vikiwemo *Tanzania Institute of Accountancy, Institute of Social Work, Tanzania Insurance Institute* na Chuo cha Polisi Moshi na Dar es Salaam;

(c) Ilitoa machapisho na majarida ya kitaaluma ya *TEWW, Journal of Adult Education No.18, Studies in Adult Education No. 66* na *Alumni Newsletter;*

(d) Ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana tangu ulipoanzishwa 2004 - 2009 kwa nchi nzima;

(e) Ilifanikisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaosoma kupitia Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kutoka 49,533 mwaka 2009 hadi 62,533 mwaka 2011;

(f) Ilizindua utekelezaji wa Programu ya *Integrated Post-Primary Education (IPPE)* katika Wilaya za Siha na Temeke. Masomo ya Ufundi na masuala mtambuko ya Programu ya *(IPPE)* yameandaliwa kwa mtindo wa moduli;

(g) Iligharimia mafunzo ya kujiendeleza kwa watumishi 42 katika ngazi zifuatazo: shahada ya uzamivu wahadhiri 2; shahada ya uzamili wakufunzi 5; shahada ya kwanza 2; na mafunzo ya kitaalamu ya muda mfupi kwa watumishi 33 wa kada zisizo za kitaaluma; na

(h) Iliandaa na kusambaza nakala 300 za moduli za Elimu Masafa na Ana kwa Ana katika mikoa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Tanzania, ina majukumu ya kubuni na kuandaa mitaala na mihtasari ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Elimu Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo: Ilitoa mafunzo elekezi kwa walimu 265 wa shule za sekondari; iligharimia mafunzo ya waratibu wa mitaala sita; ilikamilisha maandalizi ya moduli za masomo 17 kwa ajili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada na cheti na kuzihariri tayari kwa uchapishaji; na iliandaa na kuifanyia majaribio mihtasari sita ya masomo ya ufundi kwa ajili ya Kidato cha 1 - 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba nchini; kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Vijiji, Wilaya hadi Mikoa na kutoa mafunzo na kuendesha Mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliwezesha kupatikana kwa jumla ya vitabu 93,914; kati ya hivyo, 817 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 1975, vitabu 87,847 vilipatikana kwa njia ya msaada na vitabu 5,250 vilinunuliwa na hivyo kufanya idadi ya vitabu vyote katika maktaba nchini kufikia 1,091,043;

(b) Iliwezesha kupatikana kwa machapisho ya magazeti na majarida 32,828. Kati ya hayo, 28,810 ni Magazeti na 4,018 ni Majarida na hivyo kufanya jumla ya magazeti na majarida yote kufikia 673,730;

(c) Ilisambaza jumla ya vitabu 50,670 kwenda katika maktaba 20 za Mikoa, 14 za Wilaya na 2 za Tarafa;

(d) Ilitoa ushauri kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba katika shule 164 na vyuo 60;

(e) Iliwezesha udahili wa wanafunzi 579 wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka, ambapo wa ngazi ya Cheti walikuwa 264, wa Stashahada 169 na wa mafunzo ya awali 146;

(f) Iliwezesha uhitimu wa wanachuo 392 (cheti – 184, Stashahada – 62 na mafunzo ya awali – 146); na

(g) Ilikamilisha uandaaji wa michoro ya mabweni mawili ya wanafunzi wa kike na mkandarasi amepatikana na amekwishaanza kazi ya ujenzi wa bweni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu Bagamoyo *(Agency for the Development of Educational Management-ADEM)*, una majukumu makuu manne: Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti katika masuala yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; na kuandaa na kusambaza makala na vitabu mbalimbali vya uongozi na uendeshaji wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ulitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ulipanua wigo wa kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa kufungua kituo cha mafunzo Kanda ya Ziwa kwenye majengo ya Kituo cha Taifa cha Kisomo cha Elimu ya Watu Wazima, Mwanza. Kituo kina wanachuo 77; kati ya hao, wanawake ni 43 na wanaume ni 34;

(b) Ulitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa wanachuo 386 kati ya 420 waliotarajiwa. Wanachuo 309 wako Kituo cha ADEM-Bagamoyo na 77 wako Kituo cha ADEM- Mwanza;

(c) Ulitoa mafunzo ya awali ya Ukaguzi wa Shule kwa Wakaguzi wa Shule 214 sawa na asilimia 93.9 ya Wakaguzi 228 waliolengwa;

(d) Ulitoa mafunzo ya mwezi mmoja ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Maafisa Elimu wapya 69 wa ngazi ya Halmashauri, sawa na asilimia 92 ya maafisa 75 waliotarajiwa;

(e) Ulitoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Sekondari 881 na Maafisa Elimu 20 wa Mikoa, katika utekelezaji wa MMES Awamu ya II (2010-2015). Washiriki walitoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara;

(f) Ulitoa mafunzo juu ya mbinu bora za usimamizi wa shule kwa maafisa 285, ambapo Maafisa Eelimu wa Mikoa walikuwa 21, Maafisa Elimu wa Elimu ya Sekondari 132 na wa Elimu wa Elimu ya Msingi 132;

(g) Uliandaa mahitaji ya mafunzo kwa ajili ya Kamati za Shule za Msingi, Waratibu Elimu Kata na Bodi za Shule za Sekondari ili kubaini maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kuandaa mafunzo. Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha washiriki kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari katika maeneo yao kwa ufanisi;

(h) Ulikamilisha Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Wakala *(Master Plan);* na

(i) Uligharimia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 26 yaliyoendeshwa ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi. Aidha, Wakala ulifadhili mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ina majukumu ya kutekeleza Programu za unesco nchini, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilisimamia, kuratibu, pamoja na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Ushirikishwaji *(Participation Programme)* kulingana na maamuzi ya kikao cha 35 cha

Mkutano Mkuu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO General Conference);*

(b) Ilisimamia utekelezaji wa Programu katika sekta tano za *UNESCO* pamoja na Programu ya Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia, ambapo Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam zilishiriki katika warsha za usafi na utunzaji wa mazingira wa Jiji la Dar es Salaam;

(c) Iliendelea kusimamia ushiriki wa Wataalam wa Tanzania katika Programu mbalimbali ikiwemo Programu ya Maji, Programu ya Bahari, Progamu ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu na Programu ya Mtu na Mazingira;

(d) Ilitoa vitabu na vifaa vya maabara ya lugha kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), vitabu, vifaa vya maabara na kompyuta kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Barabara ya Mwinyi, Wilayani Temeke na Shule ya Umba Korogwe, Tanga, kupitia Miradi Shirikishi. Aidha, ilisimamia utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Mazingira ya Kufundishia na Kujifunzia katika Shule ya Sekondari ya Maneromango - Kisarawe;

(e) Iligharimia masomo ya wanachuo sita wa kike katika ngazi ya uzamili katika masomo ya sayansi; na kuwezesha uanzishwaji wa Kituo cha Habari kinachotumia TEHAMA kwa ajili ya Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania (BAMVITA);

(f) Iliendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika na Programu ya Uhuishaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, kwa kushirikiana na *UNESCO*. Aidha, ilishirikiana na wadau wa astronomia na kemia katika kutekeleza Programu za *UNESCO* nchini;

(g) Ilisimamia mpango wa kuimarisha elimu ya sayansi katika shule zilizo katika mtandao wa *UNESCO* na kuanza kugawa Vionambali *(Telescope)* 250 katika shule mbalimbali na kuhamasisha shule nyingi zaidi kujiunga na mtandao wa *UNESCO* Tanzania Bara na Visiwani;

(h) Iliwezesha uwasilishwaji Bungeni Miswada miwili ya Utamaduni kwa ajili ya kuridhiwa; Mkataba wa *UNESCO* wa Mwaka 2001 wa Kuhifadhi Urithi wa Kiutamaduni (*Convention on the safeguarding of Intangible Cultural Heritage)* na Mkataba wa *UNESCO* wa 2005 - *Convention on the Protection and Promotion of Cultural Diversity Expressions*, kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo;

(i) Iliratibu ushiriki wa Tanzania katika kikao cha 34 cha Kamati ya Kimataifa ya Urithi wa Dunia, kilichofanyika nchini Brazil tarehe 25 Julai – 3 Agosti 2010, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii;

(j) Ilitekeleza mpango wa pamoja wa mafunzo kwa watendaji wake na kuendesha warsha za kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume husika kwa kushirikina na Tume za Taifa za *UNESCO* za Afrika ya Mashariki;

(k) Iliratibu mchakato wa uteuzi wa awali wa vijana 12 watakaoshiriki katika ushindani wa nafasi za kazi za *UNESCO (Young Professionals Programme);* na

(l) Ilichapisha na kusambaza Toleo Na. 7 la Jarida la Tanzania na *UNESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kutekeleza Sera ya Mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978. Aidha, Baraza lina jukumu la kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada, Mtihani wa Maarifa na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na Bodi za Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Baraza la Mitihani la Tanzania lilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Liliendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2010 kwa watahiniwa 895,013;

(b) Liliendesha Mitihani ya Kidato cha Nne ya mwaka 2010, Maarifa *(QT)* wa Mwaka 2010, Kidato cha Sita 2011 na Ualimu 2011 kwa jumla ya watahiniwa 543,805;

(c) Lilisimamia Mitihani inayotolewa na Bodi za Nje ya nchi kwa watahiniwa 65;

(d) Lilinunua *server* tatu zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya matumizi yafuatayo: Kusajili watahiniwa kupitia mtandao *(online);* kuchambua Mitihani ya Taifa pamoja na kuhifadhi taarifa za matokeo na picha za watahiniwa waliofanya mtihani; na kusanifu na kukuza mifumo inayotumika katika Baraza la Mitihani;

(e) Lilikamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano 2010/11 - 2015/16; na

(f) Lilikamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Usahihishaji cha Mbezi Wani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina majukumu ya kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa na miundombinu iliyokabidhiwa na *ANC* kwa ajili ya kulinda Historia ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Baada ya Serikali ya Tanzania kukabidhiwa Kituo cha Maendeleo Dakawa kutoka kwa Wapigania Uhuru wa *ANC*, Wizara yangu imekusudia kukiendeleza kituo hiki na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi na Ufundi kupitia taasisi zilizopo na zitakazoainishwa hapo baadaye ili kiwe Kitovu cha Utoaji wa Elimu *(Centre of Excellence).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Maendeleo Dakawa chenye eneo la ekari 7,500, kina jumla ya nyumba 82 za kuishi watumishi na majengo mengine muhimu yanayowezesha uendeshaji wa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada kwa wanachuo 783. Aidha, Kituo kina shule ya sekondari ya juu ya wasichana ya kidato cha 5 na 6 (Shule ya Sekondari Dakawa), yenye wanafunzi 450 na wafanyakazi 26. Chuo cha Ufundi Stadi – *VETA* chenye wanachuo 160 na Wafanyakazi 20; Shule ya Msingi yenye walimu 15, wanafunzi 400 wa Elimu ya Msingi na 50 wa Elimu ya Awali. Aidha, kuna Zahanati inayotoa huduma kwa wanajamii waliopo ndani na nje ya Kituo. Zahanati hii ina Maafisa Tabibu wawili na Wauguzi watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya Sekta ya Elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika Miradi ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Mamlaka ya Elimu Tanzania, ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliendesha harambee kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi 2,298 wenye ulemavu katika shule 49 kwa kuwapatia vifaa vya kujifunzia na visaidizi; ambapo kiasi cha Sh. Milioni 491.2 zilipatikana;

(b) Iliimarisha miundombinu ya shule 116 za msingi na sekondari na vyuo vya elimu ya juu vinane, kwa kufadhili Miradi ya Maboresho ya jumla ya Sh. bilioni 2.1 kutoka kwenye Mfuko wa Elimu;

(c) Ilifanya ufuatiliaji, ukaguzi na tathmini katika Miradi 120 iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu;

(d) Iliendelea kuhamasisha Halmashauri za Serikali za Mitaa kuanzisha Mifuko ya Elimu na kuimarisha ushirikiano na Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania. Aidha, ilihamasisha uchangiaji wa Mfuko wa ELimu kupitia vipindi vya televisheni na redio, vipeperushi, majarida na vyombo vingine vya habari; na

(e) Ilikamilisha andiko la marekebisho la vyanzo vya mapato ya Mfuko ikiwa ni hatua ya mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, ina majukumu ya kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, kusimamia ubora wa elimu na kuidhinisha programu zinazofundishwa ili zikidhi mahitaji ya Taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilitathmini ubora wa programu 140 za masomo ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki nchini;

(b) Iliandaa na kuendesha warsha na semina 12 za mafunzo ya uelimishaji umma kuhusu majukumu ya Tume na mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi wa Vyuo Vikuu nchini;

(c) Ilikamilisha rasimu ya kwanza ya mfumo wa tuzo zinazotambuliwa kitaifa *(National Qualifications Framework)* na maandalizi ya kanuni zake;

(d) Ilitathmini na kutambua vyeti 300 vilivyowasilishwa na wahitimu wa Vyuo Vikuu vya Nje ya nchi;

(e) Iliratibu na kutathmini mradi wa majaribio ya udhibiti wa ubora wa programu za vyuo vikuu vitano vinavyotekeleza Mradi chini ya *Inter-University Council for East Africa (IUCEA);*

(f) Ilichapisha na kusambaza nakala 20,000 za Kitabu cha Mwongozo wa Mwanafunzi, nakala 1,000 za vitabu vyenye taarifa fupi za Vyuo Vikuu nchini na vipeperushi mbalimbali vinavyomwelekeza mwanafunzi jinsi ya kuomba kudahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu nchini. Aidha, Tume ilitoa taarifa mbalimbali zinazoelimisha umma juu ya majukumu ya Tume;

(g) Ilikagua na kutathmini mipango ya kuanzisha au kuhuisha Vyuo Vikuu vinane (Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan - Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya cha Mtakatifu Fransis - Ifakara Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mihayo - Tabora, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa - Lushoto, Tanga, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Bugando - Mwanza, Chuo Kikuu cha Bagamoyo, Chuo Kikuu kishiriki cha Bukoba na Kitivo cha Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino-Mtwara), kwa lengo la kutoa hati husika;

(h) Iliratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi 533,195 kwa kutumia mfumo mpya wa udahili wa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ujulikanao kama *Centralized Admission System (CAS).* Mfumo huu unahusisha vyuo 53 vya Elimu ya Juu vikiwemo vyote vya umma na baadhi vya binafsi;

(i) Iliratibu Maonesho ya Sita ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika Dar-es Salaam tarehe 27 - 29 Aprili 2011, ambayo kaulimbiu yake ilikuwa *Building a Knowledgeable, Responsible, Accountable and Progressive Society, through Higher Education Science and Technology*. Aidha, jumla ya taasisi na asasi 62 zilishiriki kutoka ndani na nje ya nchi, nyingi zikiwa ni Vyuo vya Elimu ya Juu; na

(j) Iliendesha mafunzo ya kuwaelimisha watumishi wake wote juu ya Sheria mpya ya kupambana na kuzuia rushwa nchini. Aidha, watumishi wote walishiriki kwenye mafunzo ya siku mbili juu ya tathmini ya ndani ya majukumu ya tume, kwa lengo la kuinua ubora wa utendaji wa tume na kuhimiza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lina majukumu ya kusimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundi vya umma na binafsi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/11, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilitekeleza mambo yafuatayo: Lilikagua na kutoa idhibati kwa vyuo 20 na kusajili vyuo 20; lilibaini na kusajili walimu 400 katika Vyuo vya Ufundi; liliratibu mitihani katika vyuo 30; lilisimamia uandaaji wa mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo katika vyuo 20; liliratibu udahili wa wanafunzi wa shahada na stashahada katika vyuo 17; liliratibu na kudhibiti utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo 20; na liliendesha mafunzo katika vyuo 20 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya ya mafunzo ya walimu wa ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi Raia wa Tanzania, wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilitoa mikopo kwa wanafunzi 91,568 wakiwemo 23,141 36 wanaochukua masomo ya sayansi. Aidha, ilifanikiwa kukusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya Sh. 7,998,848,817.87, kati ya Sh. bilioni 21 zilizofikia muda wake wa kukusanywa;

(b) Ilihamasisha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu wajibu wa kila mdau katika urejeshaji wa mikopo kwa njia mbalimbali, zikiwemo za warsha, mikutano, vipeperushi, magazeti, redio na televisheni. Aidha, Bodi ilikamilisha kutengeneza Hifadhi Data *(database)* ya wakopeshwaji wote kuanzia mwaka 1994 hadi Juni, 2010; na

(c) Ilianza kutumia mfumo wa kupokea maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao ujulikanao kama *Online Application System (OLAS)* ambapo waombaji hujaza na kutuma taarifa zao moja kwa moja kwenye Bodi na hivyo kurahisisha zoezi zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)*, ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha upembuzi yakinifu wa ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya za Karagwe na Korogwe pamoja na kuandaa michoro ya majengo na pia kufanya makubaliano *(Memorandum of Understanding - MOU)* kati yake na Halmashauri za Wilaya husika. Kazi ya ukarabati wa vyuo imepangwa kuanza katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12;

(b) Ilidhamini mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wake 513 katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo wa kazi. Kati ya watumishi hao, 269 ni wakufunzi na 244 ni watumishi wa waendeshaji;

(c) Ilifanya ukarabati wa vituo viwili vya Ufundi Stadi vya Mwanza na Kihonda, pamoja na kununua na kufunga mashine za kisasa katika karakana ya mafunzo ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Dar es Salaam;

(d) Ilikamilisha utafiti katiti *(Tracer Study)* kwa nchi nzima ili kufahamu hali ya ajira ya Wahitimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi, ambapo sampuli ya Wahitimu 4,923 wa mwaka 2004 hadi 2009 walifuatiliwa;

(e) Iliendeleza ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufundi stadi vya Lindi, Manyara, Pwani, Makete na Kituo cha Mafunzo ya TEHAMA kinachojengwa Kipawa Jijini Dar es Salaam;

(f) Ilikamilisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii huko Njiro – Arusha ili kuanza mafunzo rasmi katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12;

(g) Ilitoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada kwa Walimu 32 katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi - Morogoro. Walimu wengine 95 walipatiwa mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya Ualimu wa Ufundi katika Chuo hicho. Aidha, jumla ya Walimu wa Ufundi Stadi 60 kutoka Tanzania Visiwani walipatiwa mafunzo ya Ufundishaji Unaozingatia Umahiri *(Competence Based Education and Training)*. Walimu wengine 21 wa ufundi stadi walipewa mafunzo ya ufundishaji wa elimu ya ujasiriamali, yaani *Master Trainers for Micro Enterprises.* Vilevile, walimu 50 wa ufundi stadi walipatiwa mafunzo ya ushauri wa kazi za kufanya baada ya kumaliza masomo *(Career Guidance and Counselling for Vocational Training Teachers);*

(h) Ilianzisha na kutekeleza mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani uitwao *Skills Enhancement Programme (SEP)* na zoezi hili lilianza na majaribio *(Pilotting)* ya makampuni saba. Chini ya Mpango huo, wafanyakazi 235 wamepatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi wa kazi. Wafanyakazi hao ni kutoka makampuni na viwanda vya Saruji - Tanga, Tumbaku - Morogoro, Mabati *(Aluminium Africa - ALAF)* - Dar es Salaam, Chemi Cotex, TPC - Moshi na Hoteli ya Movenpick.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/11, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla ya wanafunzi 7,024; kati yao 5,029 ni wa shahada ya kwanza (wanawake 1,813, wanaume 3,216). Wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu walikuwa 1,995 (wanawake 571, wanaume 1,425);

(b) Kiliendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia shughuli za taaluma na utafiti na kusambaza matokeo yake kwa wadau mbalimbali;

(c) Kilitoa machapisho ya vitabu 25 na majarida 290 na kusambaza matokeo ya utafiti katika nyanja mbalimbali kama za mazingira, ujasiriamali, nishati, utalii, sekta isiyo rasmi, TEHAMA, sayansi asilia na timizi *(Natural and Applied Sciences),* uhandisi, mabadiliko ya tabianchi, miundombinu, lugha, utawala bora na demokrasia;

(d) Kiliandaa utaratibu mpya wa ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari eneo la Buyu, Zanzibar; ambapo ujenzi huo sasa utafanyika kwa awamu tano, kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha;

(e) Kiliendeleza ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya chuo kama vile mabweni ya wanafunzi, madarasa, maabara, barabara, mabomba ya majisafi na majitaka ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(f) Kilianzisha shahada za kwanza mbili mpya *(B.A. in Kiswahili* na *B.Sc. in Actuarial Sciences),* shahada mpya tatu za uzamili *(Master's in Intergrated Sanitation Management, MSc. in Biodiversity and Conservation* na *Master's in International Trade)* na shahada mpya moja ya uzamivu *(PhD. by Coursework and Dissertation in Political Science and Public Administration);*

(g) Kilifanya ukaguzi wa kitaaluma, menejimenti na uendeshaji katika Vyuo vyake, Shule Kuu, Taasisi na Idara zote kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa na ufanisi wa shughuli zake. Ukaguzi ulifanywa na Kamati Teule ya Mkuu wa Chuo *(Chancellor's Visitation Team);*

(h) Kilianzisha mchakato wa maandalizi ya shahada mpya nne za uzamivu *(PhD. by coursework and dissertation)* katika Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, Idara ya Sayansi za Bahari, Idara ya Zoolojia na Fani ya Sayansi za Jamii;

(i) Kilianza mchakato wa kusherehekea miaka 50 ya Chuo tangu kilipoanzishwa mwezi Oktoba, 1961, kwa kuandaa shughuli mbalimbali kama midahalo, makongamano na semina; na

(j) Kilianza mchakato wa kujenga Kituo cha Wanafunzi, yaani *(UDSM Students Centre)* ikiwa ndiyo azma ya Chuo katika kusherehekea miaka 50. Juhudi za uchangishaji na kutafuta fedha zilianza pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanachuo wapya 150 wa masomo ya sayansi na 1,007 wa masomo ya Sanaa na Sayansi za Jamii na kufanya jumla ya wanachuo wapya waliodahiliwa chuoni hapo kuwa 1,157. Ukiongeza idadi ya wanachuo 946 wa mwaka wa pili na 763 wa mwaka wa tatu, jumla ya wanachuo wote ni 2,866;

(b) Kilinunua kemikali za maabara zenye thamani ya shilingi 25,706,100 kwa ajili ya kufanyia mazoezi kwa vitendo; na

(c) Kiliendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu, ambapo jumla ya wahadhiri 42 wako kwenye mafunzo ya shahada za uzamili, wawili kwenye stashahada na 54 kwenye shahada za uzamivu ndani na nje ya nchi. Mhadhiri mmoja alimaliza shahada ya uzamivu mwezi Januari, 2011 na kurudi chuoni kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitekeleza mambo yafuatayo: Kiliongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 880 hadi 950; kilianza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara; kiliendelea kuimarisha na kupanua miundombinu ya kusomea na kujifunzia; na kiliendelea kugharimia masomo ya wahadhiri 68 katika viwango vya uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza, Shahada za Uzamili na Uzamivu; na kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Kilimo, Misitu, Mifugo, Mazingira, Wanyamapori, Ufugaji wa Samaki na fani nyingine za Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kiliendeleza utafiti unaolenga katika kuinua ubora wa kilimo, hifadhi za misitu, mifugo na maliasili nyingine, ikiwa ni pamoja na matumizi ya wanyamakazi katika Kilimo sehemu mbalimbali nchini (Kisilo Wilaya ya Njombe); Mradi wa mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji (katika Wilaya za Morogoro Mjini na Vijijini na Mvomero); ambapo wakulima zaidi ya 1,300 hufaidika kila mwaka;

(b) Kiliendeleza hifadhi na ukarabati wa Chanzo cha Maji cha Mto Mzinga kwa kushirikiana na jamii;

(c) Kiliendelea kutoa elimu kwa wanavijiji juu ya umuhimu wa upandaji miti, ufugaji nyuki na kuongeza matumizi ya pembejeo na ukuzaji wa soko kwa aina za miti isiyojulikana na isiyotumika sana nchini Tanzania, chini ya Mradi wa *Programme for Agricultural and Natural Resources Transformation for Improved Livelihood (PANTIL).* Aidha, kilihamasisha Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Arusha kupanda na kutumia miti hiyo. Vilevile, Mradi huu ulitoa makala 11 kwenye majarida ya kisayansi;

(d) Kilitoa ushauri wa kitaalamu katika kilimo, mifugo, misitu, wanyamapori, umwagiliaji na tiba ya wanyama;

(e) Kiliendelea na Mradi wa Uboreshaji wa Zao la Maharage ambao umewezesha kutoa aina za maharage za 'Pesa' na 'Mshindi' ambazo hupevuka mapema na kuiva haraka wakati wa kupika; na

(f) Kilianzisha shahada mpya sita za kwanza ambazo ni *Bachelor of Science in Human Nutrition; Bachelor of Science in Family and Consumer Sciences; Bachelor of Irrigation and Water Resources; Bachelor of Bioprocess and Post-harvest Engineering; Bachelor in Applied Agricultural Extension* na *Bachelor of Agricultural Education* zilizodahili jumla ya wanafunzi 470 katika mwaka wa masomo 2010/11. Aidha, Chuo kilianzisha stashahada mbili za Maktaba ambazo ni *Diploma in Records, Archives and Management* na *Diploma in Library Information Science* na stashahada nyingine mbili za *Tropical Animal Health* na *Diploma in Laboratory Technology Science* zitakazoanza 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara cha Moshi ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Chuo kina majukumu ya kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla ya wanafunzi 3,775 (wa kike 1,469), ambapo udahili wa wanafunzi wa kike uliongezeka kutoka 980 mwaka 2009/10 hadi 1,469 mwaka 2010/11. Hili ni ongezeko la asilimia 49.9. Aidha, ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa kozi za cheti katika Kampasi ya Kizumbi (Shinyanga) na Programu mpya katika Kampasi ya Moshi.

(b) Kiliwezesha jumla ya Wahadhiri 31 kwenda masomoni kwa ajili ya shahada za uzamili (16) na uzamivu (15);

(c) Kiliimarisha matawi manne ya Kanda huko Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga na kuyafanya yajikite zaidi katika kutoa elimu kwa jamii katika masuala ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS),* utunzaji wa mazingira na mikakati ya kupunguza umaskini;

(d) Kiliendelea na ukarabati wa miundombinu na kufanikiwa kufanya yafuatayo:-

- Kuongeza ghorofa moja kwa ajili ya ofisi kwenye Jengo la Utawala *(Block B)*, ambapo ofisi 18 na ukumbi wa mikutano vimeweza kuongezwa;

- Kuunganisha Jengo la Kilimanjaro na PPP ili kupata ofisi kwa ajili ya Taasisi ya Maendeleo Endelevu ya Ushirika na Elimu;

- Kukarabati baadhi ya nyumba za wafanyakazi na vyumba vya semina na kumbi za mihadhara;

- Kutengeneza barabara za ndani katika kampasi ya Kizumbi-Shinyanga kwa kushirikiana na *VETA* Shinyanga na kukarabati majengo na zahanati;

- Kukarabati barabara za ndani na mifereji ya maji ya mvua kuzunguka eneo la utawala na madarasa katika Kampasi ya Moshi;

(e) Kilifanya upanuzi wa Zahanati ya Chuo katika Kampasi ya Moshi, ambapo jumla ya vyumba sita vimeongezwa, vikiwemo wodi ya akina mama, ofisi tatu, chumba cha kliniki na chumba cha dawa; na

(f) Kilifanya utafiti katika maeneo ya *Role of Cooperative in Regional Economy; SACCOS' Loan Recovery in Cooperative Development in Tanga*; *Role of Produce Marketing Groups in Poverty Alleviation; and Improving Crop Markets and Marketing Information System of Oil Seed Crops: The Case of Groundnuts in Dodoma Region.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina majukumu ya kutoa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na ana kwa ana, kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kupitia vituo vyake vilivyopo mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 8,973 wa cheti, stashahada na shahada (wanawake 3,209 na wanaume 5,764) katika ngazi mbalimbali ambapo, wanafunzi wa vyeti na stashahada walikuwa 3,145, wa shahada ya kwanza 3,749 na wa stashahada na shahada za uzamili na za uzamivu 2,079;

(b) Kilifanikisha kuhitimu kwa jumla ya wanafunzi 2,373 (wanawake 956). Kati ya hao, wahitimu wa stashahada, shahada za uzamili na uzamivu walikuwa 167 (wanawake 41);

(c) Kilifanya ukarabati wa majengo ya Vituo vya Mikoa ya Kagera, Rukwa, Kilimanjaro, Ruvuma na Mara. Aidha, kilifanya ukarabati katika Vituo vya Mikoa tarajiwa ya Njombe na Katavi;

(d) Kilifanikisha kupatikana kwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vituo na ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za vituo katika Mikoa ya Lindi (ekari 100), Mwanza (ekari 17), Kigoma (ekari 22), Shinyanga (ekari 68), Pemba (ekari 4) Pwani (ekari 2), Manyara (ekari 24), Dodoma (ekari 2) na Tabora (ekari 100); na

(e) Kilinunua kiwanja kilicho karibu na majengo ya Chuo huko Mbeya ili kujenga hoteli kwa makubaliano maalum na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Ardhi kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja mbalimbali zikiwemo za maeneo ya ardhi, nyumba, mazingira na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Ardhi kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 1,013 wa shahada ya kwanza, wanafunzi 64 wa shahada za uzamili na uzamivu na 19 wa ngazi ya cheti. Jumla ya wanafunzi wote chuoni ni 2,806. Hili ni ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na mwaka wa masomo 2009/10, ambapo chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 2,143. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kike pia imeongezeka kutoka wanafunzi 634 mwaka 2009/10 hadi 744 mwaka 2010/11, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.3. Idadi ya wanafunzi wa kike ni asilimia 26.5 ya wanafunzi wote waliopo chuoni. Hili ni ongezeko la takriban asilimia tatu ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Mwaka wa masomo 2009/10, wanafunzi wa kike walikuwa asilimia 24 ya wanafunzi wote;

(b) Kilianzisha Programu mpya mbili za Shahada ya Kwanza ambazo ni Uhandisi Ujenzi *(Civil Engineering)* pamoja na Fedha na Uhasibu *(Finance and Accounting);*

(c) Kiligharimia mafunzo ya wanataaluma wapya 13 na wafanyakazi waendeshaji wapya 12;

(d) Kilikamilisha awamu ya nne ya ujenzi wa jengo jipya la mihadhara na ofisi *(Lands Building)* na hivyo kuweza kupata madarasa 17 ya ziada, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,580 kwa wakati mmoja. Kukamilika kwa jengo hili pia kumewezesha upatikanaji wa nafasi za bohari kwa ajili ya programu ya uhandisi ujenzi na karakana ya Skuli ya Jiomatiki;

(e) Kilikamilisha kazi ya kutengeneza mfumo wa usambazaji wa majisafi kwenye mabweni kwa kuongeza matanki. Aidha, ilifanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya vyoo, ofisi, madarasa na mabweni na kuongeza vitanda na kukamilisha

ukarabati wa mfumo wa majitaka kwenye mabweni yote na ujenzi wa mtambo wa kuchuja majitaka. Zaidi ya hayo, chuo kilifanikiwa kujenga mabenchi 70 ya zege kwenye maeneo ya mabweni na madarasa kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi;

(f) Kiliandaa michoro ya awali ya jengo jipya la kumbi za mihadhara na ofisi za wahadhiri pamoja na ya makazi ya Makamu Mkuu wa Chuo na mabweni ya wanafunzi; na

(g) Kilikamilisha maandalizi ya maandiko manane ya miongozo na taratibu za uendeshaji wa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/11, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi 342 wa shahada ya kwanza katika fani mbalimbali za afya na tiba na wanafunzi 218 katika shahada za uzamili na uzamivu;

(b) Kilifanikiwa kumpata mshauri elekezi wa kuandaa *Master Plan* pamoja na makisio ya gharama za ujenzi wa hospitali katika Kampasi ya Mloganzila ambapo kazi imeanza;

(c) Kilifanikiwa kukamilisha taratibu zote za makubaliano ya mkopo nafuu kutoka Serikali ya Korea ya Kusini na kusaini mkataba wa mkopo huo tarehe 15 Septemba, 2010, ambapo mshauri elekezi wa ujenzi wa hospitali katika Kampasi ya Mloganzila amepatikana na kuanza kutengeneza michoro *(hospital design);*

(d) Kilifanya ukarabati wa mgahawa wa wanafunzi katika Kampasi ya Muhimbili, kumbi za mihadhara ya kufundishia katika kampasi za Muhimbili na Bagamoyo na baadhi ya nyumba za wafanyakazi zilizoko Bagamoyo;

(e) Kiliweka samani katika mgahawa mpya wa wanafunzi uliopo Barabara ya Chole Dar es Salaam na miundombinu ya mawasiliano katika jengo jipya la Kampasi ya Muhimbili;

(f) Kilikalimisha utafiti wa awali kuhusu upatikanaji wa kipimo cha kugundua ugonjwa wa malaria kwa haraka *(rapid diagnostic colour test)* na kuwasilisha taarifa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii;

(g) Kilikamilisha utafiti wa Chanjo ya Majaribio dhidi ya UKIMWI *(Clinical Trial of HIV Vaccine)* ambapo matokeo ya awali yanaonesha kuwa chanjo hii ni salama na hivyo ina uwezo wa kuufanya mwili kutengeneza vichocheo vya kinga dhidi ya Virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, bado haijathibitika iwapo chanjo hiyo ina uwezo wa kukinga

watu wasipate maambukizi mapya ya VVU au kupunguza ongezeko la Virusi vya UKIMWI mwilini; na

(h) Kiliendelea kufanya utafiti wa aina mbalimbali za magonjwa ya akina mama na watoto katika maeneo yafuatayo: Namna ya kupunguza vifo vya watoto wachanga *(perinatal mortality);* uboreshaji wa huduma ya wajawazito na wazazi hususan rufaa wakati wa dharura; matukio ya kubakwa na kudhalilishwa watoto; na unyanyasaji wa kijinsia ikijumuisha ubakaji na ukatili majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Mzumbe kina majukumu ya kutafuta, kukuza, kuhifadhi na kueneza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla wa wanafunzi 3,545 ambapo, 1,283 walikuwa wa Shahada ya Kwanza (623 wa kike), 92 stashahada (44 wa kike), 277 cheti (110 wa kike) na 1,943 wa shahada za uzamili (777 wa kike);

(b) Kiliwezesha wahadhiri 11 kujiunga na masomo ya shahada ya uzamivu na wengine 19 katika shahada ya uzamili. Aidha, wahadhiri saba walirudi kazini baada ya kuhitimu shahada za uzamivu na wengine 12 shahada za uzamili. Wahadhiri wengine 62 wanaendelea na masomo ya uzamivu na 12 uzamili;

(c) Kilikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi inayoendelea itaiwezesha hosteli kuchukua wanafunzi wengine 200, ambapo mkandarasi anakamilisha ujenzi wa kuta katika ghorofa ya nne;

(d) Kilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la ofisi za wahadhiri na kuziwekea samani;

(e) Kiliwezesha ujenzi wa kuta za maktaba kufikia kimo cha kuanza kuweka madirisha. Maktaba hiyo ikikamilika, itakuwa na uwezo wa kuchukua wasomaji 600 kwa wakati mmoja; na

(f) Kilikamilisha upatikanaji wa vitalu vitatu vilivyopo Upanga ambapo taratibu za kuhamisha miliki za viwanja hivyo kutoka *NHC* kwenda Chuo Kikuu Mzumbe zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dodoma kina majukumu ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za Ualimu, Hisabati, Sanaa na Lugha, Sayansi za Jamii, Tiba na Uuguzi, Sayansi za Kompyuta na Sayansi Asili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu cha Dodoma kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanafunzi wapya 8,000. Aidha, kilidahili wanafunzi 600 wa shahada za uzamili;

(b) Kilikamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Sanaa za Lugha na Sayansi za Jamii na kukifanya Chuo hicho kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 20,000;

(c) Kilikamilisha ujenzi wa barabara za ndani kwa asilimia 80. Aidha, miundombinu ya majisafi na majitaka inaendelea kujengwa ili kukidhi mahitaji;

(d) Kiliwezesha uchimbaji wa visima kumi na viwili vya maji kwa lengo la kupata wastani wa lita 100,000 kwa saa. Mahitaji halisi ni lita 400,000 kwa saa;

(e) Kiligharimia ununuzi wa zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia; na

(f) Kilifanya tathmini ya kitaalamu ili kuona maeneo yanayohitaji kuimarishwa katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyererem, kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada; kutoa mafunzo ya uongozi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili wanachuo 1,212 (420 - Cheti, 320 - Stashahada na 472 - Shahada ya Kwanza), ambapo wanawake ni 742 ambayo ni sawa na asilimia 61.2 ya wanchuo wote;

(b) Kiligharimia mafunzo ya wafanyakazi 14 ambapo 11 ni wanataaluma (Shahada ya Uzamivu sita, Shahada ya Uzamili watano), na wanne ni wafanyakazi waendeshaji (Shahada ya Uzamili mmoja, Shahada ya Kwanza ya Ukutubi wawili na Stashahada ya Kawaida ya Ufundi mmoja);

(c) Kilikamilisha tathmini ya Mitaala ya Programu za Cheti, Stashahada na Shahada ya Kwanza ili kuinua ubora wake. Mitaala hiyo imekwishawasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na kuidhinishwa rasmi;

(d) Kilikamilisha uandaaji wa mitaala ya ualimu kwa ajili ya Programu za Stashahada na Shahada ya Kwanza. Mitaala hiyo imekwishawasilishwa *NACTE* kwa kuidhinishwa;

(e) Kiliendelea na ujenzi wa Jengo lenye madarasa na ofisi kwenye Tawi la Chuo eneo la Bububu, Zanzibar, ambapo Jengo hilo litaanza kutumika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012. Ujenzi huo unafanyika kwa awamu tatu; na

(f) Kiliendelea kufuatilia katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi ufukweni mwa Bahari ya Hindi, Kivukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi Arusha kina majukumu ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundi katika fani za magari, ujenzi, mitambo, umeme, barabara, sayansi na teknolojia ya maabara, eletroniki na mawasiliano ya anga; kwa kiwango cha cheti na stashahada. Aidha, chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo yake ya taaluma na kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kilidahili jumla ya wanafunzi 357 wa mwaka wa kwanza ambapo kati yao 332 walidahiliwa katika ngazi ya stashahada na 25 katika ngazi ya Shahada;

(b) Kiliendesha mafunzo ya Kozi ya Awali *(Pre-Entry Course)* kwa wanafunzi wa kike 64 kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania *(TEA);*

(c) Kiliandaa mitaala minne mipya ya Programu za Ufundi Sanifu *(NTAs 4 - 6)* katika Madini Vito na Usonara *(Lapidary and Jewellery Technology);* Ujenzi na Umwagiliaji *(Civil and Irrigation Engineering);* Magari na Mitambo Mikubwa *(Heavy Duty Equipment Technology);* na Umeme wa Magari na Elekroniki *(Auto Electric and Electronics);*

(d) Kilikarabati bweni la wanafunzi wa kiume (*Hostel I*); ofisi tano za watumishi/wanataaluma *(Shamba Building)* na nyumba tano za Watumishi wa Chuo;

(e) Kiligharimia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 14 (Shahada wanne, Stashahada ya Uzamili wanane na Shahada ya Uzamivu wawili);

(f) Kilianza upanuzi wa Jengo la Utawala;

(g) Kilinunua gari moja aina ya *pick-up* ili kuinua ubora wa huduma za taaluma;

(h) Kiliendeleza Ushirikiano na Chuo Kikuu cha Camosun cha Nchini Canada kupitia Mradi wa *Education for Employment (EFE).* Wanataaluma wanne walipata mafunzo ya muda mfupi nchini Canada; na

(i) Kiliendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi Barani Afrika, chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA).*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyooneshwa katika ngazi mbalimbali, Wizara yangu ilikabiliana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2010/11. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto hizo:-

(a) Kushuka kwa kiwango halisi cha uandikishaji wa rika lengwa *(Net Enrolment Ratio (NER))* katika elimu ya msingi kutoka 95.9 mwaka 2009 hadi 95.4 mwaka 2010;

(b) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya ufundi;

(c) Upungufu wa walimu, wakufunzi na wahadhiri;

(d) Uhaba wa madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba, maabara na karakana;

(e) Uhaba wa nyumba za walimu, wakufunzi na wahadhiri;

(f) Kushuka kwa ufaulu wa Kidato cha Pili kutoka asilimia 65.3 mwaka 2009 hadi 61.8 mwaka 2010;

(g) Kushuka kwa ufaulu wa Kidato cha Nne kutoka asilimia 72.5 mwaka 2009 hadi 50.2 mwaka 2010;

(h) Ufinyu wa nafasi za kujiunga na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo idadi ya wahitimu wa elimu ya msingi na sekondari kwa mwaka ni 639,700 wakati nafasi za mafunzo ya ufundi na ufundi stadi ni 84,000 tu;

(i) Upungufu wa rasilimali watu, miundombinu na fedha kulingana na ongezeko la uandikishaji na gharama katika ngazi zote za elimu;

(j) Kushuka kwa idadi ya Wananchi wanaoshiriki katika Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) kutoka washiriki 957,289 mwaka 2009 hadi 924,893 mwaka 2010;

(k) Kukosekana kwa mfumo unaowezesha kutambua na kutumia matokeo ya utafiti unaofanyika katika maeneo mbalimbali na kuwafikishia wadau matokeo yake; na

(l) Kuimarisha utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kuoanisha taarifa za wakopeshaji na zile za Tume ya Vyuo Vikuu, Baraza la Mitihani na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya Mwaka 2010/11, Wizara imejizatiti kutekeleza yafuatayo katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Ofisi ya Kamishna wa Elimu, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya uteuzi wa wanafunzi wenye ulemavu waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi kwa ajili ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2012;

(b) Kuboresha utoaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kununua na kusambaza vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia pamoja na visaidizi katika Shule za Msingi na vitengo 317, Shule 30 za Sekondari na Vyuo vya Ualimu 7;

(c) Kuendelea kusimamia ubora wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutoa ithibati ya vitabu;

(d) Kutafsiri taarifa ya utafiti wa Mradi wa *SACMEQ III* katika Kiswahili;

(e) Kuandaa na kutangaza vipindi 576 vya redio kwa masomo ya Shule za Msingi;

(f) Kuandaa na kutangaza vipindi 52 redioni kuhusu mbinu za ufundishaji;

(g) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Elimu ya Mazingira na Elimu kwa Maendeleo Endelevu;

(h) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Kampeni ya Elimu kwa Wasichana;

(i) Kuhamasisha Menejimenti ya Wizara na Wafanyakazi wengine kuhusu upimaji wa hiari wa VVU katika sehemu za kazi; na

(j) Kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa Huduma za Unasihi katika Kanda za Ziwa, Magharibi, Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini - Magharibi na Nyanda za Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Msingi itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mwongozo na kuwajengea uwezo wasimamizi wa Elimu ya Awali na Msingi ngazi ya Mkoa na Halmashauri juu ya mwongozo wa viwango na uendeshaji wa Elimu ya Awali na Msingi;

(b) Kuandaa Mwongozo wa Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali;

(c) Kuandaa Mwongozo wa Ufundishaji wa Walimu na Waendeshaji wa Elimu ya Awali kuhusu Upimaji na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Elimu ya Awali;

(d) Kufuatilia uandikishaji wa watoto wote wa rika lengwa katika Elimu ya Awali na Msingi, mahudhurio na mikakati ya wanafunzi kubaki shuleni hadi kuhitimu;

(e) Kufanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa elimu ya awali na msingi, hususan katika upatikanaji na matumizi ya vifaa sahihi vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwemo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo;

(f) Kusimamia na kuratibu Awamu ya Pili ya MMEM na kukamilisha andiko la MMEM Awamu ya Tatu Mwaka 2012 - 2016;

(g) Kuratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu wa sayansi, hisabati na Lugha ya Kiingereza ili kuinua na kuimarisha kiwango cha taaluma katika elimu ya awali na msingi;

(h) Kuandaa na kupima mafanikio ya ufundishaji na ujifunzaji na kuratibu uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV, Ufundi Stadi na Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Elimu ya Msingi;

(i) Kufanya mapitio ya mtaala wa Elimu ya Msingi kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania, kwa lengo la kuinua ubora wa ufundishaji na kujifunza;

(j) Kuratibu Mpango wa Lishe Shuleni unaofadhiliwa na *World Food Programme (WFP)* na kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni; na

(k) Kuhuisha miongozo ya uandikishaji kwa lengo la kufafanua na kusimamia majukumu ya kila mdau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Sekondari itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 2,500 wa masomo ya Sayansi, Hisabati, TEHAMA na *English;*

(b) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa njia ya TEHAMA ikizingatia mazingira ya shule zetu za sekondari kwa kuanzia na shule 30 za majaribio;

(c) Kuendesha kambi za masomo ya sayansi kwa ajili ya wasichana ili kuwajengea uwezo wa kufaulu katika masomo hayo;

(d) Kuendesha Programu za TUSEME kwa lengo la kuwawezesha wasichana kujiamini;

(e) Kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya uandishi wa insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika; na

(f) Kufuatilia taarifa za utekelezaji wa mitaala na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Ualimu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanachuo 14,041 (Cheti 8,360, Stashahada 5,681) katika mafunzo ya ualimu tarajali na kazini na kufanya idadi ya wanachuo wote kuwa 24,600;

(b) Kuendesha mafunzo kazini kwa ajili ya walimu 2,052 wanaofundisha masomo ya sayansi, hisabati na lugha katika Shule za Msingi na Sekondari ili kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo hayo;

(c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Programu ya MWAKEM;

(d) Kuendesha mafunzo kwa wakufunzi na walimu wanafunzi kuhusu matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza;

(e) Kuendelea kusimamia na kuimarisha michezo katika vyuo 11 vya ualimu vya Serikali;

(f) Kuimarisha miundombinu ya Vyuo 10 vya Ualimu vya Serikali ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu;

(g) Kuinua ubora wa maabara za vyuo tatu vya Ualimu vya Serikali vyenye mchepuo wa Sayansi kwa kuvipatia vifaa na kemikali zinazotakiwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika vyuo hivyo; na

(h) Kuimarisha uwezo wa wakufunzi na watendaji 30 wa Idara na Vyuo vya Ualimu vya Serikali katika usimamizi wa Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu (MMEMWA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, itafanya yafuatayo:-

(i) Kuzindua mpango wa Ndiyo Ninaweza kwa lengo la kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(ii) Kuwezesha uandaaji na utoaji wa machapisho 21 ya magazeti vijijini katika kanda saba za kisomo;

(iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu ufundishaji kwa kutumia mbinu shirikishi katika Halmashauri kumi za majaribio; mfumo wa habari na takwimu katika Halmashauri za Miji 12 na Programu za EWW na ENMRA katika Halmashauri 132;

(iv) Kufuatilia na kutathmini majaribio katika Halmashauri tisa zilizo chini ya mpango wa Ndiyo Ninaweza wa kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(v) Kuandaa mafunzo kwa wawezeshaji 50 wa mpango wa Ndiyo Ninaweza kwa wanakisomo wenye mahitaji maalumu;

(vi) Kufanya utafiti ili kujua kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika Halmashauri zote nchini;

(vii) Kuratibu uandaaji wa utekelezaji wa mfumo unaoainisha sifa na viwango vya wahitimu wa Mipango ya EWW na ENMRA; na

(viii) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Elimu kwa Wote kuanzia mwaka 2000 hadi 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Juu, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kugharimia mafunzo ya wanafunzi 1,900 (Madaktari wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo) kwenye Vyuo Vikuu vya ndani;

(b) Kudhamini wanafunzi 50 raia wa Uganda wanaosoma kwenye Vyuo Vikuu hapa nchini na Watanzania 76 wanaosoma Msumbiji chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na Uganda na Tanzania na Msumbiji;

(c) Kuendelea kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa kudhamini wanafunzi watano, Raia wa China katika Vyuo Vikuu nchini;

(d) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi, kupitia vyombo vya habari, Maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu na kutembelea wadau;

(e) Kugharimia mahitaji maalum ya wanafunzi 112 wenye ulemavu katika Vyuo Vikuu nchini;

(f) Kudhamini mafunzo ya shahada za uzamili kwa wanataaluma 80 katika vyuo vikuu vya umma;

(g) Kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 40 kupitia Mpango wa DAAD;

(h) Kuratibu uteuzi wa wanafunzi 190 kwa ajili ya nafasi zinazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea ya Kusini, Uturuki, Misri na India; na

(i) Kuandaa maandiko ya Miradi ya Utekelezaji wa MMEJU katika maeneo yafuatayo: Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Vyuo Vikuu vya Umma; utafiti katika maeneo yaliyoainishwa katika Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; uendelezaji wa wafanyakazi wanataaluma na waendeshaji; TEHAMA; kuendelea kutekeleza Mradi wa Sayansi na Teknolojia katika Elimu ya Juu *(Science and Technology in Higher Education)* hasa katika ujenzi na mafunzo ya wanataaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU) na kuanza utekelezaji wake;

(b) Kuratibu zoezi la kuvijengea uwezo vyuo 15 vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika utoaji wa Elimu inayozingatia umahiri, uchambuzi wa mahitaji ya soko la ajira na masuala ya utafiti kwa kushirikiana na Umoja wa Vyuo Jamii vya Canada *(Association of Canadian Community Colleges);*

(c) Kuratibu zoezi la kufanya uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika wilaya 15 ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi;

(d) Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(e) Kukamilisha uhuishaji wa mipango, mikakati na miongozo ya utekelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(f) Kuratibu uanzishwaji wa vyuo vya ufundi stadi vya wilaya; na

(g) Kuratibu ukamilishaji wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam na cha Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Ukaguzi wa Shule itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kukagua jumla ya Asasi za Elimu 20,045;

(b) Kusimamia, kuendesha na kufanya tathmini ya kiwango cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha pili mwaka 2011 kwa kushirikiana na Idara ya Elimu ya Sekondari;

(c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa shule katika ngazi za Kanda na Wilaya; na

(d) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 70 wa shule ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Sera na Mipango itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha na kuandaa Mikakati na Miongozo ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo;

(b) Kuwasilisha kwa wadau, Sera ya Elimu na Mafunzo iliyohuishwa na kutoa elimu juu ya utekelezaji wake;

(c) Kuendelea kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu kwa kugatua mfumo wa ukusanyaji Takwimu *(Database)* kwenda kwenye Halmashauri 40 chini ya Awamu ya Pili ya MMES 2010 - 2015;

(d) Kuandaa Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Elimu *(Joint Education Sector Review)* wa mwaka 2011 unaoshirikisha wadau wa elimu;

(e) Kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya elimu katika ngazi zote;

(f) Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara *(Ministerial Strategic Plan)* na kuandaa Mpango wa Wizara wa miaka mitano unaolingana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano; na

(g) Kuandaa Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha ya Umma *(Medium Term Expenditure Framework)* wa miaka mitano kutokana na Mpango wa Wizara wa Maendeleo wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma bora za elimu kwa kuajiri watumishi wapya 833, kutoa vibali vya wataalamu wa kigeni 800, kuratibu upandishaji vyeo wa watumishi 917 na uthibitishaji kazini wa watumishi 351;

(b) Kuratibu utekelezaji wa Mkataba Mpya wa Huduma kwa Mteja;

(c) Kuratibu tathmini ya utendaji kazi wa watumishi kwa njia ya wazi *(OPRAS)* kuanzia mwezi Julai, 2011; na

(d) Kuanza kutumia mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi taarifa zote za kiutumishi kwa wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano, katika mwaka 2011/12, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu utoaji wa habari katika vyombo vya habari kuhusu matukio mbalimbali ya Sekta ya Elimu ili kuufahamisha Umma kuhusu maendeleo ya Sekta ya Elimu na kuweka kumbukumbu za matukio ya Wizara;

(b) Kukamilisha Mkakati wa Mawasiliano na Habari unaohusu shughuli za Wizara;

(c) Kuandaa na kutangaza vipindi 20 vya redio na televisheni vya kuelimisha jamii kuhusu maendeleo na changamoto za Sekta ya Elimu;

(d) Kuandaa makala 20 juu ya matukio ya Sekta ya Elimu, kwa ajili ya kuzichapisha katika magazeti;

(e) Kuratibu upatikanaji wa majibu ya maswali yanayoulizwa na wadau wa elimu kupitia Tovuti ya Wananchi *(www.Wananchi.go.tz);*

(f) Kuandaa, kuchapa na kusambaza nakala 100,000 za Jarida la *EdSDP* kwenye kanda nane za Elimu ili kuihamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza Mipango ya Elimu;

(g) Kuandaa machapisho mbalimbali yakiwemo mabango, vipeperushi, vijarida, shajara na kalenda kwa ajili ya kuwaeleza wadau juu ya sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Elimu; na

(h) Kuandaa na kuratibu Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Ukaguzi Makao Makuu ya Wizara, vituo 30 vikiwemo Vyuo vya Ualimu, Ofisi za Kanda za Ukaguzi wa Shule na Vituo vya Elimu vya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa mwaka 2011/12 kwa kuzingatia Bajeti iliyopitishwa;

(b) Kuhakikisha kuwa manunuzi ya Wizara yanafanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo;

(c) Kuhesabu mali kwa ajili ya kufunga mwaka wa fedha na kubaini na kushughulikia vifaa vinavyostahili kufutwa;

(d) Kuandaa mafunzo juu ya Sheria na Taratibu za Manunuzi ya Umma kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo;

(e) Kuweka kumbukumbu sahihi za vifaa na mali za Wizara; na

(f) Kutangaza zabuni na matokeo yake kwenye magazeti na Tovuti ya *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Kitengo cha Fedha na Uhasibu, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa ripoti mbalimbali za fedha na kuziwasilisha kwa mamlaka husika;

(b) Kuchambua Ripoti za Mkaguzi wa Nje na Mkaguzi wa Ndani na kuratibu majibu ya hoja za Ripoti ya Ukaguzi kabla ya kuyawasilisha kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali;

(c) Kuhakikisha ya kuwa malipo yanafanywa kwa kuzingatia Taratibu, Kanuni na Sheria za Manunuzi na Fedha za Umma; na

(d) Kusimamia na kushauri kuhusu Makusanyo ya Maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/12, Wakala, Taasisi na Mabaraza ya Wizara, zitatekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2011/12, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi kwa kutumia *Competence Based Education & Training Curriculum (CBET),* kwa walengwa 140 wa ngazi ya Cheti, 300 wa Stashahada na 352 wa Shahada;

(b) Kudurusu Mtaala wa *CBET* ngazi ya cheti, stashahada na shahada na kuwajengea uwezo wakufunzi wa TEWW katika kutoa mafunzo yanayozingatia uwezo na umahiri;

(c) Kutekeleza mpango mkakati wa UKIMWI wa TEWW *(HIV and AIDS Work Place Strategy);*

(d) Kufanya utafiti juu ya programu zinazotolewa na taasisi ili kubaini umuhimu wake katika jamii;

(e) Kutoa machapisho na majarida ya kitaaluma ya *Journal of Adult Education No.19* na *Studies in Adult Education No. 67;*

(f) Kujenga vyumba vya semina na kumbi za mikutano katika Kituo cha WAMO, ofisi na madarasa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma na Arusha na kukarabati jengo la makao makuu ya taasisi na kujenga hosteli ya wanafunzi katika Mkoa wa Dar es Salaam;

(g) Kuunganisha Makao Makuu ya Taasisi na Vituo vitano katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta kwa ajili ya kuinua ubora wa utoaji wa Elimu Masafa;

(h) Kuendesha mafunzo ya uratibu, usimamizi na menejimenti ya Vituo vya MEMKWA na MUKEJA katika Wilaya 75 zilizobaki;

(i) Kuratibu maandalizi ya Mkutano wa Elimu Masafa katika Nchi za *SADC (DEASA Conference)* utakaofanyika Tanzania;

(j) Kuchapa masomo ya Hatua ya I na II ya Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(k) Kuandika na kuchapa kwa mtindo wa moduli masomo ya Ufundi na Biashara kwa ajili ya Kidato cha 5 na 6;

(l) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma kupitia Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kutoka 49,533 hadi 69,533;

(m) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya *Integrated Post-Primary Education (IPPE)* katika Wilaya za Temeke, Magu, Siha, Hai, Bagamoyo, Makete na Mtwara; na

(n) Kuratibu mafunzo ya Diploma ya Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii kwa njia ya Elimu Masafa kwa Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii *(FDC)* kwa ushirikiano na *Karibu Tanzania Association (KTA)* na *Karibu Sweden Association (KSA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Taasisi ya Elimu Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya mapitio ya mitaala ili kuinua ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;

(b) Kutoa mafunzo ya kubuni na kutekeleza mtaala ngazi ya cheti na shahada; na

(c) Kujenga kituo cha mafunzo ya mtaala na utafiti wa maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuinua ubora wa huduma za Maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 19, kwa kuongeza machapisho 50,000;

(b) Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;

(c) Kutoa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa walengwa 200 wa cheti, 200 wa stashahada na 150 wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya Wafanyakazi wa Maktaba za Umma, Shule, Vyuo na Taasisi nyingine nchini; na

(d) Kuendeleza ujenzi na kuimarisha Chuo cha Mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka *(School of Library, Archives and Documentation Studies - SLADS)* Bagamoyo, kwa kuanza ujenzi wa hosteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM)*, katika mwaka 2011/12, utatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi 600 wa Idara mbalimbali za elimu, walengwa wakiwa ni Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata, Maafisa Elimu ngazi ya Wilaya, Walimu wa Shule za Awali, Msingi na Sekondari, Wafanyakazi katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na Mameneja na Wamiliki wa Shule zisizo za Serikali;

(b) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu 1,000;

(c) Kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata 2,800 nchini kote juu ya mbinu bora za kusimamia Elimu ya Sekondari katika kata zao;

(d) Kutoa mafunzo kwa wajumbe 5,000 wa Kamati za Shule juu ya usimamizi wa Elimu ya Msingi;

(e) Kutoa mafunzo kwa Wajumbe 1,500 wa Bodi za Shule juu ya usimamizi na uendeshaji wa Shule za Sekondari;

(f) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa Elimu Taaluma na Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu 86 juu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini;

(g) Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Wakuu wa Shule 240 wa Shule za Serikali na zisizo za Serikali;

(h) Kutoa mafunzo ya awali ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Wakuu wa Shule wapya 1,000 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara;

(i) Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa wakaguzi 240 kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara; na

(j) Kutoa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Maafisa Elimu 106 wa Wilaya na Mikoa ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Tume ya Taifa ya *UNESCO* itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu ushiriki wa Serikali katika kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* utakaofanyika Oktoba, 2011 Paris - Ufaransa, Makao Makuu ya *UNESCO,* pamoja na utekelezaji wa maamuzi ya kikao hicho;

(b) Kuratibu uanzishwaji wa Kikundi cha Wanawake katika Sayansi Tanzania *(STI4W Reference Group)* ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika sayansi na ubunifu;

(c) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Ushirikishwaji ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Utafiti na Uhifadhi wa Nyaraka za Masuala ya Jinsia, Tengeru - Arusha;

(d) Kuratibu ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa Programu za *UNESCO,* kupitia Dawati la Vijana la Tume ya Taifa ya *UNESCO;*

(e) Kuhamasisha shule nyingi zaidi kujiunga na mtandao wa *UNESCO* katika kutekeleza Programu za *UNESCO;* na

(f) Kuratibu mchakato wa taifa wa kuridhia Mkataba wa *UNESCO* kuhusu Kupinga Utumiaji wa Dawa za Kuongeza Nguvu Michezoni *(Convention on Antidoping in Sports).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Tanzania, katika mwaka 2011/12, litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2011 kwa watahiniwa 992,795 waliosajiliwa;

(b) Kuendesha Mitihani ya Kidato cha Nne, Maarifa (Qualifying Test- QT), Kidato cha Sita na Ualimu, ambapo watahiniwa wanatarajiwa kusajiliwa kwa ajili ya mitihani hiyo;

(c) Kutoa mafunzo kwa walimu wanaoshiriki katika kazi za Baraza la Mitihani ili kuongeza ufanisi katika utungaji wa maswali ya mitihani; na

(d) Kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya juu ya matumizi ya karatasi za *Optical Mark Reader (OMR)* katika kujibu maswali ya mtihani ili kuongeza ufanisi katika shughuli za usahihishaji Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Kituo cha Maendeleo Dakawa kitatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuendelea kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za historia ya ukombozi Kusini mwa Afrika;

(b) Kuendelea na mchakato wa kukifanya Kituo kuwa Kitovu cha Utoaji wa Elimu ya Sayansi na Ufundi *(Centre of Excellence);* na

(c) Kuandaa mpango wa kisheria wa uendeshaji wa Kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha harambee kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana wa Shule za Sekondari;

(b) Kuendelea kuimarisha miundombinu ya Shule za Sekondari 197 na Vyuo vya Elimu ya Juu vitatu kwa kufadhili Miradi ya Maboresho;

(c) Kufanya tathmini na ukaguzi wa Miradi 70 inayofadhiliwa na Mfuko wa Elimu;

(d) Kuwapatia mafunzo watumishi 30 wa Mamlaka ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi; na

(e) Kukarabati majengo yatakayokuwa Ofisi za Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutathmini ubora wa programu 100 za masomo ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki nchini kwa lengo la kuziidhinisha;

(b) Kuendesha warsha na semina tano za kuwajengea uwezo Viongozi wa Vyuo Vikuu ili kuinua ubora wa Uongozi wa Vyuo Vikuu nchini;

(c) Kukamilisha rasimu ya kanuni za utekelezaji wa Mfumo wa Tuzo Zinazotambuliwa Kitaifa *(National Qualifications Framework);*

(d) Kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uwezo wa Vyuo Vikuu vilivyopo na vipya katika kutoa elimu bora kwa kuzingatia vigezo na kutumia takwimu na taarifa mbalimbali toka Vyuo Vikuu kwa ajili ya kusaidia kutoa maamuzi sahihi kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya juu nchini;

(e) Kuendelea kuratibu na kutathmini Mradi wa Majaribio ya Udhibiti wa Ubora wa Programu za Vyuo Vikuu vitano unaotekelezwa na *IUCEA;*

(f) Kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Tume, kupitia machapisho mbalimbali na vyombo vya habari na kutoa miongozo kwa Vyuo Vikuu nchini kuhusu udhibiti wa ubora wa elimu ya juu;

(g) Kuendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu nchini na nje ya nchi;

(h) Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi za kudumu za Tume;

(i) Kuendelea kuratibu na kuandaa Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuuelimisha umma kuhusu malengo, maendeleo na mchango wa taasisi za elimu ya juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini; na

(j) Kujenga uwezo wa Wafanyakazi wa Tume katika kukabiliana na changamoto za maendeleo ya elimu ya juu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/12, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi litatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua vyuo 20 na kutoa ithibati na usajili kwa vyuo vinavyostahili;

(b) Kubaini na kusajili walimu 400 katika Vyuo vya Ufundi;

(c) Kuratibu mitaala 30 na uendeshaji wa mitihani katika vyuo 30;

(d) Kusimamia vyuo 20 katika kutengeneza mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo;

(e) Kuratibu udahili wa wanafunzi wa shahada na stashahada katika vyuo 17;

(f) Kusimamia utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo; na

(g) Kuendesha mafunzo ya walimu katika vyuo 20 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, katika mwaka 2011/12, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mikopo kwa Wanafunzi 91,568 wa elimu ya juu wa mwaka wa kwanza na wale wanaoendelea na masomo na kwa wanafunzi wanaosoma shahada za uzamili na uzamivu;

(b) Kuimarisha utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuoanisha taarifa za wakopeshwaji na zile za Tume ya Vyuo Vikuu, Baraza la Mitihani na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(c) Kutoa Elimu kwa Umma, kwa kutumia vipeperushi, magazeti, redio, televisheni, warsha na maonesho, kuhusu kuchangia gharama za Elimu ya Juu; na

(d) Kusogeza huduma za utoaji wa mikopo karibu na Wananchi kwa kuanzisha Ofisi ya Kanda huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha andiko la Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Ufundi Stadi wa Miaka Mitano *(VETA Development Corporate Plan IV) 2012 - 2017;*

(b) Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ya Vituo vya Ufundi Stadi vya Wilaya (*District Vocational Training Centres Programme)* kwa kukarabati vituo na kujenga vituo vya ufundi stadi katika Wilaya za Karagwe, Korogwe na Mwanga na kujenga chuo Ludewa. Kituo cha Ufundi cha Wilaya ya Makete, ambacho ujenzi wake unatarajiwa kukamilika hivi karibuni kitaanza kutoa mafunzo katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2011/12;

(c) Kujenga uwezo wa wakufunzi 70 na watumishi wa kawaida 50 katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi;

(d) Kufanya utafiti wa soko la ajira nchi nzima ili kubaini mahitaji ya mafunzo ya ufundi stadi kisekta, hususan stadi zinazohitajika na wawekezaji *(Potential and Emerging Skills);*

(e) Kutekeleza mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani uitwao *Skills Enhancement Programme (SEP)* kwa kampuni zisizopungua kumi nchi nzima ili kuimarisha stadi kwa wafanyakazi na tija kwa viwanda husika;

(f) Kutekeleza Mpango wa *VETA* wa kuimarisha Vyuo vya Ufundi Stadi *(Modernization of Vocational Training Centres)* kwa kukarabati Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi vya Mwanza, Moshi, Mtwara, Kihonda na Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro pamoja na kuweka mitambo ya kisasa ya kufundishia ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia;

(g) Kuanzisha mafunzo ya hoteli na utalii katika Chuo cha *VETA* cha Hoteli na Utalii huko Njiro, Arusha ambapo wanafunzi 50 wa ngazi ya Stashahada wataanza mafunzo mwezi Januari, 2012; na

(h) Kuanzisha mafunzo ya ufundi stadi katika fani za useremala, uashi, magari, umeme, upishi na TEHAMA katika vyuo vipya vya Manyara, Lindi, Pwani na kituo cha TEHAMA cha Kipawa, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 7,260 ambapo, 5,030 ni wa shahada ya kwanza na 2,230 ni wa shahada ya uzamili na uzamivu;

(b) Kuendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia utafiti na mafunzo, hasa katika nyanja za sayansi asilia na tumizi *(Natural and Applied Sciences)*, teknolojia, elimu, mabadiliko ya tabianchi, miundombinu, mazingira, ujasiriamali, nishati, utalii, sekta isiyo rasmi, TEHAMA, lugha, utawala bora na demokrasia na baadaye kutoa machapisho 30 ya vitabu na 305 ya majarida;

(c) Kuendeleza ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(d) Kuendeleza mikakati ya ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari eneo la Buyu, Zanzibar;

(e) Kuanzisha Shahada za Kwanza za *B.Sc. in Textile Engineering* na *B.Sc. in Textile Design;*

(f) Kukamilisha na kuanzisha shahada nne za uzamivu *(Ph.D by Coursework and Dissertation)* katika Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, Idara ya Sayansi za Bahari, Idara ya Zuolojia na Fani ya Sayansi za Jamii;

(g) Kuendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa shughuli za taaluma *(quality assurance);*

(h) Kuendelea kuajiri na kugharimia mafunzo ya wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji kwenye fani mbalimbali;

(i) Kuendelea na utekelezaji wa mipango ya kusherehekea Miaka 50 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuandaa Dira ya Miaka 50 ijayo ya Chuo kuendesha midahalo, makongamano na kutoa machapisho na huduma kwa umma; na

(j) Kuanza ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi *(Student Centre)* ikiwa ni azma mojawapo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kusherehekea miaka 50 ya Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wenye sifa za kujiunga na masomo ya Chuo Kikuu 1,200 (200 wa fani ya sayansi);

(b) Kununua vifaa vya maabara na samani za maktaba na vitabu zaidi vya kufundishia;

(c) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye ulemavu;

(d) Kujenga jengo la kitivo cha sayansi za jamii;

(e) Kupanua jengo la kitivo cha Elimu kwa ajili ya kuongeza ofisi kwa walimu;

(f) Kujenga jengo la utawala kwa ajili ya ofisi za wafanyakazi waendeshaji;

(g) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;

(h) Kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada za uzamili na uzamivu;

(i) Kujenga kituo cha afya ili kuwa na jengo maalum la kutolea huduma za afya;

(j) Kujenga jengo la maabara na madarasa katika shule ya sekondari ya mazoezi;

(k) Kuajiri jumla ya wafanyakazi 75; kati ya hao, 30 ni wahadhiri na 45 ni waendeshaji;

(l) Kukarabati miundombinu ya umeme, barabara na viwanja vya michezo;

(m) Kuzuia mmomonyoko wa udongo katika Hosteli ya Mbagala; na

(n) Kutengeneza *Master Plan* ya chuo na kununua/kutafuta ardhi nyingine kubwa kwa ajili ya upanuzi wa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, katika mwaka 2011/12, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 880 hadi 950;

(b) Kuanza ujenzi wa Jengo la Utawala;

(c) Kuendelea kuimarisha kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia Chuoni; na

(d) Kuendelea kugharimia masomo ya wahadhiri katika viwango vya uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanachuo 8,572 wa shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu;

(b) Kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kuanzisha shahada mpya saba za kwanza na tatu za uzamili;

(d) Kuanza mradi wa uvunaji maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji;

(e) Kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Bioteknolojia ya Kilimo *(National Agrilcultural Biotechnology Institute)* ili kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa Kilimo Kwanza; na

(f) Kufanya utafiti unaolenga katika kumwondolea mkulima umaskini, kukuza uchumi na kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi (Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo), katika mwaka 2011/12, kitatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuanzisha Programu za Cheti na Stashahada katika Kampasi ya Kizumbi, Shinyanga ili kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,652 mwaka 2010/11 hadi 4,068 mwaka 2011/12;

(b) Kuwaendeleza wahadhiri 20 katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu;

(c) Kuinua ubora wa utafiti na kuandaa makala mbalimbali ili kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii, ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS),* maendeleo ya ushirika, utunzaji mazingira na upunguzaji wa umaskini;

(d) Kuimarisha matawi manne ya chuo ya kanda katika Mikoa ya Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga;

(e) Kuinua ubora wa kiwango cha huduma za utafiti na ushauri, kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi, hususan Chuo cha Ushirika cha Uingereza, *University of Stirling* cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Zambia, *Humber Institute of Technology and Advanced Learning (HITAL);*

(f) Kuimarisha mipango ya uenezi wa elimu nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, *Co-operative Audit and Supervision Corporation (COASCO),* Muungano wa Vyama vya Ushirika *(TFC)* na wengineo;

(g) Kushughulikia mahitaji ya jamii katika masuala mtambuka kama jinsia, UKIMWI, wenye ulemavu, rushwa, mazingira na wastaafu; na

(h) Kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu Kamili *(Fully Fledged University).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, kimejizatiti kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kujenga maabara za Teknolojia ya Mawasiliano Huria katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Pemba, Lindi, Mtwara, Mara na Zanzibar;

(b) Kujenga majengo ya Kituo cha Mtwara na viwanja vya michezo eneo la Makao Makuu ya Chuo Bungo Kibaha;

(c) Kukarabati majengo ya Mikoa ya Kagera (Awamu II), Musoma (Awamu ya I) Kilimanjaro (Awamu ya II) na Rukwa (Awamu ya II); na

(d) Kuongeza udahili wa wanafunzi ili ifikie 3,961 kwa shahada ya kwanza na 2,538 kwa shahada za uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2011/12, Chuo Kikuu Ardhi, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha awamu ya tano ya ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na ofisi za wahadhiri *(Lands Building);*

(b) Kuanza ujenzi wa jengo la mihadhara na ofisi za wahadhiri;

(c) Kuanza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,048;

(d) Kuanza ujenzi wa nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo;

(e) Kukamilisha ununuzi wa ardhi kwa ajili ya upanuzi wa chuo katika Kijiji cha Lupunga, eneo la Mlandizi – Halmashauri ya Mji wa Kibaha;

(f) Kuimarisha na kupanua miundombinu ya habari, mawasiliano na teknolojia;

(g) Kuajiri wafanyakazi wapya 37 (wanataaluma 22 na waendeshaji 15); na

(h) Kukarabati barabara za ndani, madarasa, ofisi za walimu, nyumba za wafanyakazi na viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 400 wa shahada ya kwanza na 250 wa shahada za uzamili na uzamivu;

(b) Kujenga miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la Mloganzila ili kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia;

(c) Kukamilisha ukarabati wa majengo yakiwemo ya utawala, nyumba za wafanyakazi, maabara za kufundishia na mabweni;

(d) Kujenga nyumba mbili za walezi wa wanafunzi *(wardens)* na Bazaar ya wanafunzi katika mabweni ya wanafunzi yaliyopo Barabara ya Chole, Dar es Salaam;

(e) Kujenga karakana ya kutengenezea vifaa vya maabara;

(f) Kuweka majiko ya gesi na samani katika mgahawa wa wafanyakazi katika jengo jipya;

(g) Kufuatilia na kutathmini matumizi na ufanisi wa dawa za malaria katika jamii; na

(h) Kuendelea kufanya utafiti wa chanjo ya UKIMWI kwa watu mia moja na ishirini kama jaribio la pili. Utafiti huu utaratibiwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo Kikuu Mzumbe, kitatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kudahili wanafunzi 3,455; kati yao, wanafunzi 1,460 wa Shahada ya Kwanza na 1,795 Shahada za Uzamili;

(b) Kukamilisha ujenzi wa Maktaba ya Kampasi ya Mbeya yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 600 kwa wakati mmoja;

(c) Kuweka samani katika hosteli ya wanafunzi wa kike katika Kampasi Kuu Mzumbe;

(d) Kujenga vyumba vitatu vya madarasa katika Kampasi ya Mbeya;

(e) Kuimarisha mfumo wa maji katika Kampasi Kuu ya Mzumbe;

(f) Kukamilisha utafiti na kutoa ushauri mbalimbali katika maeneo ya menejimenti, uongozi na Sayansi za Jamii kwa ujumla;

(g) Kuajiri wahadhiri 14 na waendeshaji 8; na

(h) Kugharimia mafunzo ya watumishi 18 katika ngazi ya Shahada za Uzamivu na 12 katika ngazi ya Shahada za Uzamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo Kikuu cha Dodoma kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani;

(b) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Asili (kwa ajili ya wanafunzi 5,000) na Chuo cha Sayansi za Ardhi (kwa ajili ya wanafunzi 3,000);

(c) Kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo cha Elimu (Walimu wanafunzi 10,000), chuo cha Sayansi za Tiba (wanafunzi 4,500) na chuo cha Sayansi za kompyuta (wanafunzi 3,000);

(d) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka;

(e) Kuhadili wanafunzi 5,000 kwenye shahada ya kwanza na 600 shahada za uzamili; na

(f) Kuendeleza utafiti katika maeneo mbalimbali ya mazingira, uchumi na tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 450 wa Programu ya Cheti, (wanafunzi 350 wa Stashahada na Wanafunzi 490 wa Shahada ya Kwanza);

(b) Kugharimia mafunzo ya wanataaluma kumi na wafanyakazi waendeshaji kumi ikiwa ni pamoja na wanaoendelea na masomo;

(c) Kuendelea kufuatilia katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi unaotishia kubomoa baadhi ya majengo ya chuo, ufukweni mwa Bahari ya Hindi;

(d) Kuanza ujenzi wa hosteli mbili za wanafunzi katika Kampasi ya Kivukoni;

(e) Kuendeleza ujenzi katika Kampasi ya Bububu - Zanzibar;
(f) Kuajiri wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji kumi; na

(g) Kuanza mafunzo ya ualimu katika Programu za Stashahada na Shahada ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/12, Chuo cha Ufundi Arusha, kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili jumla ya wanafunzi 472 wa mwaka wa kwanza; kati ya hao, 447 ni ngazi ya Cheti na Stashahada na 25 ni ngazi ya Shahada;

(b) Kuanzisha programu nne za ufundi sanifu *(NTAs 4-6)* katika Teknolojia ya Madini ya Vito na Usonara *(Lapidary and Jewellery Technology);* Uhandisi-Ujenzi na Umwagiliaji *(Civil and Irrigation Engineering);* Magari na Mitambo Mikubwa *(Heavy Duty Equipment Technology)* na Umeme wa Magari na Elekroniki *(Auto Electric and Electronics);*

(c) Kununua vifaa na zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia katika maabara na karakana ili kuinua ubora wa ufundishaji na ujifunzaji;

(d) Kuhuisha mitaala 18 ya programu zilizopo za ufundi sanifu *(NTAs 4-6);*

(e) Kuajiri wanataaluma 40 na wafanyakazi waendeshaji 30;

(f) Kuendesha kozi ya awali *(Pre-Entry Course)* ya kujiunga na Chuo, kwa wasichana, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania;

(g) Kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10;

(h) Kumalizia upanuzi wa kumbi za kusomea, madarasa na maktaba;

(i) Kumalizia ukarabati wa Bweni Na. 2 na kuendeleza ujenzi wa awamu ya pili ya Bweni Na. 3;
(j) Kujenga mfumo wa umwagiliaji na mashamba-darasa kwa ajili ya kufundishia Programu ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji;

(k) Kufanya ukarabati wa karakana na maabara *(Mechanical, Civil, Electrical* na *Automotive Engineering);*

(l) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ujenzi na Umwagiliaji;

(m) Kuongeza viti na meza zisizohamishika *(fixed chairs and tables)* katika baadhi ya madarasa ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(n) Kuendeleza mikakati ya mapambano dhidi ya maambukizi ya Ugonjwa wa UKIMWI *(HIV and AIDS)* kwa Wanajumuiya wa Chuo; na

(o) Kuendeleza ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya kimataifa sehemu mbalimbali kama ifuatavyo: Ushirikiano na Vyuo vya Ufundi Barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA);* Ushirikiano na Chuo Kikuu cha Camosun cha nchini Canada kupitia Mradi wa *Education for Employment (EFE);* kushiriki katika Mradi wa *Technical Education and Labour Market Support Programme (TELMS)* unaofadhiliwa na Serikali ya Italia; na kushirikiana na wataalamu kutoka Japani katika kufundisha Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani za pekee kwa Wananchi, Viongozi na Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Baadhi ya Wahisani hao ni Serikali za Algeria, Canada, China, Cuba, Finland, India, Ireland, Jamhuri ya Watu wa Korea, Japan, Marekani, Misri, Norway, Pakistan, Poland, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Sweden na Uturuki. Aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu zetu za Elimu ni pamoja na *Aga Khan Education Foundation, Barclays Bank,* Benki ya Dunia *(WB),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB), CIDA (Canada), COL, CRDB, DAAD, DANIDA, DFID, EDC, GTZ, ILO, International Reading Association, Irish Aid, JICA, JOVC, KOICA, NBC, NMB, NORAD, OPEC, Oxfam, Peace Corps, Plan International, Sida (Sweden),* Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU), UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, USAID, VSO, WFP, Sight Savers International, UNESCO Institute for Life Long Learning (UIL), Book Aid International, BP, Care International, CBP, Children International, Winrock International, World Vision na Airtel. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Viongozi wa Matawi ya CWT, RAAWU, THTU na TUGHE kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapofika mwisho wa hotuba hii, ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa shukurani zangu nyingi na za dhati kwa mke wangu Saumu na watoto wetu; Mariam, Karim na Malick; kwa upendo na kwa kunipa moyo, kwa ushirikiano na kwa kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mbalimbali ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu, lipitishe Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya jumla ya Shilingi 659,296,862,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/12 ili kuiwezesha Wizara kutekeleza Mpango wake. Katika maombi haya:-

Shilingi 71,767,219,156 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara ambapo: Shilingi 34,433,671,000 zinaombwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 37,333,548,156 zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo; Shilingi 452,015,541,460 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi 170,072,086,000 zinaombwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi 281,939,460,844 zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 135,518,096,000 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kati ya hizo, Shilingi 41,098,534,000 ni fedha za ndani na Shilingi 94,419,562,000 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kwa mara nyingine tena, nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa hoja yako. Hoja imetolewa na kuungwa mkono na sasa ninaomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii.

**MHE. MARGARET S. SITTA (MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114 (11), ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa siku ya leo. Ninawashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Tabora kupitia UWT na chama changu cha Mapinduzi, kwa kuniwezesha kuwa Mbunge na ninawaahidi ushirikiano wa hali ya juu.

Ninaishukuru pia familia yangu, inayoongozwa na Mheshimiwa Samuel J. Sitta, Mbunge, kwa ushauri na ushirikiano mkubwa wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti, ukiwemo wewe mwenyewe, kwa kuchaguliwa kutuongoza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kazi za Kamati hii ni kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, mwezi Machi 2011, Kamati ilikutana na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kupata Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Chuo, mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo. Aidha, mwezi Aprili, 2011, Kamati ilikutana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Tume ya Rais ya Kushughulikia Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mapendekezo na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa taasisi hizi ni sehemu ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Mei, 2011, Kamati ilikutana Dar es Salaam kufikiria na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii yenye Fungu 46, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, iliyowasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, Kamati inampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa uamuzi aliouchukua wa kuwapongeza wanafunzi 20 waliofaulu vizuri katika Mitihani ya Kidato cha Sita ya Mwaka 2010/2011. Hatua hii ni nzuri kwani inasaidia kuibua ushindani baina ya Wanafunzi, Walimu, Shule, Wilaya na Mikoa na hivyo kuongeza kiwango cha ufaulu nchini. Kamati inategemea pongezi hizi zitawajumuisha pia wanafunzi watakaofanya vizuri katika Elimu ya Vyuo Vikuu nchini katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha tarehe 30 - 31 Mei, 2011, Kamati ilielezwa jinsi Wizara ilivyotekeleza malengo yake ya bajeti na mtiririko wa fedha kutoka Hazina kuwa, jumla ya shilingi 533,974,403,704.00 iliidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011, shilingi 407,023,946,725.00, sawa na asilimia 76 ya Bajeti ya kawaida *(recurrent),* zilitumika. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Wizara hii ilipangiwa kutumia shilingi 139,632,007,000.00. Kati ya hizo; shilingi 44, 652,142,292, sawa na asilimia 32 ya bajeti ya maendeleo zilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha elimu na mafunzo nchini. Serikali imetekeleza ushauri huo kama ifuatavyo:-

(a) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo kwa wenye mahitaji maalumu;

(b) Kutoa vibali vya kusajili Shule za Sekondari kwa kuzingatia uwepo wa Maabara zenye vifaa;

(c) Kutekeleza mpango wa ufundishaji kwa njia ya TEHAMA; na

(d) Kukabiliana na changamoto zinazokabili elimu ya msingi ikiwemo kushuka kwa ufaulu hasa katika masomo ya Sayansi.

(e) Wizara imeanza kugharamia mahitaji maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi *(MUCCOBS)* na Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA).* Aidha vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, vilinunuliwa na kusambazwa katika shule na vitengo vya shule za msingi 317; shule za sekondari 30; na vyuo vya ualimu 7. Aidha, Mamlaka ya Elimu Tanzania iliipatia *UDSM* vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu vyenye thamani ya shilingi 153,295,000.00.

(f) Kutoa vibali vya kusajili shule za Sekondari kwa kuzingatia uwepo wa maabara zenye vifaa. Kamati ilielezwa kwamba, moja ya vigezo vikuu vya kuwezesha shule kusajiliwa ni shule kuwa na maabara tatu (ya Fizikia, Kemia na Biolojia). Wizara inahimiza kuwepo kwa maabara zenye vifaa vinavyofanya kazi katika kila Shule ya Sekondari. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO*, imeanzisha utaratibu wa kutoa Vivunge vya Sayansi *(Science Micro Kits)* katika Shule za Sekondari za Wilaya 35 za majaribio.

(g) Kutekeleza Mpango wa ufundishaji kwa njia ya TEHAMA; Shule 150 za Msingi katika mikoa minane zinanufaika na Elimu kwa njia ya TEHAMA kupitia Mradi wa *Bridge – it* unaofadhiliwa na Shirika la *USAID*. Kila shule imepatiwa *TV* na simu za mikononi za aina ya Nokia kufundishia masomo ya Sayansi na Hisabati kwa Darasa la V na la VI. Aidha, jumla ya watendaji 1,103 wamepewa mafunzo kuhusu utekelezaji wa utoaji elimu kwa njia ya TEHAMA.

(h) Kukabiliana na changamoto zinazoikabili Elimu ya Msingi ikiwemo kushuka kwa ufaulu hasa katika masomo ya Sayansi. Wizara imeendesha mafunzo kwa walimu 1,210 wa elimu ya msingi wanaofundisha masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza. Aidha, mwongozo wa ufundishaji wa Sayansi kwa Vitendo umeandaliwa na uko tayari kwa majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati. Hivyo, kuna ushauri wa Kamati ambao utekelezaji wake haujakamilika na maelezo ya Serikali yanaonesha kuwa, mchakato wa kuyafanyia kazi unaendelea. Kwa mfano, Serikali ilishauriwa kutenga kiasi cha asilimia nne badala ya asilimia mbili ya Ushuru Maalumu wa Kuendeleza Mafunzo ya Ufundi *(Skills Development Levy)* kwa ajili ya *VETA.* Taarifa ya Utekelezaji ilionesha kuwa, Wizara imewasilisha ombi hilo HAZINA. Kwa maelezo haya ni wazi kuwa, utekelezaji bado haujakamilika. Kamati inahitaji taarifa kuhusu utekelezaji wa ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa maoni haya, Kamati ilielezwa pia mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika mwaka 2010/2011 ikiwemo kukamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo. Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa, Kamati ilihoji kuhusu maeneo yafuatayo:-

- Mikakati mahususi inayochukuliwa na Serikali kuongeza uwezo wa *VETA* kutoa elimu ya ufundi kwa idadi kubwa ya vijana wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari, ambao hawakuendelea na Elimu ya Juu;

- Suala la Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini ambalo limekuwa moja ya chanzo cha migogoro ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;

- Ufaulu mdogo wa wanafunzi katika matokea ya Kidato cha Nne ya mwaka 2010/2011;

- Ujenzi wa nyumba za walimu wa Shule za Msingi na Sekondari;

- Umuhimu wa mafunzo kazini kwa walimu kuendana na mabadiliko ya mitaala ya kufundishia; na

- Madai mbalimbali ya Walimu na Wahadhiri yakiwemo malipo ya nyumba za Wahadhiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekusudia kukusanya mapato yenye jumla ya Sh. 121,766,401,334/=. Aidha, Wizara imeomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 659,296,862,000/=, kati ya fedha hizo Sh. 523,778,776,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida *(recurrent expenditure)* na Sh. 135,518,096,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo *(development)* kwa mwaka 2011/2012. Uchambuzi ulionyesha kuwa kiasi kinachopangwa kukusanywa na Wizara kama maduhuli ya Serikali ni asilimia 20.19 ya bajeti iliyopangwa katika fungu 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia Taarifa ya Waziri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Kamati haikuridhika na mgawanyo wa fedha za bajeti kutozingatia vipaumbele vya Wizara na hivyo kutoa ushauri wa kuhamisha fedha katika baadhi ya vifungu vya Wizara *(reallocation)* ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2011/2012, Kamati ilibaini kuwepo upungufu wa fedha kiasi cha Sh. 146,500,000,000/=. Kutokana na hali hiyo pamoja na mambo mengine, Kamati yangu ilimpa Waziri muda zaidi ili aweze kushughulikia upungufu huo na kuleta mrejesho mbele ya Kamati wakati wa Vikao vya Bunge hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara Dodoma kupata mrejesho wa mapendekezo ya Kamati. Taarifa aliyoitoa Waziri kwa Kamati ilionyesha kuwa, Jumla ya Sh. 84,000,000,000/= ambazo ni asilimia 57.3 ya upungufu wa bajeti uliyodhihirika ziliongezwa na Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati yangu. Kati ya Fedha hizo, Sh. 77,600,000,000/= ziliongezwa kwenye fungu la mikopo ya Elimu ya Juu na Sh. 6,400,000,000/= kwa ajili ya kugharamia deni la nyumba za Wahadhiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za haraka na kuweza kutenga fedha zilizohitajika kugharamia mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Mwaka 2011/2012 na posho ya nyumba kwa Wahadhiri nchini. Aidha, ni vyema wanafunzi wa Elimu ya Juu kuthamini hatua za Serikali katika kutoa mikopo ya Elimu ya Juu, na hivyo watumie nafasi hiyo vizuri kwa manufaa ya Taifa. Hali kadhalika, Serikali ihakikishe kuwa fedha za mikopo ya wanafunzi zinatolewa kwa muda muafaka badala ya kuzichelewesha kwani husababisha migogoro na kuathiri ratiba za masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhika na majibu ya hoja za Wajumbe yaliyotolewa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi hasa baada ya kuahidi kushughulikia upungufu, na hivyo kupitia bajeti ya Wizara hii kifungu kwa kifungu na hatimaye kukamilisha zoezi zima la kufikiria na kujadili bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni katika Elimu ya Msingi. Kwa kuwa wanafunzi wanatumia muda mwingi wa kazi wakiwa shuleni, ni wazi kuwa wanahitaji huduma ya chakula ili waweze kupokea mafunzo na stadi za maisha wanazojifunza. Kamati inashauri kuwa ni vyema Mikoa mingine kuiga hatua zilizochukuliwa na Mikoa ya Mbeya na Iringa kutoa huduma ya chakula shuleni kwa kuwa huduma hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kufanya wanafunzi watulie shuleni. Aidha, Halmashauri zihimizwe kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia yakiwemo madarasa, madawati, ofisi, vyoo, nyumba za walimu, vifaa vya kufundishia na maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa pamoja na jitihada za Serikali za kuandaa idadi kubwa ya walimu wa shule ya Sekondari nchini, wengi wa wahitimu katika taaluma ya Ualimu wanaopangiwa vituo vya kazi Mikoani, Wilayani na Shule za Kata kwa ujumla hawafiki katika vituo hivyo vya kazi. Athari yake ni kuwa shule nyingi zimekuwa na walimu wachache ambao wanafundisha zaidi ya idadi ya vipindi vinavyokubalika. Kamati inashauri kwamba:-

· Serikali irudishe utaratibu wa kutoa posho maalumu kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu Vijijini ili wavutike na kubaki katika maeneo yao ya kazi *(Teachers Retention Scheme);* na

· Ujenzi wa nyumba za walimu upewe kipaumbele katika maeneo yenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ugatuaji umepeleka Elimu ya Sekondari nchini kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ni vyema Bunge kupitia Kamati ya Huduma za Jamii lipewe nafasi ya kupata Taarifa kuhusu maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika ngazi ya Halmashauri ili kuweza kufuatilia vyema majukumu ya Kamati katika kusimamia Sekta ya Elimu. Aidha, ni vyema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na TAMISEMI kushirikiana kwa karibu zaidi katika utendaji kazi wa Sekta ya Elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Elimu katika ngazi zote kwa kutenga fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yake. Aidha, suala la kufanya Idara hii kuwa Taasisi inayojitegemea lifanyiwe kazi. Aidha, Shule binafsi ziendelee kukaguliwa katika kusimamia ubora wa elimu na mitaala inayotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ualimu ni taaluma ya muda mrefu nchini na inaendelea kukua mwaka hadi mwaka lakini taaluma hii haina chombo mahsusi kwa ajili ya kuitolea mwongozo na udhibiti wa kimaadili na mwenendo *(Professional Board)* kama zilivyo taaluma nyingine zikiwemo Uhasibu na Udaktari. Hivyo, Kamati ina ushauri kwamba, ni vyema kada ya Ualimu/Uhadhiri iundiwe chombo mahsusi kwa kutambua na kusajili wanataaluma hawa, kudhibiti maadili na mwenendo, ili kumaliza tatizo la watu wasio na taaluma kufanya kazi hii bila maadili husika. Hatua hii itaisaidia Serikali katika kutambua na kutatua changamoto mahsusi kulingana na mazingira husika na hivyo kuimarisha utendaji kazi wa Walimu nchini. Aidha, mafunzo kwa vitendo yanayotolewa kwa wanafunzi vyuoni yakiwa ni pamoja na ya Ualimu *(BTP)* yapewe uzito wa kutosha kwani kiwango cha fedha kinachotolewa kwa mwanafunzi wa Ualimu kwa siku bado ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Elimu ya Ufundi, kwanza inasema mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi ni muhimu sana katika kuandaa idadi kubwa ya vijana ambao hawakubahatika kuendelea na Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu kwa kuwapatia ujuzi mbalimbali utakaowawezesha kuajiriwa na kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kwamba wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari bila kupata nafasi ya kuendelea na masomo ni 770,245 kila mwaka. Uwezo wa Vyuo vya *VETA* pamoja *FDC* ni wanafunzi 125,000 tu kwa mwaka, sawa na asilimia 16.2 ya wahitaji wote. Hivyo kundi la vijana ambalo halina mahali pa uhakika wa ajira kwa waliomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari ni takribani 645,245 kwa mwaka. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, zoezi la ujenzi wa Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya likamilike ili Vyuo hivi vianze kutoa huduma mapema iwezekanavyo. Takribani Wilaya 136 hapa nchini zikikamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya, zaidi ya wanafunzi 81,600 watachukuliwa kila mwaka kwani kila Chuo cha Wilaya kinategemewa kuchukua vijana 600 kwa mwaka.

Pili, mpango maalumu uandaliwe utakaowawezesha wahitimu wa Vyuo vya *VETA* kujiendeleza kitaaluma na kufikia ngazi ya juu ya ufundi ikiwemo Stashahada/Shahada na kuendelea. Pia vipaumbele katika ujenzi wa Vyuo hivi vielekezwe katika Wilaya zenye upungufu wa taasisi za mafunzo. Aidha, panapokuwa na mipango ya misaada katika Sekta hii ya Elimu na Ufundi, Mikoa yenye upungufu iangaliwe kwanza. Kamati inapenda kujua hatima ya Tume/Kamati iliyoundwa

kushughulikia uoanishaji wa *VETA* na Vyuo vya Ufundi *(FDC)* ili kuongeza uwezo wa utoaji wa mafunzo ya ufundi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ulikuwa katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ambayo inatakiwa iimarishwe kwa ajili ya kusimamia utoaji na urejeshaji mikopo na Elimu ya Juu.

Takwimu zinaonyesha kwamba ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu nchini kutokana na ongezeko la Vyuo vya Elimu ya Juu nchini limesababisha ongezeko la mahitaji ya kiasi cha fedha zinazotolewa na Serikali kugharamia mikopo hiyo mwaka hadi mwaka kama jedwali linavyoonesha.

| **Na.** | **Mwaka** | **Idadi ya Wanafunzi** | **Kiasi cha fedha za Mikopo iliyotolewa** |
|---|---|---|---|
| 1. | 2005/06 | 42,729 | 56,111,371,483.00 |
| 2. | 2006/07 | 47,554 | 76,193,757,565.00 |
| 3. | 2007/08 | 54,670 | 110,751,964,205.00 |
| 4. | 2008/09 | 58,798 | 139,093,681,094.00 |
| 5. | 2009/10 | 72,035 | 186,484,719,680.71 |
| 6. | 2010/2011 | 96,328 | 185,000,000,000.00 |
| 7. | 2011/2012 | 109,092 | 323,900,000,000.00 |

Chanzo: Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Juni 2011

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la mahitaji, Kamati inashauri kwamba, Serikali iimarishe uwezo wa kuendelea kutoa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini, kama ifuatavyo:-

· Serikali kutafuta mbinu mbadala za kupata fedha kuinua uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaoongezeka mwaka hadi mwaka;

· Katika kutoa mikopo husika, vigezo maalumu vitumike kuwatambua walengwa/wenye uhitaji ambao ni wanafunzi kutoka familia zenye kipato duni;

· Ili kuimarisha urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa tangu mwaka 2006, kiundwe chombo mahsusi chini ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, kufuatilia ukusanywaji wa marejesho ya mikopo iliyokwishatolewa. Aidha, taarifa za mikopo husika zitambulike kwa walengwa ili kurahisisha ukusanyaji wa fedha hizo kwa ushirikiano wa Mwajiri na Bodi ya Mikopo; na

. Fedha za Marejesho ya mikopo hiyo na matumizi yake zitambulike bayana kwa kuonekana katika taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kila mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha mchakato mzima wa utoaji na hatimaye urejeshwaji wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, Kamati inaushauri kwamba:-

- Ni vyema zoezi zima la utoaji Vitambulisho ya Taifa likamilike ili kuweza kutambua wanafunzi wanaokopa na waliokopa na uraia wao;

- Uwepo utaratibu wa kueleweka wa kutoa taarifa kwa mwanafunzi kuhusu taarifa za mikopo kwa ujumla katika kila mwaka wa masomo;

- Kuanzisha Dawati la Malalamiko katika Taasisi hii ili wadau waweze kutoa kero zao na kupata ufumbuzi mapema iwezekanavyo;

- Kuwepo uhusiano wa wadau wa mikopo ikiwemo mwanafunzi, Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)*, Vyuo vya Elimu ya Juu, Hazina na Bodi ili kuweza kubadilishana taarifa;

- Kuwepo na Ofisi za Bodi ya Mikopo kikanda ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hii kwa wanafunzi hasa walio katika maeneo ya Mikoa ya pembezoni; na

- Kudhibiti ongezeko la karo hasa katika Vyuo visivyo vya Serikali Mwaka hadi Mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lililotiliwa mkazo ni utulivu katika maeneo ya Vyuo nchini ambalo ni muhimu sana. Kamati inasikitishwa na hali ilivyo katika baadhi ya Vyuo Vya Elimu ya Juu nchini, kwani ni vyema Serikali itafiti vyanzo vya migomo na migogoro katika Vyuo vya Elimu ya Juu hasa vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hisia kwamba migomo ya wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu inatokana na ushabiki wa kisiasa, pamoja na ushawishi wa Viongozi wa Vyama vya Siasa. Kamati inashauri kuwa iwe ni marufuku kwa viongozi wote wa vyama vya siasa kufanya Mikutano ya Kisiasa katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Kwa misingi hiyo, maeneo ya Vyuo vya Elimu ya Juu, "*University Compasies*" yatumike kwa shughuli za mafunzo na utafiti pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ina ushauri kuhusu Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)*. Utaratibu wa kukagua utoaji wa Elimu katika Vyuo Vikuu bado haujaeleweka vizuri. Mihula ya masomo kwa njia ya Semista imekuwa ikitumika na vyuo vingi nchini. Lakini imeonekana katika baadhi ya Vyuo kwamba, wanafunzi wamekuwa wakilundikiwa vipindi inapofikia karibu na vipindi vya mitihani. Kamati inashauri kwamba *TCU* iandae utaratibu madhubuti wa kutathimini utoaji wa elimu katika ngazi hii ikiwemo majengo yanayokidhi mahitaji ili kupata wahitimu walioandaliwa vyema kutumikia nchi katika taaluma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM)*, kwamba miundombinu imekuwa ya muda mrefu mno na hivyo kuhitaji ukarabati wa hali ya juu ikiwemo hosteli, maji taka, na lifti. Chuo hiki pia kinahitaji

bwalo linaloweza kuhudumia wanafunzi wote kwa mara moja. Katika hili Kamati inasisitiza kwamba Serikali itumie mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vya fedha mbalimbali ikiwemo majengo ya Mji wa Mlimani *(Mlimani City)* kukarabati miundombinu ya chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni malalamiko ya muda mrefu sasa kwa wahadhiri kupata mwongozo wa malipo ya Uzeeni *(Pension).* Kamati inasisitiza kwamba tatizo la malipo ya uzeeni linalowakabili Wahadhiri nchini litafutiwe ufumbuzi wa kudumu mapema iwezekanavyo. Hali kadhalika, suala la utofauti wa viwango vya mishahara kati ya Wahadhiri na Wafanyakazi katika Vyuo vya Elimu ya Juu litafutiwe ufumbuzi wa kudumu. Watumishi wapate stahiki kulingana na viwango vya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu ni muhimu sana. Ni dhahiri kwamba vijana waliopata mafunzo ya JKT baada ya kumaliza masomo ya Sekondari wamekuwa na utayari wa kuitumikia nchi yao katika uzalendo wa hali ya juu. Katika hili, Kamati inashauri kwamba utaratibu wa Vijana kupitia Mafunzo ya JKT urejeshwe kwani mafunzo haya ni msingi katika kuwajengea vijana dhana nzima ya kuipenda, kuitumikia na kuilinda nchi yao na hivyo kuimarisha uzalendo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa Fedha za Bajeti ya Wizara ambao ushauri wake ni kama ifuatavyo; katika kupitia vifungu vya Wizara hii, Kamati ilibaini kwamba kiwango kikubwa cha fedha za bajeti ya Wizara kimekasimiwa kuendesha shughuli za Makao Makuu (Wizarani) ikiwemo mafunzo mbalimbali. Mfano, mafunzo ya kuzuia rushwa *(anti corruption)* kwa Watendaji wa Wizara hutengewa fedha mwaka hadi mwaka. Kamati inashauri kwamba ni vyema mafunzo ya aina hii yakatolewa kwa Watendaji katika Taasisi za Wizara wakiwa ni watoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Watu Wazima ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii. Kamati inasisitiza kwamba jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha Elimu ya Watu Wazima nchini ambayo imeonekana kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa elimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ni jambo la muhimu sana. Suala la hatima ya wanafunzi wa kike wanaoachishwa masomo baada ya kupata ujauzito shuleni litolewe uamuzi kwani limeshughulikiwa kwa muda mrefu na kutumia kiasi kikubwa cha fedha katika kufanya utafiti nchi nzima, lakini hadi sasa halijatolewa uamuzi. Hali kadhalika elimu ya afya inatakiwa iimarishwe shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Spika na Ofisi yake kwa kushirikiana na Kamati yangu kila tunapohitaji ushauri wake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Philipho A. Mulugo na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Khamisi O. Dihenga kwa kushirikiana na Kamati kwa wakati kila inapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa busara, uzalendo na umakini katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa bajeti ya Wizara hii. Aidha, mahudhurio yao katika shughuli za Kamati yamekuwa mazuri. Kwa kuuthamini ushirikiano huo, naomba niwatambue mmoja mmoja kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Dkt. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Anna MaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Dkt. Seif S. Rashidi, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Rashidi Ali Omar, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Highness S. Kiwia, Mheshimiwa Antony G. Mbassa na mimi mwenyewe Mheshimiwa Margaret S. Sitta - Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Happiness Ndallu, kwa kuratibu vyema na kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili likubali kuidhinisha Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii. Sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, karibu.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa hotuba yangu, naomba nieleze bayana kwamba kutokana na muda, sitasoma ripoti nzima, kwa hiyo, naomba Idara cha *Hansard* kirekodi hotuba kama ilivyo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge hili, kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa maoni yetu, naomba nikishukuru chama changu cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA. Vile vile na kwa umuhimu wa kipekee namshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami natoa ahadi kwao kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, kuwatumikia wananchi na Taifa langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani zangu za dhati kwa Baraza la Wanawake Chadema *(BAWACHA)*, kwa kunichagua kuwa miongoni mwa Wabunge wa Viti Maalumu kuiwakilisha Singida Bungeni. Aidha, nakishukuru Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kubuni utaratibu uliotumika kutuchagua Wabunge wa Viti Maalumu wa chama chetu bila manung’uniko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, napenda kuipongeza familia yangu pamoja na wazazi wangu, Baba Mchungaji na mama Mchungaji Gerson Mtinda kwa kunipa msaada mkubwa na kuniombea katika kazi hii ninayoifanya. Nasema Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu ya kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi, Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ualimu, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi pamoja na Taasisi na Mabaraza yaliyo chini yake. Aidha, Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini. Wizara, pia ina wajibu wa kufanya mapitio, kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sera, mipango, sheria na kanuni za elimu zilizopo, kulingana na mabadiliko ya dira ya Serikali na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya awali ni mafunzo ya awali ambayo humwandaa na kumjenga mtoto katika mchakato mzima wa shule. Ingawa Wizara imeshaandaa mtaala wa elimu ya awali, lakini elimu hii haijaenea sana vijijini. Taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2010 inaonyesha ongezeko la 3.3% ya wanafunzi waliojiunga na shule hizo za awali kutoka 896,146 mwaka 2009 hadi 925,465. Hili ni tatizo kwani tafiti zote zinaonyesha umuhimu wa elimu ya awali katika kumjengea mtoto msingi imara wa elimu katika ngazi zinazofuata. Vile vile tafiti zimeonyesha kwa uwazi kabisa umuhimu wa elimu ya awali katika makuzi bora na maendeleo endelevu ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuelewa umuhimu wa shule hizi za awali kwa maendeleo ya Sekta ya Elimu hapa nchini, hivyo basi, ni bora shule hizi zikawekwa katika mfumo rasmi wa uendeshaji katika Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ijipange vizuri ili kila mtoto hapa nchini mwenye umri kati ya miaka minne na mitano ahudhurie elimu ya awali kabla ya kujiunga na Elimu ya Msingi. Shule hizi au vituo hivi vya Elimu ya Awali vigharimiwe na Serikali za Mitaa, chini ya usimamizi wa Maafisa Watendaji wa

Serikali hizo na kuongozwa na walimu wastaafu, hasa akina mama, ambao kwa ngazi hii wanafaa zaidi kuliko akina baba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hilo, Serikali inapaswa kujipanga vizuri ili kukabiliana na changamoto zilizopo. Kuna changamoto tatu. Ya kwanza ni uchache wa Shule za Awali zinazomilikiwa na Serikali. Ya pili, ni upungufu wa walimu wenye taaluma ya mafunzo ya Elimu ya Awali, na changamoto ya tatu ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia Elimu ya Awali (Picha/Michoro, vitabu vya kiada na ziada).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu zilizotolewa katika taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2010 kuwa kuna wanafunzi 883,667 katika Shule za Awali za Serikali 41,798. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa takwimu sahihi ya idadi ya waalimu halisi waliohitimu au ni wangapi ambao wapo wanaofundisha shule hizo za awali za Serikali na pia tunataka tuambiwe ni vyuo vingapi na ni vipi vinatoa mafunzo kwa waalimu wanaokwenda kufundisha katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kabisa kuwa Serikali imerudisha jukumu la kuendesha na kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari TAMISEMI. Hata hivyo, raslimali za kuendeleza elimu zimebakizwa Wizara ya Elimu. Kitendo hiki cha kugatua majukumu peke yake bila ya kugatua na raslimali za utekelezaji wake zinakwamisha sana Halmashauri zetu kutekeleza majukumu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi matakwa ya elimu bora, ni lazima Kitengo cha Ukaguzi wa Elimu kwa ngazi zote, yaani Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari kufanya kazi mara kwa mara. Kitendo cha kukiachia kitengo cha ukaguzi kutegemea mawasilisho ya makato ya ada ya Sh.500/= kwa kila ada ya mwanafunzi kwa kila shule ni kukifanya Kitengo cha Ukaguzi kudumaa na kutokufanya kazi yake ipasavyo. Hii maana yake ni kwamba kwa zile shule ambazo hazitaweza kuwasilisha kiasi hicho cha pesa maana yake ni kwamba hazitaweza kukaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itenge bajeti kamilifu kwa kitengo hiki cha ukaguzi na ripoti yake iwe inafanyiwa kazi na vitengo husika ili kuweza kurekebisha kasoro zilizopo katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri akijibu swali Na. 66 hapa Bungeni tarehe 14 Februari, 2011 alisema kwamba, nanukuu: “Idara imeanzisha utaratibu wa ukaguzi wa shule kwa kuzingatia makundi ya ubora ambapo shule zilizo chini ya kiwango zitakaguliwa mara nyingi zaidi ili kuinua kiwango cha ubora. Vilevile Wizara katika utaratibu wake wa kuimarisha ukaguzi wa shule, imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Shule kwa lengo la kuwawezesha Walimu Wakuu na Waratibu Elimu Kata kama Wakaguzi wa Ndani na wa karibu wa shule, kusimamia shule ili ziweze kujiletea maendeleo kwa kuzipatia msaada endelevu wa kitaalamu na kitaaluma”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kazi ya ukaguzi haipaswi kufanywa na walimu Wakuu wa Shule, kwani hata Mwalimu Mkuu

naye anatakiwa kukaguliwa. Je, utaratibu upi utatumika? Ifahamike kuwa huyu ndiye msimamizi wa masuala ya shule, hivi atakuwa tayari kujikosoa yeye mwenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kubadili mfumo wa Elimu ya Msingi ili iweze kujitosheleza kwa kuhakikisha kuwa wahitimu wanapata maarifa na stadi za maisha zitakazowawezesha kujitegemea pindi watakapomaliza masomo yao na kukosa fursa za kujiendeleza zaidi kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inapendekeza maboresho yafuatayo ili kuweza kuinua na kuimarisha kiwango cha Elimu ya Msingi hapa nchini:-

(i) Muda wa Elimu ya Shule ya Msingi usogezwe kutoka miaka saba ya sasa hadi kufikia miaka tisa au kumi. Hii inamaanisha kuwa watoto watamaliza shule wakiwa na umri wa kati ya miaka 15 na 17, umri unaomwezesha kijana kukaribia sana kuanza maisha ya kazi, kwa mujibu wa sheria za nchi na sheria za kimataifa. Pia utaratibu huu utakwenda sambamba na zoezi linaloendelea la Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhuisha mfumo wa mitaala kuweza kufanana na hivyo kuwa na elimu inayofanana na mpaka sasa ripoti ya awali imeshawasilishwa Wizarani.

(ii) Mtaala wa Elimu ya Msingi upanuliwe kwa kuingiza muhtasari wa Kidato cha Kwanza na cha Pili cha sasa kuwa sehemu ya Elimu ya Msingi. Aidha, katika upanuzi huu wa mtaala, fursa kwa vijana wengi kupata utaalam na stadi za kujitegemea mapema itazingatiwa, ikiwa ni pamoja na kuingiza katika mtaala huo, elimu ya uzazi na mahusiano, kuwiana na umri wa mwanafunzi na utawapatia vijana wa kike stadi za kuweza kujikinga na tatizo la kuanza ngono katika umri mdogo, na hivyo kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la mimba za utotoni.

(iii) Ujenzi mpya, uboreshaji na ukarabati wa shule zote za msingi nchini, kwani shule nyingi katika ngazi ya Elimu ya Msingi hazina vyumba vya madarasa vya kutosha, na zile ambazo zina vyumba vya madarasa vya kutosha, viko kwenye hali mbaya na hii inatokana na shule hizi kujengwa muda mrefu. Uboreshaji huu wa vyumba vya madarasa utakwenda sambamba na uchongaji wa madawati ya kutosha, ili kuondokana na utegemezi kwa wahisani kuzipatia madawati shule zetu za Elimu ya Msingi, ambalo linapaswa kuwa jukumu la Serikali.

(iv) Uchimbaji wa matundu ya kutosha na ujenzi wa vyoo vya kisasa, hii itasaidia katika kulinda afya za watoto wetu, kwani hali ilivyo sasa shule nyingi za Elimu ya Msingi hazina vyoo vya kutosha, na nyingine hazina kabisa huduma hii.

(v) Utoaji wa chakula cha mchana mashuleni, ili kukabiliana na wimbi la utoro na usinziaji darasani kwa sababu ya njaa miongoni mwa watoto wa shule, Wizara irudishe huduma hii muhimu iliyokuwepo hapo zamani wakati wa Mwalimu Nyerere, na huduma hii igharimiwe na Halmashauri za Majiji, Miji na Wilaya, kwani mtoto mwenye njaa, au asiye na uhakika wa lishe, hawezi kuambulia chochote darasani kimasomo. Kama alivyosema mwanazuoni maarufu Plato, kuwa "akili yenye afya iko katika mwili wenye afya."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Sekondari hutolewa katika ngazi mbili tofauti na hadi tarehe 30 Juni, 2011, jumla ya shule zote za Sekondari nchini zilikuwa 4,266. Kati ya hizo, shule 3,397 ni za Serikali (3,308 za wananchi za kutwa, 89 ni shule kongwe za Serikali) na 869 ni shule zisizo za Serikali. Jumla ya wanafunzi katika Shule za Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali nchini ni 1,638,699. Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza – Kidato cha Nne ni 1,566,685 (wasichana 699,951).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita ni 72,014. Idadi hii ya wanafunzi waliopo shuleni ni kielelezo dhahiri kuwa kuna tatizo kubwa na la kimsingi, hasa kwenye mfumo wetu wa Elimu ya Sekondari na hasa ikizingatiwa kuwa kuna ufinyu wa nafasi za kujiunga na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo idadi ya wahitimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa mwaka ni 639,700 wakati nafasi za mafunzo ya ufundi na ufundi stadi ni 84,000 tu.

Kambi ya Upinzani tunahoji vijana wanaomaliza Kidato cha Nne wanakwenda wapi? Kwani ni wachache sana wanaopata fursa ya kwenda Kidato cha Tano, na ikizingatiwa kuwa tuna upungufu mkubwa sana wa Vyuo vya Ufundi hapa nchini. Tunataka maelezo ya kina kuhusiana na suala hili na mpango madhubuti wa kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010 na ya mwaka 2010 - 2015 ilitamka wazi kuwa Serikali itajenga Vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya nchini. Jambo la kushangaza ni kuwa ahadi hii mpaka leo bado haijatekelezwa na badala yake wananchi wanaendelea kupewa ahadi hewa.

Kwa mwaka huu wa fedha kwenye kitabu cha bajeti ya Serikali, kitabu cha Maendeleo *Volume IV* fungu 1003, kasma 4397, Serikali imetenga Sh. 100,000,000/= kwa ajili ya kuisaidia *VETA* kiwango ambacho ni kidogo zaidi mara tano ya fedha zilizotengwa mwaka jana.

Kambi ya Upinzani, inataka majibu kutoka Serikalini: Je, kutenga kiasi kidogo cha fedha za maendeleo kwa ajili ya *VETA* kitaweza kweli kujenga vyuo hivyo kila Wilaya kama ambavyo Serikali imekuwa ikiwaahidi wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha ufaulu katika mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2010, idadi kubwa ya wanafunzi waliopata Daraja la I – III ilishuka sana kwani kati ya watahiniwa 38,781 waliopata Daraja la I - III katika mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2010, wanafunzi 19,126 wanatoka Shule za Sekondari za Kutwa. Aidha, wanafunzi 3,697 wametoka katika Shule Kongwe za Sekondari za Serikali na 15,958 wanatoka katika Shule za Sekondari zisizo za Serikali. Takwimu zinaonyesha kushuka kwa ufaulu wa Kidato cha Nne kutoka asilimia 72.5 mwaka 2009 hadi 50.2 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za Serikali ni kuwa hadi Juni, 2011, jumla ya shule zote za sekondari nchini zilikuwa 4,266. Kati ya hizo, shule 3,397 ni za Serikali (3,308 kutwa, 89 ni shule kongwe za Serikali) na 869 ni shule zisizo za

Serikali.Takwimu hizi maana yake ni kuwa kiwango cha ufaulu kwenye Sekondari za Kata ni sawa na kusema kuwa shule hizi zimefaulisha kwa wastani wa kila shule ni wanafunzi sita tu waliopata Daraja la I - III, wakati shule kongwe zimefaulisha wastani wa wanafunzi 42 waliopata Daraja la I - III na shule za binafsi zimefaulisha wastani wa wanafunzi 18 kwa kila shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonyesha umuhimu wa kuwa na shule za Bweni kwani wanafunzi wanapata muda wa kutosha kusoma na pia kuwa na maeneo ya kusomea badala ya hali ilivyo kwa wanafunzi wa kutwa ambao wengi wao majumbani kwao wanakuwa na majukumu makubwa sana ya kazi mbalimbali. Kambi ya Upinzani, inahoji kwamba yapo wapi mafanikio ya Shule za Kata ambayo kila siku Serikali imekuwa ikiyasifia hapa Bbungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa mfumo wa Elimu ya Sekondari ufanyiwe mabadiliko kutoka miaka sita ya sasa kuwa miaka minne, kwa kuunganisha mitaala ya vidato vya tatu, nne, tano na sita kuwa mtaala mmoja wa Elimu ya Sekondari. Hii itasaidia sana kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata sifa za kujiunga na Eelimu ya Sekondari na, pamoja na badiliko hilo la msingi, Wizara itilie mkazo mambo yafuatayo:-

(i) Uimarishwaji wa ufundishaji wa lugha ya Kiingereza. Hili lifanywe kwa kuboresha mazingira mazuri ya kujifunzia lugha ya Kiingereza, ikiwemo kuzipatia shule walimu wenye ujuzi wa kufundisha lugha hiyo. Hii lengo lake ni kuhakikisha mwanafunzi anapoingia Kidato cha Pili anaifahamu vizuri lugha ya Kiingereza katika kuelewa, kuandika, kuongea na kujieleza. Kadhalika, Serikali ianzishe Taasisi ya kufundisha lugha za kigeni, ambapo lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina, Kijapani, Kiarabu, Kihindi na nyinginezo zitafundishwa kwa viwango vya kati na juu.

(ii) Uimarishwaji wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Pamoja na kutilia mkazo ufundishaji wa lugha za kigeni, Wizara iweke msisitizo wa pekee katika kuifahamu lugha ya Kiswahili sanifu. Wanafunzi Watanzania ni lazima waimudu lugha yao ya Taifa bila kujiona duni kwa kufanya hivyo, waweze kupambanua Kiswahili cha Mtaani na Kiswahili sanifu, wakati huo huo wakijiimarisha katika lugha za kigeni. Kambi ya Upinzani inaamini kwamba wanafunzi wetu wanaweza kumudu vizuri lugha nyingi kwa kiwango kile kile, bila kuathiri kwa namna yoyote uzalendo wao kwa Taifa letu.

(iii) Katika kufanikisha azma ya uimarishwaji wa ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati, Wizara izingatie maandalizi ya walimu wa masomo haya kwa uhakika, ujenzi wa maabara za masomo haya na kuziwekea vifaa na nyenzo zote za msingi za kufundishia masomo haya, pamoja na kemikali zinazohitajika.

(iv) Kuhusu somo la elimu viumbe, shule ziweke utaratibu wa kufuga wanyama wadogo wadogo na kutunza mimea ya aina mbali mbali kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fani hii ya masomo ya Sayansi, na hasa Hisabati, mbali na jitihada za makusudi za kuhamasisha wanafunzi wa kike kupenda kuchukua masomo haya, Wizara iboreshe ufundishaji wake uendane na misingi yake ambayo inazingatia sayansi ya mantiki inayojengeka hatua kwa hatua ili kuwavutia wasichana wengi, lakini pia kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wote kwa jumla ili kuondokana na tatizo la kukaririshwa ambalo hupelekea kutofanya vizuri katika somo la Hisabati.

(v) Uhimizwaji wa ufundishaji wa stadi za maisha na TEKNOHAMA, kwa kuhakikisha kuwa matumizi ya teknolojia ya kisasa yanaanza mapema kwa wanafunzi wetu, ili wafikie kwenye kiwango cha kimataifa cha elimu na ujuzi, mapema inavyowezekana.

(vi) Serikali ianzishe shule mpya za kitaifa za bweni za sekondari na shule hizi zichukue wanafunzi wote waliofanya vizuri zaidi katika mitihani yao ya mwisho ya Elimu ya Msingi kutoka sehemu zote za Tanzania. Katika kila Mkoa kujengwe angalau shule moja ya kitaifa, itakayochukua wanafunzi kutoka katika Mikoa mingine, kwa lengo la kujenga "utaifa" na "uzalendo" miongoni mwa wanafunzi.

(vii) Serikali irejeshe utaratibu wa usafiri wa "*warrant*" kwa wanafunzi. Ili kuondoa makali ya gharama za nauli kwa wazazi, ni wazi kuwa utaratibu huu ni aghali, lakini Kambi ya Upinzani inaamini kuua "utaifa" ni aghali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kubadilisha na kuboresha sekta ya Elimu ya Juu, ili iweze kuwa ya kisasa zaidi na kumwandaa msomi wa Tanzania kushiriki katika kutumia elimu yake kuiletea Tanzania maendeleo na vile vile kumpatia nyenzo za kisasa za kielimu zinazoendana na ulimwengu wa kisasa. Lengo hasa la dhamira hii ni kuhakikisha kuwa Elimu ya Juu inapatikana kwa kila Mtanzania anayeitamani, na mwenye uwezo kiakili wa kuipata elimu hiyo itakayokuwa ya kisasa, na mwenye nia ya dhati ya kutoa mchango wake kuliendeleza Taifa letu, ikiwa ni njia ya kuirudishia jamii ujuzi atakaoupata huko chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupanua wigo na kuboresha Elimu ya Juu nchini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuanzisha mfuko wa Elimu ya Juu, "*Uhuru Scholarship Fund*" kwa ajili ya kugharimia masomo katika Vyuo Vikuu vya Umma. Kuhusu wanafunzi wanaofaulu kwa viwango vya Daraja la I na la II wasichana, hawa hawatachukua mikopo, badala yake wanafunzi hawa watalipiwa gharama zote kadri wanavyofaulu na kupanda, kuelekea viwango vya juu vya taaluma zao, kwa muda wote watakaokuwa vyuoni.

(ii) Kuweka mfumo mpya wa kugharimia Elimu ya Juu kwa ajili ya wale watakaofaulu kwa viwango vya Daraja la III na la IV. Mfumo huu mpya uwekwe ili kuhakikisha kuwa gharama za Elimu ya Juu hazimkwazi mwanafunzi yeyote anayeitamani, na mwenye uwezo kiakili kuipata Elimu ya Chuo Kikuu. Katika kutimiza azma ya uwekaji wa mfumo huu, Serikali ihakikishe kuwa kila Mkoa unaanzisha Mfuko

wa Elimu ya Juu, taasisi za dini na watu binafsi wahamasishwe kwa lengo hilo, na kuwekewa utaratibu wa kisheria, ili waweze kuanzisha mifuko ya elimu inayogharimia mafunzo hayo na kamwe isiwe mikopo, kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kwa kuzingatia vigezo mahususi.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvunja Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kutokana na muundo wake, uendeshaji mbaya, na mfumo wake mbovu kisheria, uongozi wa Bodi hii ya Mikopo ya Elimu ya Juu umeshindwa kuifanya Elimu ya Juu ipatikane kwa kila mwanafunzi anayeistahili. Aidha, Bodi hii kutokana na uongozi usiofaa, imeshindwa kusimamia marejesho ya madeni kutoka kwa wanafunzi waliowahi kukopeshwa na hii inatokana na ukweli kuwa Bodi iliyopo ilitoa mikopo kwa wanafunzi 91,568 wakiwemo 23,141 wanaochukua masomo ya sayansi. Aidha, ilifanikiwa kukusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.9 kati ya shilingi bilioni 21 zilizo tayari kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, Serikali iazimie kuivunja Bodi hii, pamoja na kufanya uchunguzi huru wa fedha zote zilizotumika chini ya Bodi hii hadi hivi sasa na kujiridhisha kama waliopewa dhamana hii hawakutumia nafasi zao kujinufahisha binafsi, baada ya hili kukamilika ripoti iwekwe wazi kwa umma, na mapendekezo yake yafanyiwe kazi mara moja.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bodi ya sasa ya mikopo ya Elimu ya Juu kuvunjwa, Serikali iunde chombo kipya kitakachojulikana kama Mamlaka ya Taifa ya Kugharimia Elimu ya Juu *(Tanzania Higher Education Financing Authority – TAHEFA)*. Hiki ndicho kitakuwa chombo cha kifedha ambacho kitachukua majukumu yote ya Bodi ya mikopo ya sasa, chini ya muundo mpya na sheria mpya ambayo itaweka utaratibu mpya na wa kisasa wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu, ili kuhakikisha kwamba hakuna mwanafunzi anayeitamani na mwenye uwezo kiakili wa kuipata elimu ya juu, atakayeikosa.

(v) Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa fursa kwa Vyuo Vikuu kujiendesha kiutawala, na kitaaluma, bila kuingiliwa na Serikali. Hii iwe ni pamoja na uhuru wa kujichagulia viongozi wao, na chini ya utaratibu huu, jukumu la Wizara litakuwa ni kutunga sera za jumla za kuendeleza na kuilinda Elimu ya Juu, kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa rasilimaliwatu iliyo bora, ingawa uendeshaji wa Vyuo Vikuu vyenyewe utaachwa mikononi mwa mabaraza ya Vyuo hivyo. Hii itakuwa ni kulitekeleza azimio la kitaaluma ambalo tulilisaini mwaka 1990 *(Declaration on Academic Freedom).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kujenga uwanja wa demokrasia katika Serikali za Vyuo na vile vile kuweka mazingira ambayo yatawawezesha wasomi wetu kuanza kujifunza mbinu na utendaji wa kisiasa katika mazingira ya elimu ili waweze kujifunza kuishi pamoja, kupingana kwa hoja, na kujua jinsi ya kuvumiliana katika mazingira mbalimbali yenye tofauti za kiitikadi, imani, na mitizamo. Bila kuimarisha misingi ya demokrasia katika ngazi za Taasisi za Elimu, hatuwezi kujenga Taifa linalopenda na kuheshimu misingi ya demokrasia na utawala bora. Kupiga marufuku

ushiriki wa vijana wa elimu ya katika shughuli za kisiasa ni umbumbumbu wa elimu ya siasa kunakotokana na mazoea ya kukulia katika mfumo wa kiimla na hodhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Utafiti *(National Research Council)* ili kuchochea ubunifu na kuvishirikisha Vyuo Vikuu vyetu kwenye nyanja za kimataifa, Serikali iimarishe Tume ya Sayansi na Teknolojia ambayo itaratibu na kusimamia tafiti mbalimbali za kisayansi na teknolojia, na Sera na Sheria viboreshwe ili Tume iweze kufanya kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu mengine ya Tume hii yawe ni kuanzisha na kusimamia mashindano ya changamoto za kisayansi ili kuchochea utafiti na ubunifu. Kwa usimamizi wa Tume hii, zawadi nono ya fedha taslimu itakuwa ikitolewa kila mwaka, kwa Chuo Kikuu na wabunifu mbalimbali wa vitu ambavyo havijabuniwa sehemu nyingine duniani. Katika kuunda Baraza hili, baadhi ya Taasisi mbalimbali zilizopo nchini zitaunganishwa na kuwekwa chini yake, ingawa zitaendelea kuwa huru kiutendaji, huku zikishirikiana na kutegemeana katika kuendesha tafiti zake, na kusimamia matumizi ya matokeo ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuchochea kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia nchini, Serikali sasa ivipandishe hadhi vyuo viwili vilivyopo na kuwa na hadhi ya kutoa shahada, navyo ni kimoja kilichoko Mbeya na kingine kilichoko Tanga. Vyuo hivyo ni *Mbeya Institute of Science and Technology,* ambacho kitabadilishwa kuwa Mbeya *University of Science and Technology – MUST*, na Chuo cha Ufundi Tanga, ambacho kitabadilishwa kuwa Chuo Kishiriki cha *MUST*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Vyuo vya Kati vya Jamii pamoja na kuendelea kutoa elimu ya kiwango cha shahada ya Chuo Kikuu, utaratibu wa kuwa na Vyuo vya Kati vya Jamii – *'Community Colleges'*, ambavyo vitatoa elimu sawa na inayotolewa katika semista tatu za kwanza za Chuo Kikuu ni wa muhimu sana. Madhumuni ya kuanzisha vyuo hivi ni kuanza kutengeneza kundi la wasomi wa elimu ya kati, ambao kutokana na sababu mbalimbali, wasingeweza kupata elimu kamili ya Chuo Kikuu. Vyuo hivi vya jamii vitakuwa ni kiunganishi kati ya Elimu ya Sekondari na Elimu ya Chuo Kikuu na vitakuwa na uwezo wa kutoa Shahada Shiriki. Mhitimu wa vyuo hivyo akitaka baadaye anaweza kuendelea na Elimu ya Chuo Kikuu katika taaluma yake, kwa kuendeleza pale alipoachia na siyo kudahiliwa na kuanza masomo kama mwanafunzi wa mwaka wa kwanza. Ili kufanikisha azma hii, baadhi ya vyuo vya jamii vilivyopo sasa, vipandishwe ngazi na kubadilishwa kuwa Vyuo vya Kati vya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kuwa katika bajeti yake madeni yote ya wanataaluma, ya posho ya pango kwa wanaostahili yanalipwa, na mpango wa kuboresha mafao ya wahadhiri ya uzeeni unatekelezwa kikamilifu. Lengo la azma hii ni kuwaondolea hofu ya maisha yao ya kila siku wanataaluma wetu ili waweze kujikita kweli katika kutoa elimu, kufanya utafiti kwa utulivu, na kutoa ushauri wa kitaalam ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kufaidika na utaalam na uzoefu wa maprofesa wetu hapa nchini, katika kuwanoa vijana wetu wa Vyuo Vikuu, tunashauri kuwa Serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha majadiliano na wanataaluma, pamoja na mabaraza ya Vyuo na Seneti zao, kuangalia uwezekano wa kuongeza umri wa maprofesa kustaafu, kutoka miaka 60 ya sasa hadi 70, maadamu Chuo husika kimejiridhisha kuwa Profesa husika bado utaalam wake anautumia kikamilifu na unahitajika kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Serikali ilitekeleza utaratibu wa kubadilishana wanafunzi kati ya Tanzania na Msumbiji, na Tanzania na Uganda, ambapo wanafunzi Watanzania 68 wanasoma Uganda na 29 wanasoma Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huo huo wa fedha, Serikali iliwawezesha wanafunzi watano raia wa China kusomea kozi ya muda mfupi ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya utaratibu wa *scolarship* zinazotolewa na Serikali ya Tanzania kwa Serikali ya China katika kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huo huo wa fedha Serikali ilipokea na kuratibu nafasi 132 kutoka Uingereza 12, China 72, Korea ya Kusini wawili, India 20, New-Zealand wawili, Urusi 15, Misri watano na Cuba wanne.

Kambi ya Upinzani inataka kujua ni vigezo/utaratibu gani huwa unatumiwa na Wizara katika kuwapatia wanafunzi nafasi za kwenda kusoma nje ya nchi. Hii inatokana na ukweli kuwa yamekuwapo malalamiko mengi kutoka kwa wanafunzi mbalimbali kuwa kuna upendeleo wa wazi katika kushughulikia nafasi za wanafunzi kwenda nje ya nchi. Ni chombo gani kinahusika katika kuteua wanafunzi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyefahamu kwamba sekondari zetu hususan za Kata zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu ambao wamehitimu katika ngazi ya stashahada na shahada. Tatizo hili linawafanya walimu wachache waliopo kufanya kazi katika mazingira magumu sana ikiwepo kufundisha masomo ambayo hawakusomea na kufundisha idadi kubwa ya wanafunzi bila kufuatilia *"performance"* ya mwanafunzi mmoja mmoja. Kambi rasmi ya upinzani inaona umefika sasa wakati wa Serikali kuingia mkataba wa lazima wa miaka mitano kwa wanafunzi wanaosomea kozi ya ualimu na wanaopata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo, kwa kuwapangia wanafunzi wanaomaliza shahada zao kwenda kufundisha katika Shule za Serikali.

Mkataba huu uwe unasainiwa pindi mwanafunzi anapodahiliwa na masharti yawekewe kwamba pindi mwanafunzi anapohitimu ni lazima afundishe katika Sekondari za Serikali na atakapoacha kwenda hufundisha huko basi sheria imbane arudishe mkopo aliopewa na Serikali mara moja. Kama hafanyi hivyo, sheria ichukue mkondo wake. Nachelea kusema kwamba, pendekezo hili lisichanganywe na ile sheria ya utumishi ya kufanya kazi kwa miaka miwili kwa mtumishi yeyote kabla ya kuthibitishwa, yaani "*probation period"* maana hii inahusu kada zote za ajira na siyo mkataba wa makusudi kama nilivyouelezea hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupunguza uhaba wa walimu kwa kiasi kikubwa, njia hii itasaidia kuwabana wakopaji wote kuweza kurudisha mkopo kwa wakati na kuwapa nafasi na wahitaji wengine kunufaika na mkopo huu wa Elimu ya Juu. Sambamba na hili, Serikali iweke mazingira mazuri ya kufundishia kwa walimu ikiwepo kuwajengea nyumba bora za kuishi na kuboresha maslahi yao ili wasipate tamaa ya kumezwa na soko la ajira na wao kukimbilia kufundisha shule za binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa Vyuo Vikuu hapa nchini wamekuwa wakiandamana kutokana na sababu mbalimbali na hasa kubwa ni kutokana na Serikali kutowatendea haki na hili linaendana na ama kucheleweshewa fedha zao za mkopo na wengine kunyimwa fedha kwa ajili ya kwenda kufanya mafunzo kwa vitendo kama sehemu ya masomo yao. Pindi wanafunzi hawa wanapogoma ama kuandamana wamekuwa wakipigwa na wengine kuumizwa na Jeshi la Polisi na baadhi yao kuishia kufukuzwa vyuoni na au kusimamishwa masomo kama ambavyo imetokea katika Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam, Muhimbili, Chuo cha Ardhi na vinginevyo vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya maandamano hapa nchini inaonyesha kuwa yalianza tangu kipindi kirefu kilichopita cha uongozi wa awamu ya kwanza na hata viongozi mbalimbali wa wanafunzi wakiwemo wengine ambao ni Mawaziri humu Bungeni, walishiriki kikamilifu maandamano na migomo hiyo na hata kufikia wengine kuadhibiwa na Hayati Baba wa Taifa wakati wa urais wake. Hivyo, sio sahihi hata kidogo kufikiri kuwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu ambao wanagoma na kuandamana hapa nchini basi kuna msukumo wa kisiasa kama ambavyo wanataka Taifa liamini kwani lilikuwepo tangu wakati wa chama kimoja. Suluhisho pekee ni kuondoa matatizo kwenye vyuo vyetu ili wanafunzi waweze kusoma bila matatizo kama ambavyo hali ipo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya mwaka 2009 iliyotangazwa kwenye gazeti la Serikali Namba 178 la tarehe 12/06/2009 inayojulikana kama Kanuni ya Vyama vya Wanafunzi Vyuo Vikuu *(Universities students organization regulations, 2009*) pamoja na mambo mengine kanuni hizo zimeelezea kwenye kifungu cha 14 juu ya haki za wanafunzi kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kukusanyika *(assemble);*
(b) Kuandamana *(demonstrate);* na
(c) Kutoa maoni yao *(express their opinions).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali yenyewe kutoa haki hizi kwa wanafunzi, lakini la kusikitisha ni kuwa pindi wanafunzi hawa wanapokuwa wanaandamana kama njia ya kuweza kutoa maoni yao na kama ambavyo kanuni zimewapa haki hizo, bado Serikali kwa kutumia Jeshi la Polisi wamekuwa wakiwapiga vijana hawa na hata wengine kuumizwa vibaya kama ilivyotokea hapa Dodoma kitendo kilichopelekea mwanafunzi mmoja anayeitwa Malumbo Ngata kuvunjwa mguu wa kulia

na kulazwa *Dodoma General Hospital* (*Ward 11* kitanda Na.3) kutokana na kipigo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Polisi kuwapiga wanafunzi, sasa imekwenda mpaka kufikia ngazi za Shule za Sekondari kwani ni hivi majuzi tu Polisi waliwafyatulia risasi za moto wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mbezi iliyopo jijini Dar es Salaam na kupelekea wanafunzi wengi kuumia vibaya na kulazwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, wakati walipokuwa wakidai haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ni ya hatari kwa vijana wetu kwani kama imefikia mahali pa kuwafyatulia risasi za moto wanafunzi ambao hawana silaha yoyote na Serikali imeendelea kukaa kimya bila kuchukua hatua zozote dhidi ya wanaofanya vitendo hivyo ni kitu ambacho hakikubaliki. Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali itoe maelezo kuhusiana na mambo yafuatayo;-

(i) Ni hatua gani Serikali imechukua mpaka sasa dhidi ya wale wote ambao wanasababisha majeruhi kwa kuwapiga wanafunzi kinyume cha sheria kama ambavyo kanuni tajwa hapo juu zinawapa haki ya kuandamana?

(ii) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wanafunzi ambao wamesimamishwa masomo kutokana na kutumia haki yao ya kisheria ya kuandamana na ni lini watarejeshwa vyuoni kwa ajili ya kuendelea na masomo?

(iii) Je, ni kesi ngapi ambazo mpaka sasa zinawakabili wanafunzi wa Vyuo na wa Sekondari kwa kuandamana na zipo Mahakama gani?

(iv) Ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya wale wote ambao wanasababisha kutokea kwa migomo hii vyuoni? Kwani mara nyingi watawala vyuoni wamekuwa wakihusishwa kutokana na kushindwa kutatua matatizo mbalimbali ndani ya vyuo husika.

(v) Je, Ofisi ya Waziri Mkuu imechukua hatua gani dhidi ya utawala wa Chuo Kikuu cha Dodoma baada ya Waziri Mkuu kuunda Tume kuchunguza malalamiko ya wanafunzi dhidi ya Mkuu wa Utawala wa Chuo hicho na vingine vingi nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa ni haki ya kikatiba ya wanafunzi kuandamana na kutoa maoni yao na kamwe hatutakaa kimya pindi haki za wanafunzi zinapokuwa zinavunjwa na vyombo vya Serikali na vijana wetu kuendelea kuumizwa? Kambi ya Upinzani tutalisimamia tamko la ulimwengu la uhuru wa kitaaluma, *The Declaration on Academic Freedom and Social Responsibility of Academics*, ambalo Tanzania tulisaini mnamo tarehe 19 Aprili, 1990, kwani tunaamini kuwa Taifa haliwezi kuendelea kamwe kama wanataaluma wake wananyanyaswa na kukosa uhuru wa kutoa maoni yao kwa uwazi na bila kipingamizi chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kuwa Serikali iliunda Tume ya Prof. Maboko kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha migogoro na migomo kwenye Vyuo

mbalimbali hapa nchini na Tume hizi ni mwendelezo wa Tume nyingi ambazo ziliwahi kuundwa kwa miaka nenda rudi na kila mara Tume hizi huja na majibu yanayoshabihiana kuhusiana na vyanzo vya migogoro na hatimaye migomo na maandamano kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini. Kambi ya Upinzani tunataka kujua ni lini mapendekezo ya Tume ya Prof. Maboko yatawekwa hadharani kuhusiana na vyanzo vya migogoro hii na migomo kwenye Vyuo Vikuu ili matatizo hayo yaweze kutafutiwa ufumbuzi na hatimaye visingizio bandia vya vyanzo vya migomo na maandamano Vyuo Vikuu viweze kuachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limekuwa likishuhudia kushuka kwa viwango vya ufaulu wa mitihani mwaka hadi mwaka katika ngazi za Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Pamoja na mambo mengine, mtazamo wa Kambi ya Upinzani kuhusu hili ni kwamba hali hii inasababishwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa vifaa, walimu, vitabu vya kiada na ziada, maabara, motisha kwa waalimu, kiwango kidogo cha watoto kupenda kusoma, na kutokuwepo kwa utamaduni wa kusoma vitabu miongoni mwa Watanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa kwa Taifa letu. Changamoto ya kujenga tabia za watoto wetu kupenda kusoma, na kwa njia hiyo hatimaye kukuza utamaduni huo miongoni wa Watanzania, hatuna budi kuwafanya watoto wetu wapende kusoma na kuwafundisha kupenda vitabu tangu wanapokuwa wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko faida nyingi za kumfanya mtoto apende vitabu. Mbali na kumjengea tabia ya kupenda elimu, kwa watoto walio wengi, kusoma kwa kujifurahisha kunaweza pia kuwaepusha na tabia nyingine ambazo huharibu watoto, kama vile kucheza michezo isiyo na maana kwenye kompyuta, ama kuangalia programu za hovyo kwenye luninga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa, tunapaswa kuandaa mkakati wa kuhamasisha wazazi kuwafundisha watoto wao kupenda vitabu tangu wakiwa wadogo. Ili mkakati huu uweze kufanikiwa, lazima ianzishwe kampeni maalum ya kitaifa katika kumshirikisha kila mzazi, kwani ni sehemu muhimu sana ya malezi ya mtoto. Kila mzazi hana budi kufahamu ni vitu gani ambavyo mtoto wake anavipenda, na vipi anavichukia, ili kubaini aina ya vitabu ambavyo vitamfurahisha, na kwa njia hiyo, kumvuta na kumwingiza kwenye ulimwengu wa kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wetu tuna mazoea ya kuwafanyia sherehe watoto wetu, kuadhimisha kumbukumbu za siku zao za kuzaliwa, na huwa tunawanunulia zawadi. Mzazi akishabaini kitabu anachokifurahia mtoto wake kukisoma, zawadi ya kitabu kama hicho kwenye sherehe kama hiyo ni ya maana zaidi ya zawadi nyingine zote tulizozoea kuwapa watoto wetu. Mkakati huu ni changamoto kwetu ya kututaka tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka, Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania *(BAMVITA)* huwa linaandaa na kuendesha tamasha la maonyesho ya vitabu jijini Dar es Salaam, na kila Mkoa, nchi nzima. Ni budi sasa kwa Wizara na Serikali kuanzisha

mkakati wa kuhamasisha Watanzania wote kutembelea maonyesho haya mwaka huu, tukifuatana na watoto wetu, ili kuwapa fursa ya kuona vitabu mbali mbali, kuchagua wanavyopendezwa navyo na tuwanunulie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkakati huu uwe endelevu, Serikali inapaswa kuhamasisha kuundwa kwa vikundi vya watoto, na kuanzisha vyama vya watoto vya kusoma vijulikanavyo kama Mahema ya Watoto ya Kusoma *(Childrens' Reading Tents).* Vikundi hivi vitakavyoanzishwa kwenye ngazi ya Kata, vitasimamiwa na Serikali za Mitaa, na kuendeshwa na Walimu wastaafu, sambamba na shule ngazi ya Elimu ya Awali, ambazo nimeshazizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika azma hii ya kujenga tabia na kukuza utamaduni wa kupenda kusoma miongoni mwa Watanzania, mbali na kuimarisha Maktaba Kuu ya Taifa na Maktaba za Mikoa, tuanzishe Maktaba Tembezi *(Mobile Libraries)*, kuhudumia wananchi walioko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na adha kubwa inayowakumba wanafunzi na hasa wanaosoma maeneo ya Miji na Majiji imekuwa ikitishia uhai wa kukua kwa kiwango cha elimu nchini mwetu. Hali hii inatokana na mradi wa mabasi ya wanafunzi uliokuwa ukitoa huduma hii ya usafiri kwa wanafunzi kuhujumiwa na kuangamizwa. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali itoe majibu kuhusu mradi huu na ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa kwa wale waliohusika na ambao mpaka sasa wengine ni viongozi, tunataka wahusika hawa wachukuliwe hatua kwani wameshiriki kwa kiasi kikubwa kuongeza mateso kwa wanafunzi hawa.

Tunaishauri Serikali kuwa kutokana na mradi wa mabasi yaendayo kasi *DSM* ni muda muafaka sasa wa kulifanya shirika la *UDA* kuwa ni kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi ili kuweza kupunguza adha wanayokumbana nayo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Utawala na Raslimali watu ilipokea madai ya watumishi mbalimbali yaliyowasilishwa Wizarani. Hivi sasa, madai ya watumishi 3,050 yanachambuliwa na kuhakikiwa ili kuainisha yale yanayostahili kulipwa, ambapo inatarajiwa kuwa ifikapo mwisho wa Juni, 2011 madeni hayo yatakuwa yamehakikiwa yote na kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu, ni hatua gani imefikiwa mpaka sasa kuhusiana na uhakiki wa madeni ya watumishi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Julai, 2010 hadi Aprili, 2011 madeni yenye thamani ya Sh. 777,918,643/= yaliyotokana na malimbikizo ya mishahara yaliwasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini malimbikizo ya waalimu hawa yatalipwa na hasa ikizingatiwa kuwa Waziri wa Fedha kwenye hotuba yake alisema kuwa mwaka huu wa fedha waalimu hawatalipwa mafao yao. Hivi waalimu hawa ni kwanini wao tu ndio wanyimwe haki hiyo ya kulipwa haki zao? Au mpaka wagome ndio Serikali itoe vitisho na iwalipe waalimu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na waalimu wetu kuendelea kuumia kutokana na tatizo la kiwango kidogo cha mishahara na ukizingatia kuwa wanakuwa na wakati mgumu sana kuweza kukopeshwa na Benki mbalimbali za kibiashara hapa nchini, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali sasa kuweza kuweka utaratibu maalum wa kuhakikisha kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo waalimu ni wanachama wake waweke utaratibu maalum wa kuwakopesha waalimu kutokana na makato yao kwenye mifuko hiyo ili waweze kujenga nyumba na kuweza kujikwamua kwenye hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninawashukuru wote mliotoa hotuba zenu, kuanzia Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzania. Sasa ni wakati wa michango kuchangia hoja hii. Naomba niwataje ambao wataanza. Tutaanza na Mheshimiwa Pindi H. Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Anthony Mbassa na baadaye Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Chiku Abwao ajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Anthony Mbassa.

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia nikiwa mchangiaji wa kwanza. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kunipa nguvu na niweze kushukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi ambao nawawakilisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba nami ni Mjumbe katika Kamati hii ya huduma za Jamii. Nitaomba nielekeze mchango wangu katika mambo makubwa matatu. Nitaongelea suala zima la Elimu ya Watu Wazima na wale ambao wapo katika mfumo usio rasmi, nitaongelea suala zima la madai ya Walimu na vilevile suala zima la Elimu ya Ufundi hususan Vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa michango yote iliyotolewa na hotuba zilizotangulia na hususan kwa namna ya pekee hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo imeonyesha uhai na nini kinahitajika kifanyiwe kazi katika Wizara hii. Tukiangalia idadi ya wananchi wetu tulionao leo hii, takwimu zinaonyesha kwamba asilimia 31 ya watu ambao tulitegemea wajue kusoma na kuandika hawajui kusoma wala kuandika, kwa maana ya Elimu ya Watu wazima, kwa maana ya kundi la watu maalum ambao wamekosa elimu, na watu hawa ukiangalia mazingira waliyonayo hususan Walimu wanaowafundisha watu hawa yamekuwa yakipuuzwa na yamekuwa hayapewi stahili inayokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia huko vijijini, ndiko watu hawa waliko wengi na waliopo mijini naweza kusema ni wachache. Walimu wanaojitolea kuwafundisha watu hawa, ina maana wana shughuli nyingi za kuendesha maisha yao ya kila siku. Lakini ukiangalia vilevile mazingira waliyonayo kwa maana ya vituo na vifaa vya kufundishia pamoja na stahili zao kwa kweli ni kitu ambacho kimeachwa nyuma kwa muda mrefu sana na hakipewi umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tunajiuliza, tunataka tuwe na Taifa la watu wanaojua kusoma na kuandika, huyu adui ujinga tutamweka pembeni kwa mikakati hii? Leo hii inafikia mahali tunasema kwamba suala zima la wananchi kuhusishwa katika miradi mbalimbali linakwama kwa sababu ya watu kutokujengewa uelewa, lakini laiti watu hawa tungeweka mikakati thabiti wakafundishika, kukawa na vifaa vya kufundishia Walimu wakapata motisha, japo ni ujira mdogo tu ambao wengine wamediriki kuniandikia *message* wanasema huu ujira hauna tofauti na ujira wa mkoloni ulivyokuwa, lakini ukiangalia katika maeneo mengi na hususan katika Jimbo langu, vituo hivi kwa kweli havifuatiliwi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifikia mahali wakati mmoja nikaomba Afisa Elimu anayehusika, basi anipe takwimu ya vituo hivi, wapi wanakofundishiwa hawa watu wazima? Hivi vituo vya MEMKWA vinaendeshwaje? Lakini mpaka leo hii takwimu hizo sikuweza kupata. Sasa hapa najiuliza, tunapotaka kufuta wimbi hili la watu wasiojua kusoma na kuandika tutafanikishaje kama hatuwezi kuweka mikakati ya dhati ya kuweza kusaidia watu hawa ambao wanafundisha wananchi wetu huko vijijini? Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. Waheshimiwa Wabunge wote hapa mtakuwa mashahidi na hususan katika kipindi cha kupiga kura, utakuta msururu mkubwa sana, watu wamesimama kwenye vituo hawajui kusoma na kuandika na matokeo yake hawa watu wanapoteza haki yao ya msingi. Mtu anakwenda kupiga kura anamwambia, basi mimi nataka nimchague Fulani, anafika mtu pale anamwandikia ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tafadhali, Wizara inayohusika iliangalie kundi hili, tuwape matosha hawa Walimu wanaotufundishia watu wetu vijijini, tuwajengee mazingira mazuri ili kusudi waweze kuipenda kazi yao na tuweze kupunguza adui ujinga. Ukiangalia ni wachache sana ambao wanajitolea kufanya kazi hii. Lakini basi kwa wale ambao wamejitolea, ninaomba tafadhali vituo hivi viangaliwe upya, vipewe vifaa vya kufundishia, vipewe Walimu na Walimu hawa wapate mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea uwezo na kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako hili limekuwa likijadili mara kwa mara kuhusu matokeo mabaya ya wanafunzi wetu, lakini katika changamoto tulizoziona ni pamoja na suala zima la Walimu. Hapa naomba niongelee Walimu kwa ujumla wao. Walimu hawa ni kundi kubwa ambalo sasa hivi limeachwa nyuma. Napenda kumpongeza Rais wa Chama cha Walimu -Bwana Musiba kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatetea Walimu. Ni harakati nyingi ameziendesha, lakini ukiangalia, Walimu hawa wameachwa. Leo hii katika Halmashauri zetu nyingi kumekuwa na Umangimeza, Walimu hawa hawaangaliwi stahili zao wala maisha yao yanavyokwenda. Leo hii Mwalimu anatoka kwenda kufundisha kilomita nane, aidha aanze kugombania usafiri wa baiskeli na mwanafunzi au usafiri wa pikipiki. Lakini anaendaje na kurudije? Huyu mwajiri haliangalii hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata walioko kule vijijini, ukiangalia anafanyaje kazi, anaishi vipi, bado imekuwa ni tatizo kubwa sana. Tunahimiza kujenga nyumba za Walimu, lakini nyumba hizi hazina umeme, hazina maji, huyu Mwalimu atapataje muda

wa kuandaa masomo kwa ajili ya wanafunzi? Huyu Mwalimu atapataje muda wa kutafuta maji kama haitafikia hatua ya kuanza kuwatuma hawa wanafunzi wakamchotee maji? Ni kitu ambacho sisi hatukitaki kwa sababu mwanafunzi amekwenda pale kusoma, siyo kwenda kuchota maji. Lakini hayo ndiyo mazingira ya Walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna Walimu ambao wanadai posho na mishahara yao. Mimi hapa katika Jimbo langu nina orodha na kuna Walimu 85 tangu mwaka 2008 mpaka leo hii wanadai mapunjo ya mishahara yao, hawajapewa hata senti. Sasa niambie kundi hili la Walimu 85 na bado kuna kundi lingine ambalo bado linadai mishahara ya karibu miezi tisa hawajapewa. Niambie Mwalimu huyu ataingia darasani akiwa na morali gani wa kufundisha? Leo hii ataweza kuandaa kipi kizuri amfundishe mwanafunzi aweze kufauli vizuri? Tofauti na kufikiria, ataweza kudhibiti nakisi hii ya mapato ndani ya familia kwa kuanzisha Kituo cha kufundisha *tuition?* Matokeo yake ataandaa kile kidogo kwa kufundishia wanafunzi na muda wake mwingi atautenga kwa ajili ya kufundisha *tuition*. Hapa ndipo mnapompa mtego mzazi, ambaye hana pesa kwa ajili ya kumpeleka mwanafunzi au mtoto wake *tuition*, basi mtoto huyo atapata shida. Naomba kabisa Wizara hii pamoja na suala zima la ugatuaji, waangalie stahiki na stahili za hawa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Walimu nina imani kubwa wakipewa mishahara yao, mapunjo yao yakalipwa, watafanya kazi vizuri na suala la ufaulu litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni nafasi za Walimu wanazozipata kwenda kujiendeleza. Leo hii kumekuwa na Maafisa huko ambao Mwalimu akionekana anataka kujiendeleza, kwao inakuwa ni mwiba mkali, hawawaruhusu na matokeo yake Mwalimu ukiangalia umbali anakotoka kwenda Ofisi za Elimu kushughulikia ruhusa za kwenda chuoni inakuwa ni msalaba kwake. Leo hii katika Jimbo langu la Biharamulo Magharibi, Mwalimu anayetoka Mkukwa, anayetoka Kanyoni kuja pale Wilayani ni siku nzima imekwenda, ategemee akamilishe shughuli zake na arudi. Matokeo yake inapofikia mahali huyu mtu kwa sababu anakwenda ofisini na ofisi zetu nyingi hazina mkataba kwa mteja, matokeo yake amsubiri Afisa akishamaliza shughuli zake ndiyo amhudumie na Afisa kama hakujipanga vizuri, basi barua yake itaishia kuwekwa kapuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachouliza, tunahitaji tuwe na Walimu ambao hawataki kujiendeleza au Walimu ambao wamejiendeleza kwa ajili ya ufanisi wa shughuli zetu hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hawa Walimu wasaidiwe, hakuna Mwajiri anayependa abaki na watumishi ambao hawakujiendeleza. Leo hii Walimu waliothubutu kufanya hivyo, wengi sana wana kesi. Aidha, wanaambiwa kwamba wameondoka vituoni bila kuaga na ukiangalia, Mwalimu huyu amefuata *process* zote na *process* hizo imefikia mahali huyu Mwalimu anapoondoka tu Afisa anakwenda kule shuleni kumbana Mwalimu Mkuu. Huyu mtu ameondoka lini? Imekuwaje? Matokeo yake anaandikiwa barua za utoro. Wengi wamefungiwa mishahara, wengi sana hawalipiwi. Kuna ubaguzi gani wachache walipiwe na wengine wasilipiwe? Nafikiri motisha kwa hawa Walimu ni

kumweleza, umepata nafasi, yawezekana leo hii fungu hatunalo la kukusomesha, basi usubiri mwakani upate stahili zako uende chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inashangaza mtu mmoja anapata ufadhili wa kwenda kusoma na mwingine hapati. Mbaya zaidi, anayethubutu kwenda, basi huku nyuma inakuwa ni fujo tu. Sasa, tunapomfungia mwalimu mshahara, tunategemea tumemkomoa yeye au tumekomoa na familia nzima? Naomba, tafadhali Wizara iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, wamesema kwamba wanataka kuanzisha Vyuo vya Fedha katika kila Wilaya. Naomba kabisa kwa moyo wa dhati, suala hili lifanyike na lisiwe tu hadithi za kuandika katika vitabu vyetu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Wilaya nyingi hasa hizi za pembezoni kuna shida kubwa sana, hakuna Vyuo vya Ufundi. Vijana wetu wanamaliza shule, wanabaki tu vijiweni. Lakini vyuo hivi vikianzishwa, nina imani vitasaidia kabisa kuanza kuwajengea vijana uwezo na pili kuleta ajira kwa hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Jimboni kwangu kuna mzee mmoja ndio amejitolea tu, ana Chuo anakiita Chuo cha *VETA*. Lakini, ukiangalia Serikali haijasaidia chochote kile. Hawa watoto wanaishi katika mazingira magumu, anavyowafundisha ni yeye mwenyewe anajua, hana walimu wa kutosha, hana nini. Sasa jamani, Serikali naomba itambue hata michango ya watu binafsi, watu kama hawa wasaidiwe waongezewe nguvu kwa sababu wanasaidia kunusuru maisha ya vijana wetu, vinginevyo, tutaweka vijana wetu katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa kuokoa muda wetu. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda niwashukuru Wanambeya, naona mambo yanakwenda *against all odds*. Hongera sana kwa Wanaiziwa kwa kuendelea na mchakato wa ufyatuaji matofari kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Daktari. Hongera sana kwa Wanansalaga kwa kukamilisha uchimbaji wa Bwawa la Samaki. Mchakato wa *Airport* na Barabara vinaendelea, wananchi ni mashahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nichukue nafasi hii kuwashangaa baadhi ya Waheshimiwa humu ndani. Kila siku ndani ya hili jengo wanatuchana CHADEMA kuhusiana na maandamano yetu, lakini, kinyume na yote nashangaa juzi wamekwenda Mbeya na wamefanya maandamano…

**MWENYEKITI:** Naomba ukae!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Na mbaya zaidi wamekwenda Mbeya wakiambatana na Waasisi wa CCJ. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba ukae! Kwa mujibu wa Kanuni ya 64, tunaambiwa: "Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko katika mjadala". Naomba u-*focus* kwenye Sekta hii ya Elimu. Maandamano ya Mbeya siyo katika mjadala wa leo. Ahsante sana. Mheshimiwa endelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na Waheshimiwa kutokufanikiwa, lakini napenda niyatumie maandamano ya Mbeya kama *justification* kwamba maandamano ni poa na yanaruhusiwa. Kwa hiyo, wanafunzi wa vyuo mnaweza mkaendelea kuandamana pale ambapo mnadai mambo yenu ya msingi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wakiandamana watafukuzwa!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba msizungumze bila ridhaa ya Kiti. Anayezungumza chini chini asifanye hivyo. Mwongee kupitia Kiti. Mheshimiwa Mbilinyi naomba uendelee.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na shutuma nyingi dhidi ya CHADEMA kwamba tunapeleka siasa vyuoni. Mimi naomba niseme hivi, wote tunapeleka siasa vyuoni kwa sababu tunaona kila siku Katibu Mwenezi wa CCM, Nape yuko UDOM. Afadhali hata angekuwa Mbunge, eehe, yeye ni kiongozi wa Chama wa Uenezi, anakwenda pale kufanya uenezi na hakuna kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu *the other day* ndani ya nyumba yako Tukufu, Mheshimiwa Spika alikuwa anatoa tangazo kwamba kuna mahafali ya wanachuo ambao ni wana-CCM akiwaalika Wabunge ambao ni wana-CCM kuhudhuria yale mahafali. Hiyo kama siyo siasa vyuoni ni kitu gani? Kwa hiyo, siasa vyuoni itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotakiwa hapa ni kuongelea mambo ya msingi kwamba nini kifanyike katika kuendeleza elimu yetu, siyo vinginevyo. Watu wanakaa humu, wanaongea hili, wanaongea lile, lakini shule zetu tunajua kabisa hazina maabara pamoja na kwamba tunajisifia. Tunatengeneza wanasayansi wa kwenye makaratasi. Leo hii wanafunzi wengi wa Tanzania wanasoma ili kuwa Watangazaji wa Redio FM na siyo watalaam. Kwa hiyo, tunatakiwa tuangalie maeneo hayo kwa kuboresha elimu yetu. Boresha kila mahali, boresha *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* inatakiwa waboreshe *programme* zao. Waache kufundisha mambo ya *panel bitting*, kujaza *put* kwenye gari. Siku hizi magari yote ni *computerized*, sayansi imesogea, shavu la gari likigongwa, watu wanatoa wanaweka lingine, kama siyo jipya wanaweka *used*. Kwa hiyo, *VETA* inatakiwa wajikite katika

elimu ya utalaam zaidi inayoendana na sayansi ya leo, elimu inayoendana na *computer* katika kuleta *programme* zao kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sielewi kabisa hii Bodi inafanya nini kwa sababu kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri, Bodi ya Mikopo imeelezewa majukumu yake kana kwamba haina tatizo lolote. Utadhani kwamba kila kitu kinakwenda sawa. Hakuna hata mstari mmoja ulioelezewa matatizo. *The other day* tuliuliza hapa kwamba Serikali ina mpango gani na Bodi? Tukaambiwa kwamba Rais ameunda Tume, lakini matokeo ya ile Tume tulitegemea hata tuone mistari miwili yameandikwa katika hotuba ya Waziri ili kuwapa matumaini wanafunzi kwamba sasa hivi kuendelea mbele, suala la mikopo yao litakuwa halina tatizo. Ndiyo maana nasema kwamba, mimi natarajia kwamba matatizo kwenye mikopo yataendelea kuwepo, na kwa maana hiyo, basi wanafunzi inabidi waendelee kuandamana mpaka kila kitu kitakapokaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ada. Katika vitu ambavyo vimenikwaza au nimeona kwamba ni tatizo kwa wananchi wangu wa Mbeya Mjini ni pamoja na ada. Watoto hawana ada, wanafunzi hawana ada. Kama ningeweza kulipia ada kila mwanafunzi, basi nilitakiwa nitumie zaidi ya shilingi milioni 150/200 kuwalipia wanafunzi wale. Sasa hii hela itatoka wapi kwa Mbunge? Hii hela, Mbunge atatoa wapi? Tunakalia tu kusema elimu bure, haiwezekani! Rudisheni elimu bure! Ninyi mmesoma kwa hela za *GAPEX (General Agricultural Produce Export)* Kampuni ya Kuuza Mazao Nje; korosho, karanga, kahawa, choroko na vitu kama hivyo, na Mwalimu Nyerere akawapeleka madarasani, mkasoma mpaka Vyuo Vikuu na mkagoma na mkamaliza. Lakini leo hii ni Mawaziri, halafu mnakaa hapa mnazungumzia mpaka kuchimba *Uranium*, halafu mnasema eti elimu bure haiwezekani. Hicho kitu hakipo. Somesheni Taifa, somesheni, watoto wasome na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Bodi ya Mikopo ni *disaster*. Nataka kusikia maelezo kwamba nini kinafanyika, kwamba ile Tume ya Rais imekuja na matunda gani katika suala zima la kurekebisha Bodi ya Mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sijaona mnazungumzia madeni. Kuna madeni mengi sana mnayo, kila kona watu wanadai. Walimu wanadai. Kwangu Mbeya walimu zaidi ya 300 wanadai takribani shilingi milioni 400 toka mwaka 2007, lakini mpaka leo hii ndiyo hadithi. Toka wakati wa kampeni nazungumzia hili suala la walimu wangu Mbeya, mpaka leo hii nazungumzia suala la walimu wangu Mbeya. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mlugo, unatakiwa uwajibu watu wako wa Mbeya kwamba hizi hela watalipwa lini ili tuanze upya tuendelee na mambo mengine?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachia madai ya walimu, tuje kwenye madeni ya wazabuni. Wazabuni wanaleta chakula, wanaleta huduma kwenye shule, kwa nini hamwalipi? Wanalalamika! Mfano shule ya Iyumba Mbeya, sina raha mimi Mbunge pale kwa ajili ya kupokea *message* za Wazabuni wa Iyunga Mbeya. Wanataka hela zao! Wengine wanadai shilingi milioni 500, wengine wadai shilingi milioni 200. Maelezo ya *RAS* Mkoa wa Mbeya yanatofautiana na maelezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI. Maelezo ya *RAS* yanasema suala liko kwa *CAG*, wakati katika hao hao wazabuni

wanaodai, wengine wanajibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwamba suala liko kwa Katibu Mkuu Elimu na Mafunzo ya Ufundi na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nauliza, nani analo suala la madai ya watu wa Iyunga? Walipeni wazabuni wa Iyunga fedha zao ili Mbunge wao nitulie, nifanye kazi za kuchimba mabwawa na kusimamia barabara. Hatuwezi kusimamia kitu kimoja kila wakati, wakati wa kampeni tunaongea lugha hiyo hiyo, wakati tumeishaingia hapa sasa hivi badala ya kufanya shughuli za maendeleo, tunaongea lugha hiyo hiyo. Walipeni wazabuni wa Iyunga ili waendelee na maisha yao kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *MIST*. Japokuwa tunasema kwamba *MIST* inaelekea Chuo Kikuu, lakini nimejaribu kupitia kitabu cha hotuba ya Waziri, sijaona *MIST* imeguswa popote wala mchakato wowote wa kutuelekeza kule. Kwa hili nalo nitaomba maelezo. Lakini zaidi ya hapo, kuna wakazi wa maeneo yale ya *MIST*, wakazi wa Sistila takribani 881 wameondolewa katika ile ardhi na ardhi imechukuliwa na *MIST*. Wanadai mafao yao ili waendelee na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo lingine nililonalo katika Jimbo langu. Watu wa Sistila, watu wa maeneo ya *MIST* Iyunga wanataka kujua nini hatima yao katika suala zima la ardhi yao iliyochukuliwa ili waendelee na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaongea sana. Mwisho wa yote, nataka niwape pole wananchi wangu waliopigwa nondo juzi usiku akiwemo jirani yangu Alfa Kimario. Nasikitika kwamba nondo zimerudi kwa sababu *RPC* badala ya kuangalia usalama, sisi tulishaondoa suala la nondo, lakini yeye ameng’ang’ana tu na kuwakamata Wabunge wa CHADEMA pamoja na wafuasi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Lakini mimi nimekuomba kwamba nichangie mchana au kesho. Nilikuandikia *note*, sijui bahati mbaya imechelewa kufika kwako au vipi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, endelea!

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, basi kwa kuwa sikujiandaa vizuri, lakini nina mambo ya msingi ya kuchangia, wacha nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia hii nafasi. Awali ya yote, naomba nitoe pongezi sana kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo kwa jitihada kubwa ambazo imekuwa ikizifanya kuhamasisha umma na kutoa elimu ya uraia kwa njia ya maandamano ambayo hatimaye naona sasa hata Chama cha Mapinduzi kimeona umuhimu wa maandamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitumie nafasi hii pia kupongeza maandamano kwa jitihada za chama changu kwa kuwa mambo mengi yamefanikiwa

katika nchi hii baada ya wananchi kulalamika, siyo kwa hiari ya Serikali kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba likubalike kabisa na Watanzania wajue maandamano ni kitu muhimu sana kwa pale wanapotaka kusikika kwa yale yanayowasumbua katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Wizara hii ya Elimu ina matatizo makubwa sana ambayo yamekuwa ndiyo chanzo cha maandamano kila leo. Hakuna mwananchi anayetaka kuwa maskini. Umaskini ni kitu kibaya ambacho kila mtu anakikataa na kinaathiri maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wamekuwa ni kielelezo cha umaskini katika Taifa letu. Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Walimu wanafanya kazi kwa kubembeleza kupata haki zao, kitu ambacho ni kinyume. Ndiyo maana nasema maandamano hayatakaa yaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza walimu kwa kuwa wavumilivu, kwa sababu wangekuwa hawana uvumilivu, hakika wao ndio walikuwa wa kwanza kuanza kuandamana katika Taifa hili. Lakini sisi Chama cha Demokrasia na Maendeleo tunasema, tutaandamana kwa niaba ya walimu mpaka kuhakikisha na wao wanathaminiwa haki zao zinaheshimika, wapate mafao yao kwa wakati na Serikali izingatie kuhakikisha inaboresha maisha ya walimu kadri iwezekanavyo, waishi katika nyumba bora na wao waishi kama binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ya kushangaza sana, juzi hapa nilikuwa nyumbani, bahati mbaya namuuguza mama yangu, lakini nilishuhudia zawadi zikitolewa hapa na kupewa orodha ya wanafunzi waliofanya vizuri. Lakini mimi nilijiuliza, hizi Shule za Kata ambazo wanafunzi wamepata ushindi mkubwa zaidi, shule ambazo walimu wake hawatoshi, shule ambazo hakuna vifaa vya kufundishia, shule ambazo ukweli ni kwamba hakuna sifa nyingi za kuzisifu kiasi kwamba wanafunzi wakaweza kupata elimu bora na kuwawezesha kupata ushindi kiasi kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kama napinga kwamba sifurahi Shule za Kata zikifanya vizuri, lakini nina wasiwasi, isije ikawa ni mbinu zimefanywa kwa makusudi kwa kuwa tumekuwa tukilalamikia sana Shule za Kata kwamba hazifanyiwi vizuri, hazina ubora, hazina walimu wa kutosha, hazina vifaa vya kufundishia, ili kuwadanganya Watanzania sasa wafikiri zile shule ni bora, waanze kuwapeleka watoto waache kuwapeleka shule zenye ubora ambazo zina kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote mimi huwa naongozwa na dhamira yangu. Huwa nasema kile ambacho nakiamini, kile ambacho nakiona. Naona kuna haja kabisa ya kufanya utafiti wa matokeo ya mitihani ambayo yalitokea mwaka huu. Kuna haja ili tuweze kujua kama ni kweli Shule za Kata ndiyo zimefanya vizuri kiasi kile? Kuna tatizo gani katika shule hizi za watu binafsi, Shule ambazo zina walimu wa kutosha, shule ambazo zina vifaa vya kufundishia, shule ambazo ziko katika mazingira mazuri,

wanafunzi wafeli, wafaulu watoto wanaosoma katika shule ambazo zina mazingira ya miujiza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebidi niliseme hili kwa sababu kwa kweli linanisumbua katika akili yangu. Ningeomba nipate maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni miujiza gani imefanyika kwa hawa watoto waliofanya vizuri katika ya Shule za Kata ambazo tunazijua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, bado nipo katika Shule za Kata. Sasa hivi utaifa wetu unaingia mashakani. Sasa hivi kuna dalili zote za kuonyesha ukabila unakuja katika nchi yetu, jambo ambalo halifai na jambo ambalo linatakiwa kila kiongozi kulikemea. Lakini mimi katika kufikiri, nimegundua kwamba hizi Shule za Kata pia zinaweza kuwa ni chanzo cha kuleta ukabila katika Taifa letu kwa sababu watoto wanaishi katika mazingira yale yale ya wao kuwa pamoja, kabila lile lile moja, kiasi kwamba hawachanganyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nadhani tulifaulu katika Taifa letu ni pale zamani ambapo wanafunzi walikuwa wakibadilishwa maeneo. Mtoto, *primary* atasoma Iringa, *secondary* atasoma Dodoma, akija *High School* atasoma Tabora ili mradi ilikuwa wanafunzi wanachanganyika, matokeo yake wakakua katika malezi bora ya kuamini kwamba Watanzania wote ni ndugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie namna ya kurudisha utaratibu huu wa zamani wa kuwabadilisha watoto kusoma maeneo mbalimbali kwa malengo ya kuwachanganya ili kuleta mshikamano na upendo ili suala la ukabila katika Taifa letu lisiweze kuwepo. Hili ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, liendane na kwamba, kwa sababu najua Serikali ilifikia hapo wanafunzi wasome Shule za Kata jirani na maeneo wanayoishi kwa kukwepa majukumu ya kuwasafirisha, naunga mkono hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kusema kwamba mrudishe *warrant*, zitumike sasa hivi kwa ajili ya kuwasafirisha wanafunzi ili dhana ya ukabila isiwepo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na *style* hii ya Shule za Kata, hakika ukabila hatutakuwa na nguvu ya kuuzuia, utarudi, utakuja kwa nguvu na hatimaye hatutakaa tuelewane, nchi yetu itaingia katika vita vya kupigana wenyewe kwa wenyewe na upendo katika Taifa letu utapungua, jambo ambalo ni hatari katika Taifa ambalo linapenda amani kama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza mwanzoni kuhusu umaskini. Umaskini umekuwa kwa kweli ni tatizo. Lakini, umaskini huu ukianzia kwa mwalimu unakuwa ni tatizo kubwa zaidi. Mtu akiwa hawezi kumudu kuendesha maisha yake, hata akili yake kufanya kazi vizuri inakuwa ni tatizo. Anafungwa hata fikra kupanua wigo wa upana wa fikra zake kwa kuwa badala ya kuwaza maendeleo, badala ya kuwaza kazi ya kufanya darasani, anawaza kesho atakula nini, atalala wapi, ataishi vipi, atasafiri vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa kwa nguvu zetu zote kuhakikisha kwamba tunaboresha maisha ya walimu. Ukiacha kutatua matatizo ambayo yanatokana na wao kuchelewa kupata haki zao, hizo haki zenyewe ziboreshwe zitoshe, waboreshewe mishahara yao, mishahara yao bado hairidhishi na mpaka sasa Serikali haijatamka wazi inapandisha mishara kwa kiwango gani. Ni bora tuweke mambo wazi ili Watanzania wajue.

Sasa hivi Ualimu watu wanaona kama ni kifo, mtu akienda anaangalia tu mazingira aliyopelekwa na shule anayotakiwa kufundisha, kesho yake anageuza. Watoto wa Mijini wameshindwa kwenda Vijijini kufundisha kwa sababu wanapelekwa kuishi maisha ambayo hawakuyazoea. Leo mtoto anaishi Mjini toka amezaliwa anaona umeme unawaka, toka amezaliwa hajui shida, anapelekwa Kijiji ambacho umeme hakuna, barabara mbovu, nyumba ndiyo kama ya kufugia ng’ombe, ni vitu vya ajabu kabisa. Tunatakiwa tuboreshe maisha ya Walimu kwa sababu hawa ndiyo chanzo kikubwa cha kuleta elimu nchini na ndiyo wao wanaoweza kutupa mwongozo hata wa maisha yetu ya baadaye, Walimu wametufikisha hapa tulipo. Tunapowafikisha Walimu katika mazingira magumu kama hayo, tunatoa maneno mazuri tu katika hotuba ya bajeti lakini Walimu wanateseka, maisha wanayoishi siyo ya kibinadamu, wanahangaika, maji ya shida Vijijini, umeme hakuna, nyumba zinatisha, leo Walimu mnategemea watafundisha, wao wanaroho za kishetani kusema kwamba wana maruhani ya kuishi mahala pachafu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu hakiridhishi na hakipendezi, Walimu ni lazima tuwaboreshee maisha yao, Walimu ni lazima tuwaone ni kifaa ambacho kinatakiwa kulindwa kwa heshima na taadhima. Tuwape moyo wa upendo maana wanaishi kwa kutegemea mshahara ambao utatokana na kazi yao, kwa sababu Mwalimu hata ukisema afanye biashara, atafute mbinu zingine za kujitegemea akiamua kufanya hivyo ujue ni lazima wanafunzi wataathirika kwa sababu muda mwingi atautumia katika kujitafutia riziki ili aweze kujikwamua, matokeo yake hatakuwa na fursa nzuri ya kufundisha wanafunzi, shida zitaendelea kuwepo, watoto watakuwa wanaendelea kukosa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nisisitize kuhusu migogoro ya Vyuoni, penye ukweli patabaki kuwa na ukweli siku zote. Migogoro ya wanafunzi vyuoni, migomo ya wanafunzi vyuoni inatokana na huduma mbovu ambazo haziwatoshelezi. Wakitimiziwa mahitaji yao kwa wakati na wakisikilizwa shida zao na kutekelezewa mahitaji yao, hakuna migomo itakayotokea shuleni. Matokeo yake sasa badala ya kuwatekelezea wanafunzi mahitaji yao na kuzuia migomo kwa njia za halali, kuwakamilishia yale ambayo yanawafanya wagome, Serikali imekuwa ikitumia nguvu nyingi sana. Inafikia kutumia nguvu ya Dola ikiwa ni pamoja na kuwapiga risasi za moto wanafunzi. Hili ni jambo la hatari sana. Hawa ni wanafunzi ambao bado akili zao hazijakomaa, kila siku washuhudie risasi, washuhudie virungu na mabomu, tunajenga Taifa la ukatili, tunawapa mioyo ya kikatili wanafunzi, matokeo yake nchi hii itakuwa na watu makatili na tutashindwa kuwaongoza. Tunawafundisha watoto hawa kuwa na roho mbaya, watoto hawa tunawafundisha kutokupendana, watoto hawa tunawatia ujasiri wa mapambano kinyume na taratibu za nchi yetu kama tulivyolelewa na marehemu Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upendo unatokana na wazazi kuwaonyesha ni namna gani tunawapenda watoto na wao kuwasisitizia waishi katika upendo ni kuwazuia kupambana, kugombana na kupigana, lakini kinyume chake sisi viongozi ndiyo tunatumia Dola kuwapa ujeuri wanafunzi, kuwafundisha ukatili, kuwafundisha roho mbaya, kwa sababu mwanafunzi kama anashuhudia umwagikaji wa damu, mwanafunzi anashuhudia mtu akipigwa virungu kama mnyama atakuwa na upendo wa namna gani yeye asimfanyie mtu mwingine? Tunahalalalisha vitendo hivi vya kiharamia na vitendo vya kikatili. Naomba sana Waziri wa Elimu, turudi nyuma na tujitafakari, tuangalie ni jinsi gani tuweze kulea Taifa letu, tuangalie ni jinsi gani tutumie Dola yetu. Dola isiwe chombo cha kuwatishia watu na kuwaumiza na kuwakandamiza na kuwaua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe salamu kwa Jeshi la Polisi, tabia hii wanayoifanya ya kupambana na wananchi bila sababu, hata katika masuala ya msingi, nazungumzia masuala ya elimu, elimu ni pamoja na Elimu ya Uraia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nakushukuru sana muda wako umekwisha.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Namwita sasa Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambayo ni Wizara yangu, mimi ni Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze bajeti hii, ni nzuri, imeonesha kabisa kwamba ina nia ya kutaka kuboresha utoaji wa taaluma katika nchi ya Tanzania ingawa bajeti ni ndogo. Naomba Serikali itazame upya Wizara hii, fedha hizi ni ndogo kulingana na kero zilizomo katika Wizara hii. Kama Waziri atakuwa anapewa bajeti ndogo, vitendea kazi namba moja katika Wizara ni fedha, naomba sana Serikali itazame suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ombi langu hilo la kwanza, napenda nizungumzie kuhusu madai ya Walimu. Inasikitisha sana tunapopewa taarifa na Walimu, mlolongo wa fedha nyingi wanazodai. Kwa mfano, Mkoa wa Singida wameniletea taarifa kwamba wanadai shilingi milioni 548, ndugu yangu tunakwenda wapi? Fedha hizi ni nyingi mno, huu ni Mkoa mmoja tu na Wilaya zake, bado Taifa zima linadai zaidi ya bilioni 29. Kutangaza mgomo kwa Walimu ni hatua ya mwisho sana, sitegemei Walimu wafike huko, navyowajua ni waadilifu kwelikweli. Naiomba Serikali ifike wakati sasa kupitia bajeti hii iweze kumaliza kulipa madai ya Walimu. Walimu watafurahi sana, mtakuwa mmewaongezea ari ya kazi endapo watasikia Waziri akitamka kwamba madai yao yote yatalipwa kupitia bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia kama Waziri hatatamka hili, mtawafikisha Walimu mahali pagumu au kwenye lengo ambalo hawakulitarajia. Sitegemei Walimu wa Tanzania wanaweza wakagoma bila sababu za msingi na sitegemei wagome. Naiomba sana Serikali ihakikishe inatafuta fedha mahali popote kwa namna yeyote ili kuhakikisha Walimu wote wanalipwa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tunalimbikiza madeni haya yote sababu ni nini? Kwa nini umhamishe Mwalimu wakati huna hela, kwa nini umpe safari Mwalimu wakati huna hela? Wapeni majukumu Walimu wakati mna fedha za kuwalipa, huwezi kumhamisha Mwalimu wakati huna hela, huko kote ni ku-*create* madeni, kwa nini tunayatafuta madeni? Naomba sana tuwatendee haki, kama kweli mnaona ni rahisi Mwalimu kupewa uhamisho ajitegemee, aende kwa gharama zake, hebu na Wabunge leo msiwape posho tuone kama watakubali, kaeni mwezi mzima Wabunge hapa hawana posho kama patakalika hapa! Kama mnaona kwamba ni wajibu kwa yeyote kufanya kazi na alipwe basi na Walimu tuwafanyie hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya Walimu inasema Wajibu na Haki. Walimu wako tayari kutimiza wajibu wao, lakini hawapati haki zao vilivyo, tunawavunja moyo. Naiomba sana Serikali, Walimu ni kundi kubwa sana katika Taifa hili, ni aibu sana endapo tutafikia hatua ya Walimu kutangaza mgogoro na Serikali, kundi kubwa kama hilo. Naamini Waziri ni Kaka yangu, ni mtu mwenye upendo na Walimu na muadilifu kwelikweli, ombi langu atalisikia kwa makini na kwa huruma ya hali ya juu sana, nina hakika kesho atatoa jibu katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu *OC* ya Idara ya Elimu, tunaenda wapi? Idara ya Elimu ni Idara kubwa sana Mkoani, lakini sasa hivi imekuwa ni kieneo kidogo, kimekuwa chini ya Meneja wa *Cluster*. Meneja wa *Cluster* anashika Idara karibu tano, Mhandisi wa Maji, Idara ya Kilimo iko chini yake, Idara ya Utamaduni na Michezo, Idara ya Elimu pamoja na Afya, hivi kweli huyu mtu mmoja mkimkabidhi Idara hizi zote ziwe chini yake, Afisa Elimu wa Mkoa akitaka kufanya kazi zake ni mpaka aende kuomba hela kwa Meneja wa *Cluster,* hivi kweli mnamtendea haki Afisa Elimu? Taasisi kubwa kama hiyo, si afadhali Afisa Elimu angepewa U-Meneja wa *Cluster* tungeelewa, Idara kubwa ndani ya Mkoa. tunaiomba Serikali, Idara ya Elimu ipewe *OC* yake. Kumtegemea mtu tunakwamisha taaluma katika Mikoa yetu. Najua kupanga ni kuchagua lakini hapa mimi sioni kama tumekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mikopo ya Vyuo Vikuu, hivi tangu tumeanza kuwakopesha hawa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, ni shilingi ngapi ambazo tumewakopesha na ni shilingi ngapi zimesharejeshwa? Utafiti wangu unaonyesha kwamba ni fedha nyingi zinazokopeshwa hazirejeshwi na hazirejeshwi kwa sababu wasomi hawa wanapomaliza masomo yao wanakosa ajira, kujiajiri hawawezi. Hivi huyu msomi atarejesha vipi pesa kama hana ajira? Natoa ombi kwa Serikali na naomba Wabunge mniunge mkono, naiomba Serikali ifikie mahali sasa tuwape fedha hizi wanafunzi wa Chuo Kikuu bure, tusiwakopeshe tena kwa sababu ni kama tunatwanga maji kwenye kinu hazirudi, sasa kama pesa hazirudi, si bora tujue kwamba hizi tumetoa

bure tu. Naishauri Serikali kwamba tutoe fedha hizi bure kwa sababu urejeshwaji wake ni utata, mpaka sasa hivi hata takwimu sidhani kama ziko sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja nilikuwa naongea naye juzi akasema kwamba Mheshimiwa mimi ni mpaka nilijisalimisha mwenyewe, Serikali haikunidai, nimekaa miaka kama minne nikaamua kujisalimisha mwenyewe, sasa inafikia hatua ya mtu kujisalimisha mwenyewe, anawaambia kwamba mimi nilikopa nahitaji kurejesha! Je, hao wasiokuwa na moyo wa kujisalimisha si matatizo makubwa? Naomba Serikali itafakari katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mitaala ya elimu, kila Mtendaji Mkuu anapoingia, anaingia na mtaala wake, akiingia mwingine anaingia na mtaala wake, hivi jamani Serikali hata Sera ya Elimu haipo? Hatufuati Sera ya Elimu, naomba twende na Sera. Kubadili mitaala kila leo na tunabadili mitaala lakini Walimu hatuwapeleki kuwasomesha, Mwalimu amechukua mafunzo miaka 20 iliyopita leo unaleta mtaala mpya unategemea nini hapa, kuna taaluma nzuri itatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tutafakari katika hili, suala la kubadilibadili mitaala ya elimu, hatuwatendei Walimu haki, hatuwatendei wanafunzi haki, kwa sababu Walimu wanakuwa hawana taaluma ya mitaala hiyo mipya. Kama tunabadili mitaala, tuwapeleke na Walimu wakachukue mafunzo hata ya muda mfupi itasaidia ili waweze ku-*match* na mitaala hiyo. Kama haiwezekani basi hatuna sababu ya kubadili mitaala, twende na Sera ya Elimu, siyo kila mtu anayeingia inakuwa kama kampuni yake, hii siyo kampuni ya mtu. Wizara ya Elimu ni Idara ya Serikali inatakiwa ifuate Sera ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Elimu ya Watu Wazima. Katika watu ambao ukiwaelimisha uzalishaji wao ni wa muda mfupi ni hawa wa Elimu ya Watu Wazima. Wanafunzi wa Chuo Kikuu tunawasomesha kwa muda mrefu lakini huyu wa Elimu ya Watu Wazima siku chache tu anaanza kuwa mzalishaji. Kwa sababu mtu kama hajui kusoma na kuandika hata ukimpa u-mama lishe hataweza kufanya kwa sababu mahesabu hajui, hata kutengeneza mradi hajui. Naomba Idara ya Elimu ya Watu Wazima ifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 kulikuwa na Katibu Mkuu mmoja alisema kwamba Elimu ya Watu Wazima itakuwa ni Idara inayojitegemea lakini mpaka leo sijaona utekelezaji wake, Idara hii haina fedha, Afisa Elimu Watu Wazima yupo pale tu, ana mikakati mizuri lakini utekelezaji wake unahitaji fedha, hana fedha. Naomba Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kiwe kitengo kinachojitegemea, nina uhakika tutaondokana na wimbi kubwa la watu wasiojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma katika watu kumi wasiojua kusoma ni mmoja, lakini leo hii katika watu kumi watatu hawajui kusoma na kuandika, tunakwenda wapi, tunapanda kielimu au tunashuka? Naomba Kitengo hiki cha Elimu ya Watu Wazima kiboreshwe, kijitegemee ili kiwe na fungu lake kiweze kujiendesha na kiweze

kufundisha watu wazima kwa kutumia programu zake za MEMKWA, MKEJA na mambo mengine mengi lakini Kitengo hakina fedha na pia hakina meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu Vyuo vya VETA. Naipongeza Serikali kwa kuamua kwamba kila Wilaya iwe na Chuo cha VETA. Namwomba Waziri kwamba katika Mkoa wa Singida, Wilaya ya Manyoni ina majengo yaliyopo katika Kata ya Njirii yaliyoachwa na wakandarasi wa barabara, ukienda Wilaya ya Iramba, Kata ya Ulemo kuna majengo yaliyoachwa na Wakandarasi wa barabara pia, naomba majengo hayo yatumike kwa kujenga Vyuo vya VETA. Sisi tulishapitisha kwenye *RCC* chini ya Mkuu wa Mkoa wetu, naomba sana unapoangalia vipaumbele angalia Manyoni na Iramba kwa sababu tunayo majengo, yasije yakaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye alikuwa msemaji wetu wa mwisho, kabla ya kusitisha, naomba niwataje ambao tutaendelea nao saa kumi na moja tukirejea, Mheshimiwa Albert Obama, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Salome Mwambu na Mheshimiwa Riziki Omar Juma. Hawa ndiyo wataanza kuchangia tutakaporejea saa kumi na moja jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni, ahsanteni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Kwanza, nichukue nafasi hii, kupongeza Hotuba zote tatu nzuri kabisa kutoka kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo, ilitolewa na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na Hotuba nzuri tena iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii pamoja na ile ya upande wa Upinzani. Ndani ya ile hotuba, kwanza, kabla sijaendelea niseme kwamba mimi ni mmoja wa Wanakamati wa Kamati ya Huduma za Jamii. Mimi ninao mchango mdogo tu kwa mambo yafuatayo hasa yanayohusu Wizara ya Elimu. Tulikutana nao, tulikuta kwanza kuna tatizo kubwa sana la Wakurugenzi Kukaimu. Tuna tatizo kubwa sana Wakurugenzi wa Elimu karibu tisa (9) tuliokuwa tunakutana nao, wengi wote wanakaimu kuonyesha kwamba huenda hawajawa na uwezo wa nafasi hizo. Sasa rai yetu ni kwamba Wizara na Serikali, ihakikishe kwamba watu hawakaimu kwa muda mrefu. Wako watu pale wamekaimu kwa miaka mitano, watu wamekaimu kwa miaka sita, siyo kitu kizuri, wanashindwa kutoa maamuzi ya maeneo yao na vitengo kwa sababu huenda wanaogopa kukosea. Kwa hiyo, tungeiomba Serikali hilo irekebishe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilivyokuwa najaribu kuangalia Wizara hii, inaanzia Shule ya Vidudu mpaka Elimu ya Juu. Nafikiria huenda ifike mahali ugatuaji huu uliotokea hizi shule nyingine kwenda TAMISEMI, basi ningeshauri TAMISEMI iendelee ku-*deal* na sekondari, shule za msingi na shule awali ili hii Wizara ya Elimu iendelee kushughulikia *high learning institution* na *vocation training* ili viweze kufanya kazi vizuri kwa sababu elimu ni taasisi, kubwa ni pana na imesambaa nchi nzima. Kwa hiyo, naona kwamba siyo vizuri malalamiko ya Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanakutana tena na Mwalimu wa Shule ya Awali kwenye Ofisi ya Waziri, wanalalamikia Ofisi moja, nafikiri siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu Elimu ya Juu, hapa napenda kuzungumzia suala la mikopo. Nashukuru Serikali kwa kuanzisha hii 4% ya *Skill Development Levy* kuwekwa pale kwa ajili ya kutatua tatizo la mikopo na fedha ambazo kwa kweli zilikuwa hazikidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye migomo ya wanafunzi wetu kwenye Vyuo Vikuu, Serikali tusijivue wajibu wetu. Huenda migomo mingine ni ya halali kabisa kulingana na stahiki zao walizotakiwa kupata hatuwapi. Sasa kwa kuwa hatuwapi zile stahiki, tusitumie kizingizio kama Serikali na sisi upande wetu kuona kwamba ni siasa imeingia. Tumeomba kwamba nalo mlione na tulivyotembelea Bodi ya Mikopo ilikuwa inasema wakati mwingine fedha hazijatoka Hazina au *TCU* hawajaleta majina au Vyuo Vikuu havijaleta ripoti. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara napo tujipange, tusikae tukafikiri kwamba migomo yote inayotokea inahusiana na siasa, huenda mingine ni ya utendaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye mitaala. Mitaala ya Wizara ya Elimu kwenye shule zetu imekuwa ikibadilika kila wakati. Ni rai yetu kwamba sasa tuanze kuwa na sera kwamba mitaala haitakuwa inabadilika kila Waziri anapoingia madarakani. Kuna Waziri anaingia anasema michezo isifanyike, kuna Waziri anasema Jiografia isifundishwe, sasa hiki kitu siyo kizuri, nafikiri tuwe na sera ambayo ina-*cover* Waziri yeyote anayeingia kwenye cheo hicho akute ule muundo na mitaala inayoeleweka na vitabu gani vinavyotumika kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Baraza la Taifa la Mitihani kwa kuzuia uvujaji wa mitihani sasa Tanzania. Tulikutana nao, walionyesha kwamba kwa kweli wameweza ku-*control* uvujaji wa mitihani. Naomba nitoe pongezi kwa Baraza la Mitihani la Taifa, kwa sababu hiyo ilikuwa ni kero ambayo ilikuwa inasumbua Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Kitabu cha Hotuba, ukurasa wa 94, utagundua kwamba Idara ya Ukaguzi haifanyi kazi vya kutosha. Utaona kwamba zile asilimia zilizopo pale na wote mna vitabu na mnaweza mkaona, asilimia ni ndogo kwelikweli. Inaonyesha kwamba Tanzania Kitengo cha Ukaguzi kimekufa na ufanisi wake haupo kabisa. Unaweza ukaangalia ukaona katika ukaguzi shule za msingi kwa mfano shule zilizotakiwa kukaguliwa ni 16,001 lakini shule zilizokaguliwa ni 1276

ambayo ni asilimia ndogo sana kabisa katika kukagua. Kwa hiyo, sasa ni vizuri hiki kitengo nacho kiwe imara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuiomba Wizara, huu mtihani wa *Form Two*, ambao tumeufuta, nafikiri ni kitu kizuri, kwa sasa hivi wanafunzi wanajua wana uhakika wa kumaliza lakini hawasomi vya kutosha. Tungeomba ile mitihani ya *Form Two* irudishwe ili wanafunzi sasa wajipime. Hii kuwa tunatoa kwa sababu ya kuogopa gharama, siyo kitu kitakachotusaidia. Kuna gharama ambazo tunaweza tukazikwepa mahali pengine tukaweka hapa vijana wetu wakawa wanapimwa jinsi wanavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa najiuliza ukiangalia shule za msingi hatuna Walimu, shule za sekondari tuna upungufu wa Walimu, Vyuo vina upungufu wa Walimu, Vyuo Vikuu vina upungufu wa Walimu, unakuta Wahadhiri hamna, Wakufunzi hamna, sasa ni vizuri kwa kweli twende mbele. Vyuo Vikuu tulivyonavyo ni vichache na nina imani kwamba mkakati maalum ukiwekwa hatuwezi kuwa tunakosa Wahadhiri kwa sababu Vyuo Vikuu hivi viko, kila siku wana-*graduate,* tunawezaje kukosa Walimu hasa wa Vyuo Vikuu na sehemu nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, huu utaratibu wa kusambaza Walimu, tungeomba kwa kweli kwa sisi tulioko Mikoa ya pembezoni Wizara ijaribu kuona kwamba inatuletea Walimu wa kutosha kulingana na idadi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija upande wa Jimbo au Mkoa wa Kigoma, sasa hivi shule za sekondari pale tuna upungufu wa karibu Walimu 357 wa Sekondari. Ombi langu kwa Wizara, kuna vijana wengi ambao wana-*graduate* sasa, Kigoma inahitaji Walimu, naleta kama ombi rasmi na iandikwe kwamba Mheshimiwa Obama ameomba Walimu waende Mkoa wa Kigoma, Jimbo la Kasulu Mjini, Vijijini na sehemu nyingine kama Namanyovu ili waweze kukidhi haja ya uhaba mkubwa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wilaya yetu ina upungufu wa vitabu vya Biolojia karibu 4,800, *Chemistry* 4,800 *Physics* 4,800 na Hesabu 9,600. Kama pale Wizarani kulingana na nilivyomsikia Naibu Waziri kipindi fulani akisema vitabu mnavyo basi ni ombi kabisa, nimeambiwa na Walimu tena vya masomo ya sayansi, tunaomba mtusaidie kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nimepigiwa simu wakati nakuja, ni madeni ya Walimu. Madeni ya Walimu yamekuwa makubwa, sasa *morale* inashuka hasa kwa sisi tulioko pembezoni ambao wanategemea mishahara yao, tunaomba kwa kweli kwa Mkoa wa Kigoma mnaweza kutuhakikishia na kutuletea haraka. Madeni yameshakuja, Kasulu kwenye rekodi yetu tunadai milioni 68.5, Kibondo tunadai milioni 34, Kigoma Vijijini zinadaiwa milioni 69, Kigoma Mjini zinadaiwa shilingi milioni 122. Kwa hiyo, Mkoa wa Kigoma ukiuangalia na ulivyo pembezoni na watu hawana vitu vingine, wanadai jumla ya shilingi milioni 295. Hawa ni Walimu wanaona kwamba ni vizuri tuwasemee. Kwa hiyo, kama kuna mgao utaanza kutoka Hazina, Wizara

inayoshughulika, Walimu wa Kigoma wanaomba wafanyiwe haraka kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kama tunavyojua kwamba sehemu kubwa ya Mkoa haina umeme. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Wizara kama kuna upendeleo wa lazima tuweze kupewa *solar* kwenye Shule zetu za Kata ili vijana wetu saa nyingine wawe wanarudi saa mbili kujisomea hata ikifika saa tano usiku waweze kurudi majumbani. Kama mpango huo upo, tunaomba kwa kweli tuweze kuwekewa *solar* ili vijana wetu waweze kusoma katika shule zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vijana wasio na uwezo ndani ya Halmashauri yetu ya Kasulu, tumejaribu kufuatilia kuona ni wapi bajeti imetengwa kwa ajili ya kusaidia wazazi ambao vijana hawa wamefaulu lakini hawana uwezo. Ni jukumu la Wizara na ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imesema kwamba itasaidia wale ambao hawana uwezo. Tunaomba mtupe mwongozo, kuna vijana wengi wamefaulu lakini wameshindwa hata kujiunga kwenye Shule za Kata, kwa hiyo, tunaomba mtupe mwongozo ili vijana wetu waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya vijana wanapomaliza shule za msingi au sekondari kuomba Ualimu. Ilikuwa ni ombi siyo lazima maombi yote yawe yanakusanywa Wizarani. Maombi yote ya wanaoomba Ualimu yana uwezo wa kupelekwa Wilayani, Wilaya zikakusanya na zikawa na takwimu ni vijana wangapi katika Wilaya yao wameomba hizo kozi ili nayo Wizara ipokee majina hayo kutoka kwenye Wilaya badala ya yote kuja kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo. Kwanza yanakuwa mengi, halafu saa nyingine hata kurekodi inakuwa vigumu. Kwa hiyo, ni wito wangu kwamba zinaweza zikafanywa kwa Mkoa hata *selection* nyingine zinaweza zikawa zinafanyika kwa Mkoa, ili mradi tu kwamba Mkoa mmeupa mgao kwamba ndani ya Mkoa wa Kigoma, tutataka wanafunzi kadhaa. Kwa hiyo, Mkoa unaweza kuchagua na hii itatusaidia ku-*balance,* kuona kwamba na Mikoa mingine haiachwi nyuma kwa sababu ya uchache wao au uwingi wao. Mtupe mgao kama mnavyofanya bajeti mnaposema *ceiling* ni hii na Kigoma mtupe *ceiling* yetu, tuwaletee wanafunzi kulingana na vipaumbele ambavyo tutakuwa tumeona ndani ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi maalum. Nilipotembelea Vyuo viwili vya Ualimu vya Kabanga na Chuo cha Ualimu TTC, walinituma yafuatayo. Chuo cha Kabanga ambacho kinafundisha Walimu, kimeniomba gari, nije niwaambie Taasisi zinazohusika na Wizara kwamba wanalo gari ambalo lina muda mrefu sana tangia nafikiri mwaka 1980 kwa hiyo, wanaomba gari. Hilo ni ombi *special* wameniambia nikuambie Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo ombi tena la TTC, Chuo cha Ualimu Kasulu, pale kinafundisha vizuri na kina uwezo mkubwa, tatizo lao ni madarasa. Kwa hiyo, wameomba madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa fursa ili kusudi niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nimnukuu Profesa mmoja ambaye ni mtalaam wa masuala ya elimu na pengine naweza kujielekeza kwenye hoja. Yeye aliweza kufafanua tafsiri ya elimu kama ifuatavyo. Alisema kwamba, *education is the process of transferring desirable habits, skills, knowledge and attitudes that makes an individual fit into the society*. Kuna vitu vinne (4) vya msingi ambavyo mtalaam huyu yeye aliweza kuona kwamba ni msingi kwa mtu yeyote ambaye anaweza akaonekana kwamba amepata elimu na ameelimika. Amezungumzia *desirable habits*, amezungumzia *skills*, amezungumzia *knowledge* na amezungumzia *attitude*. Kwa hiyo, mtu yeyote ambaye ameelimika, ni lazima aweze kuwa amefuzu katika vigezo/nyanja hizo nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tukijaribu kufanya *assessment* kwenye mfumo wa elimu yetu ambayo tunatoa hapa nchini, tunajikuta kwamba wakati mwingine hatuwezi kuwafikisha wanafunzi au watu mbalimbali ambao wana lengo la kujipatia elimu kwa kiwango kile ambacho mtaalam huyu alikusudia watu waweze kufikia kiwango hicho. Ni kwa nini labda pengine elimu yetu inaonekana kuwa ya kulegalega yaani haiwezi kukidhi viwango? Taifa lolote ambalo haliwezi likawaelimisha watu wake, likahakikisha kwamba wanaweza wakawa *competent* katika *aspect* hizo nne, Taifa hilo kupiga hatua katika *aspect* yoyote ile ya maendeleo itabaki kuwa ni ndoto ya kizungumkuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, tuna vitu mbalimbali ambavyo vinaweza vikasaidia kuweza kuhakikisha kwamba elimu yetu inazidi kuimarika na siyo kudumaa. Moja, tuna kila sababu ya kuhakikisha Serikali inaimarisha Kitengo cha Ukaguzi kwa maana katika viwango mbalimbali vya elimu kwa maana ya shule za msingi, sekondari mpaka vyuo. Idara ya Ukaguzi, ambayo inajishughulisha na elimu ya msingi pamoja na elimu ya sekondari, ni kama vile imetelekezwa, huduma ni duni kwa Wakaguzi wetu. Kwa mfano, zipo taarifa kwamba bajeti ya mwaka jana walitengewa bajeti ya wastani wa shilingi bilioni nne na kidogo lakini fedha ambazo zimepelekwa kwenye Idara ta Ukaguzi ni takribani kama milioni 900 na kidogo kutoka kwenye bilioni nne. Sasa hapa hatuwezi tukategemea kwamba Wakaguzi wetu watakuwa *efficient* katika suala zima la kuweza kuzunguka hapa na pale kwenda kuangalia kwamba shule zetu zinaendeshwa namna gani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikuombe katika bajeti ya mwaka huu pengine uangalie, fedha ambazo mtakuwa mmetenga kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi basi fedha zote mhakikishe zinawafikia. Ni kilio na ni tatizo kwa Idara ya Ukaguzi hapa nchini katika maeneo mengi ikiwemo Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Manispaa ya Kigoma Ujiji, walipewa kwa mwaka mzima shilingi kama milioni moja tu, gari hawana, wamekuwa ni watu wa kuombaomba kwenye Ofisi za Wakurugenzi hususan kwa Maafisa Elimu, wanakwenda kuomba magari ili kusudi waweze kuzunguka kwenda kufanya ukaguzi mashuleni. Sasa unategemea huyu Mkaguzi ambaye anaomba usafiri kwa Afisa Elimu ataweza kutoa taarifa nzuri dhidi ya Afisa Elimu aliyempatia usafiri? Saa ngapi huyu Mkaguzi atakuwa

huru? Hapa naomba Wizara hili suala iliangalie, Manispaa ya Kigoma Ujiji, Idara ya Ukaguzi wanahitaji gari ili kusudi waweze kufanya kazi zao vizuri. La sivyo tutaendelea kusema kwamba Wakaguzi hawafanyi kazi zao vizuri kumbe tatizo kubwa ni Wizara kuitelekeza Idara ya Ukaguzi kwa kutokuwapatia vitendea kazi muhimu ili kusudi waweze kutimiza wajibu wao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bajeti kama nilivyosema kwenye Idara ya Ukaguzi, ndio kama ambavyo imeonekana. Fedha zimetengwa bilioni nne katika mwaka 2010/2011 lakini imepelekwa milioni takribani 900 nchi nzima, hizi ni fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza katika hilo, Idara ya Ukaguzi imeonekana kwamba ilipaswa kuwa ni Idara ambayo inajitegemea, muitoe kwa Kamishna wa Elimu. Hilo suala mlikuwa mmejadili wakati fulani nilipata kusikia huko kwamba mlikuwa mmeamua kwamba mwaka huu huenda ingekuwa ni Idara ambayo inajitegemea na ikawa na fungu lake la bajeti. Suala hili kwenye bajeti sijaona kwamba kweli Idara ya Ukaguzi imeweza kufanywa kama ni *Independent Department* ambayo itakuwa ina-*operate* yenyewe kila siku ili kuweza kuiepusha masuala ya kuweza kuwa *interfered* na mamlaka nyingine. Naomba Mheshimiwa Waziri tutumie tu akili ya kawaida, tuhakikishe kwamba Idara hii tunaifanya kuwa ni Idara ambayo ni huru. Tuifanye kuwa ni Idara ambayo ni *independent* na iweze kuwa na fungu lake la bajeti, tuwaepushe Wakaguzi wetu kwenda kuombaomba vitu kama magari kwa Maafisa Elimu ambao tunategemea wakati mwingine Wakaguzi hao watakwenda kuwakagua kwa sababu haiwezekani watu hawa wakawa huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kuhusiana na Idara ya *TSD*. Nashukuru na Waziri wa Utumishi yuko hapa, naomba naye pia aweze kunisikiliza ninachokwenda kusema. *TSD* kwa maana ya *Teacher's Service Department* ambao wanashughulika na masuala ya kuwa-*promote* watumishi kwa maana ya Walimu, kuhakikisha kwamba madaraja yao yamekaa vizuri, watu hawa wanalalamika sana kwamba hamuwapelekei pesa hata zile pengine kidogo ambazo Serikali inakuwa imetenga matokeo yake, matatizo kama ya kuwapandisha Walimu madaraja imekuwa ni tatizo kubwa sana ikiwemo kwa Walimu wa Jimbo la Kasulu Mjini, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. Hili sio tatizo la Wilaya ya Kasulu peke yake, ni tatizo la Mkoa wa Kigoma na nchi nzima kwa taarifa zilizopo. Kwa mfano mwaka jana aliyekuwa Katibu wa *TSD* Wilaya ya Kasulu, analalamika sana kwamba Walimu wanamsumbua juu ya suala la kikao kuweza kukaa na hivyo Bodi ile ya Ajira kuweza kuhakikisha kwamba wale watu wanakaa ili kuweza kuwabadilishia Walimu muundo wao wa ajira, wameshindwa kukaa kwa sababu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, haijaweza kuwapelekea pesa, kwa hiyo, vikao vimeshindikana kukaa kwa sababu wanasema wanakaa ni *quarter system*. Mama yangu Hawa Ghasia, Waziri wa Utumishi, naomba suala hili kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu, Walimu wangu wanapiga kelele kule, sasa kama Walimu wanalalamika madaraja hawapandishwi, wanapoomba pesa kwa ajili ya kwenda masomoni, wanapoomba likizo inakuwa ni migogoro, badala yake tunakuwa tunawalazimisha wao waendelee kubaki tu kufanya kazi, *promotion* hawapati, saa ngapi Mwalimu huyu atakuwa na moyo wa kusema ngoja afanye kazi ili kusudi kuhakikisha kwamba anaweza akatoa elimu ambayo ni bora? Kwa hiyo, tunawavunja

moyo Walimu wetu, matokeo yake hawawezi wakafanya kazi vizuri kwa sababu tatizo kubwa liko Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna Walimu wengi sana katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu hawajapandishwa madaraja yao. Niombe Mheshimiwa Waziri, wakati unajumuisha hotuba yako na niombe Waziri wa Utumishi naye pia akusaidie, mnieleze ni nini mustakabali wa Walimu ambao wamesoma, waliokuwa *Grade A*, wamesoma wamefikia kiwango cha Shahada, wengine wamefikia Stashahada, ni lini watapandishwa madaraja yao na kubadilishiwa miundo ya utumishi kwa sababu ni tatizo la muda mrefu na tatizo limeonekana kwamba ninyi hamjapeleka pesa kule. Hili sio tatizo la Kasulu pekee yake bali ni tatizo la maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, katika Bunge la mwezi Februari, 2011 nilizungumzia tatizo lililopo baina ya *Training and Education Policy* ya Tanzania ya mwaka 1995 ukihusianisha pamoja na suala zima la *Teaching Syllabus* katika masomo mbalimbali tuliyonayo. Kuna tatizo kubwa la Sera zetu za Elimu. Ukiichukua Sera hii ya Elimu ya mwaka 1995, ukaja kuangalia na *Teaching Syllabus* kwa maana ya mtaala, unakuja kukuta kuna tofauti kubwa sana. Kwa mfano, leo ni aibu na naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu uende ukafanye utafiti, Mao Tse-Tung alipata kusema "*No research, no right to speak*" naomba uende ukafanye utafiti katika hili ambalo nakwenda kulisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu leo ukienda kwenye muhtasari wa somo la Hisabati wa Shule ya Msingi ulioandikwa kwa lugha ya Kingereza na ule ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili, ukienda kwenye *section* ya malengo pekee yake, malengo ya elimu ya msingi kwenye *syllabus* iliyoandikwa kwa Lugha ya Kiswahili yaonekana yako 18, huku ukija kuchukua muhtasari wa somo hilohilo moja, somo la Hisabati kwa elimu ya msingi, malengo ya elimu ya msingi yanaonekana yako saba (7). Kiwango kimoja cha elimu, somo moja, nchi ni moja, lakini somo moja hilohilo malengo ya elimu ya msingi yamekuwa huku yako 18 huku yapo saba (7). Kuna tatizo kubwa, nina wasiwasi na uelewa wa watu wetu waliopo Wizara ya Elimu katika suala zima la kuandaa Sera za Elimu ya nchi yetu. Huwezi somo lilelile moja, kiwango kilekile kimoja, unakuta malengo yamekuwa *stated* tofauti, sijui kuna tatizo gani. Sasa kama kwenye malengo tumekosea yanayofuata huko ndani kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninasema inawezekana mchawi wa kwanza wa elimu yetu kuendelea kudumaa itakuwa ni baadhi ya Watendaji waliopo Wizara ya Elimu, waliopewa kazi ya kuweza ku-*develop curriculum* zetu ili kusudi ziweze kuhakikisha elimu tunayoipata inatusaidia hapa nchini. Niombe Mheshimiwa Waziri, wakati unatoa ufafanuzi, utueleze ni kwa nini *objectives* zimekuwa *stated differently* wakati somo ni moja tena kiwango kilekile kimoja na unakuta kwamba pengine ina *differ* na *Training and Education Policy* ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, katika kuchangia hotuba hii, ningeomba nieleze jambo moja. Wakati Msemaji wa Kamati ya Huduma za Jamii, akiwasilisha hapa, amezungumzia suala la migomo katika Vyuo Vikuu. Naomba niseme kwamba si kwamba

wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanapogoma kwamba wanagoma bila kujua, bila kuwa na sababu ya msingi. Kwa bahati nzuri, sisi ni vijana na tumetoka Vyuo Vikuu majuzi, tatizo kubwa ambalo limekuwa linapelekea na kuchochea migomo katika Vyuo Vikuu, ni tatizo la mikopo, Serikali mnapata kigugumizi gani kuweza kuifumua *Management* ya Bodi ya Mikopo kwa sababu tatizo litakuwa Bodi pamoja na maeneo mengine ambapo pesa za Bodi ya Mikopo hupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi nimemaliza Chuo Kikuu mwaka jana, nakumbuka wakati nikiwa Chuo Kikuu nilikuwa Mbunge wa Serikali ya Wanachuo, nilimwita Rais baada ya kupata fununu kwamba pesa zimekuja, lakini inaonekana zimekwamia mahali fulani. Niliwachukua wanachuo, tukafanya maandamano, tukaenda kwa amani, tumeandamana tukaenda katika Benki 'X'. Tukafika pale tukamwambia Meneja tunataka pesa zetu, tumeambiwa pesa ziko hapa. Tukamwambia usipotupa pesa, utatutambua kwamba sisi ni watu gani, kesho yake tulipata lakini tumekuwa tunazuiwa katika Vyuo Vikuu vyetu kwamba tusiandamane na kugoma. Nakumbuka wakati ule tumehangaika zaidi ya mwezi mzima, ukiuliza Bodi watakuambia kwamba pesa tumeleta, tatizo lipo huko, kwa hiyo utakuta kuna *connection* baina ya Bodi na watu wengine, sio kwamba pesa kuchelewa Vyuoni na wanafunzi kuamua kugoma kwamba wanagoma bila ya kuwa na sababu za msingi, wakati mwingine niombe mtutumie sisi vijana kwa sababu tumetoka huko majuzi, pengine tuwasaidie mawazo, tuwaambie kuna tatizo gani. Kwa sababu haiingii akilini katika mazingira ya kawaida na wale watu ambao wako katika Vyuo Vikuu, sio kwamba wote ni watoto, kuna watu wazima, kuna wazee wanasoma pale, wengine wametuzaa, lakini na wao pia wanadiriki kugoma. Kwa hiyo, hoja sio ujana wala uzee, hoja ni tuangalie ni kwa nini Wanavyuo wa Vyuo Vikuu wanagoma, ni kwa nini wanaandamana, maslahi yao yanakuwa hayajasimamiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hii mpaka nipate majibu yale ambayo nimeyauliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami nichangie. Kwanza mimi ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, nijitambulishe halafu vilevile nilikuwa Mkuu wa Chuo cha Ualimu, Bustani, kwa hiyo, ni mdau wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najikita moja kwa moja kwa upande wa vyuo, uchakavu wa miundombinu na *teaching and learning material*. Unakuta Chuo, miundombinu ya maji taka mibovu, vyuo majengo yamezeeka kama Bustani kuna jengo la ghorofa limekataliwa na wataalamu lisitumike, lakini Wizara inaangalia tu. Maombi yanatumwa, lakini katika mgao wa fedha za ukarabati unakuta mpaka zipitie kwa Mkurugenzi wa Mipango, kwa nini Mkurugenzi wa *Teacher Education* asipewe hizo hela moja kwa moja agawe, yeye ndiye anayejua matatizo makubwa ya vyuo vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Diploma hali kadhalika, Vyuo vya *Grade* A hali kadhalika, vina matatizo kweli, vyuo vingine havina hata usafiri kama Mpuguso, Kitangali, Tandala, hivi havina usafiri, wanafunzi wakiugua wanabebwa kwenye machela kupelekwa hospitali. Naomba Wizara itupie jicho vyuo vya aina hiyo. Vyuo vingi

virithiwa, vilitaifishwa kutoka *mission*, vingine vimeanza tangu mwaka 1953 mfano Ndala yaani kinakuwa kama ka-*extended primary school*, hadhi ya chuo hamna, naomba hivi vyuo vifanyiwe ukarabati mkubwa ili na vyenyewe viwe na hadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine kwa upande wa vyuo ni ule ukiritimba ulioko, ndiyo maana Walimu wanafika wanaondoka kwa sababu mambo mengi yanakuwa hayako kwenye chuo. Ametoka kusoma, anaona maisha yakoje, leo nampeleka mahali Mwalimu hakuna hata nyumba, Walimu wapewe nyumba, nyumba zijengwe, Wizara iingilie kati sio vyuo viwe vinabangaiza mara sijui wazazi wachagie michango ndiyo jengo lijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine,  sasa hivi nafasi za ajira za uhakika zimebaki kwenye Vyuo vya Ualimu, watoto wetu wanaomaliza hizi Shule za Kata ndiyo wanapata ajira huko, wanapata mafunzo. Naomba kama wenzangu walivyochangia hizi nafasi zigawiwe kwa usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unaweza ukakuta Kilimajaro imeandikiwa yenyewe haina nafasi, lakini matokeo yake waliomaliza wanapelekwa Kilimajaro. Kwa hiyo, tuzingatie sana na hasa tuangalie zile sehemu ambazo ziko nyuma kitaaluma. Kwa mfano, Iramba Mashariki ina upungufu mkubwa sana wa Walimu. Ziko sekondari zina Walimu wawili tu, sasa Walimu wako wawili watafundisha nini na wataacha nini, ndiyo matokeo yake watoto wanapewa mpira waende kucheza, hilo naomba Wizara ilizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vilevile nachoomba, hii Idara ya Ukaguzi, imeyumba, haijulikani sasa iende wapi, TAMISEMI, Wizarani, liamuliwe moja, kama itapewa nafasi ya kujitegemea basi iwe Kurugenzi inayojitegemea, ipangiwe mafungu. Hawezi akatoka Mkaguzi Wizarani, aanze kumwomba Afisa Elimu nitengenezee gari au naomba mafuta, hakutakuwa na matokeo mazuri, lazima na yeye ataweka na kaubinadamu atakapokaguwa kile chuo. Kwa hiyo, hawa watu wajitegemee kama Kurugenzi zingine, sio kesho wako TAMISEMI, mara wanabaki kule Wizarani, hilo naliomba kabisa atupe majibu hatma ya Wakaguzi ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Walimu, hawa Walimu wanacheleweshewa sana mafao yao ya kupandishwa madaraja na madaraja hawapati kwa wakati. Kawaida, Mwalimu anatakiwa afundishe miaka mitatu, mwaka wa nne apande daraja, lakini matokeo yake hawapandishwi. Hiyo nayo inapunguza morali ya kufundisha. Hawa Walimu wetu kweli wanafanya kazi nzito, tunatakiwa tuwaenzi, walipwe na mafao yao wanayodai na nyumba wapatiwe. Mfano Mkoa wa Singida peke yake wanadai milioni 580,900,000, deni hilo ni kwa Mkoa mmoja, sasa kwa nchi nzima ni vipi? Tuwatendee haki Walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine wafikiriwe kukopeshwa vyombo vya usafiri, wengine wanakaa mbali na shule. Kuna shule zingine wanaingia darasani saa tatu asubuhi kwa sababu ni mbali, wanachelewa kufika na anapokwenda benki anatumia gharama lazima aende akalale ndiyo kesho arudi. Kwa hiyo, nachoomba Walimu wapewe

stahili zao, nao wapewe posho, wakopeshwe vyombo vya usafiri, kwanza kwa mishahara yao wanaweza kabisa kuvilipia hivyo vyombo. Wakopeshwe vyombo na wenyewe wajenge *personality* ya kuwa Mwalimu, sio Mwalimu anaendesha baiskeli anawahi shuleni au anaenda kwenye mshahara, hilo naomba kabisa Serikali ilifikirie. Walimu tuwatoe unyonge, sio Mwalimu anaenda amepauka, akiingia benki anaanza kuambiwa wewe mwanakijiji wa wapi, kumbe ni Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa mafunzo, *syllabus* zisibadilishwe kabla Watendaji yaani Walimu hawajapewa mafunzo. Mfano upande wa Ualimu, *Teaching Practice (BTP)* badala ya kufanyika wiki nane inafanyika kwa wiki nne, jamani huyu mtoto atapataje uzoefu wa kwenda kufundisha kama mafunzo ya vitendo atafanya kwa wiki nne badala ya wiki nane au saa nyingine haendi, anafanya mafunzo mfano hapohapo shuleni kwa shule zinazozunguka. Naomba *Teacher Education* ifikiriwe ili itoe Walimu bora, tuache kuambiwa VODA FASTA, Walimu bora watimize *syllabus* kama inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu fedha ya kwenda kwenye mafunzo ya vitendo ni kidogo, unakuta wanachuo wanaenda na magunia ya unga, maharage, wametoka nayo chuoni, kwa nini wasilipwe hela ya kumtocheleza hizo wiki nane, aende anunue chakula chake huko? Wanaondoka utafikiri wakimbizi na mizigo kibao. Wakifika kule wengine si ajabu wanaibiwa, unakuta wanaanza kumsumbua Mkuu wa Chuo, chakula tulipoteza njiani, mimi naomba Wizara iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda nizungumzie kidogo kuhusu shule za msingi. Shule za msingi liwe jukumu la Serikali, baada ya kujenga, Serikali ifanye *finishing* nzuri, zipendeze, zionekane shule, kama mwanzo tulikuwa tunaimba maua mazuri yapendeza, yanawaita watoto shule, lakini sasa shule ukienda unakuta dirisha ndiyo mlango wa kutokea, kwa kweli shule zetu zina hali ngumu. Mimi naomba Serikali ifuatilie kwa karibu, pesa zitolewe, ziboreshe na wanafunzi watapenda kwenda shuleni, hatutakuwa tena na watoro. Naomba hili liangaliwe sana, shule za msingi zimetelekezwa pamoja na mpango mzuri uliowekwa lakini pesa ni ndogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba nichangie kuhusu *VETA*. *VETA* kweli tumekazana na zitajengwa, kwingine zimejengwa, lakini hawa watoto mkumbuke wanatoka kwenye mazingira magumu, anaondoka hana kifaa chochote, akifika kule anakaa na ujuzi wake. Naomba Serikali iangalie hawa watoto wapewe posho ya kwenda kuanzia maisha, ya kwenda hata kuji-*organise* kwenye vikundi waombe mikopo benki, unavyomwambia tu nenda na hii randa yako, hela za kununua mbao atatoa wapi? Tuwe tunafanya mambo yote kwa mpango wa jumla, sio leo tumempa nani, kesho tuanze kumwita, mkabidhi vyombo vyote hivyo, ndivyo vitawasaidia hata kujiunga katika vikundi. Naomba wafikiriwe wanapomaliza VETA wawe *treated* kama watu wengine, wanaenda kujitegemea, hiyo ni ajira, wawezeshwe vyombo vya kufanyia kazi na pesa ya kwenda kununua zile mbao, atatoa wapi hela ya kwenda kuranda? Naomba vyuo vya *VETA* viimarishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Vyuo vya Wananchi *(FDC)* kama kwenye Jimbo langu ni chuo kizuri na majengo mazuri, lakini hakina vitendea kazi. Sasa bila vitendea kazi, hawa watoto tunaotaka wajitegemee vijijini, wajiajiri, watapata wapi ajira ya aina hiyo? Watakimbilia mijini na huko vijijini watakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba *syllabus* iongezwe maana sielewi, vitu wanavyoenda kujifunza ni vichache mno, kama VETA basi wajifunze hata kutengeneza mashine ndogondogo, *semi- process* za ku-*semi-process* mazao, za kubangua, wajifunze kutengeneza ili watakapojiunga kwenye umoja wao, wanaomba mkopo wanapewa wanaanza kuunda hizo mashine ndogondogo za *semi–processing*. Kwa hiyo, naomba hilo Wizara iangalie kwa makini, kama kweli tunataka kuwainua hao vijana wasije wakarudi tena kwenye lindi la tabia mbaya, tuwatimizie na wenyewe hii ni Serikali yao wapewe mtaji wa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba watumishi wote hususan walimu, wanatoa kodi kubwa sana kwa Serikali, wanayokatwa kwenye mishahara yao. Hiyo kodi ikiwezekana ipunguzwe, hiyo asilimia ipuuzwe, hela yote inaishia kwenye kodi, inakuja inaishia tena kwenye makato mengine, CWT, Bima ya Afya na hiyo kodi ni hela nyingi sana zinakatwa kwenye mishahara yao. Serikali ifanye tena utafiti na Wizara ilisimamie hili kwa upande wa walimu ili liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kutoa shukrani kwa hotuba nzuri iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, haya ni baadhi tu ya maboresho ili waweze kuboresha Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kujikita kabisa kwenye sehemu ya Walimu wenzangu. Walimu ni mgodi ambao unazalisha vitu vya thamani. Sisi sote humu ndani tusingekuwemo kama si Walimu. Katika nchi hii au nchi yoyote hakuwezi kupatikana kiongozi mzuri, mahiri na aliye bora kama si mwalimu. Katika nchi yoyote hatuwezi kupata mhandisi kama si mwalimu. Hatuwezi kupata daktari kama si mwalimu na hatuwezi kupata kitu chochote kizuri bila ya mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla, wanajitahidi sana kupanga mipango mizuri, pamoja na kwamba bado kipaumbele kwa sekta ya elimu ni kidogo. Hatujaipa kipaumbele na kama tungeipa kipaumbele basi kwanza tungemjali mwalimu, mwalimu bado hatujamwangalia ipasavyo. Ili mwalimu awe mwalimu bora na aweze kuzalisha matunda mazuri, anahitaji kusikilizwa madai yake na haki zake za msingi ambazo ni lazima wazipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wetu wangehitaji kupata mafunzo ya mara kwa mara ili kuweza kuongeza taaluma yao na kupata utaalam zaidi unaoendana na wakati siku hadi siku.  Walimu wetu, mwalimu anaweza akaingia kazini akafika miaka 10 hajaweza kupata nafasi ya kupata mafunzo ya ziada.  Tunamtegemea mwalimu huyu atazalisha nini?  Haiwezekani, suala la mwalimu kupata mafunzo ya mara kwa mara ni suala la msingi.  Waswahili wanasema mwalimu ni kama vile kisu.  Kisu kinahitaji kutumika, lakini baada ya muda fulani kinakosa yale makali yake, yaani kinapungua nguvu.  Kwa hiyo ili kiweze kufanya kazi vizuri zaidi lazima ukinoe.  Lazima kinolewe na mwalimu anahitaji kunolewa.   *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu wetu tunamnoa kwa ajili ya kupata mafunzo. Lakini kinachoonekana, mwalimu wetu wa Tanzania na hii ndiyo inayochangia kushuka kwa kiwango cha ufaulu. Mwalimu huyu anapangiwa kwenda kufanya kazi kwenye maeneo ya pembezoni hana motisha yoyote, hana nyongeza yoyote, hana kitu chochote ambacho kinamtia hamu ya kwenda kufanya kazi kule. Hivi tunatarajia kupata elimu iliyo bora?  Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano kama tunasema hatuna fedha za kutosha.  Kuna walimu ambao wanashindwa kuripoti katika maeneo yao ya kazi, mengi sana wanaoajiriwa kila mwaka.  Fedha zinazopotea kwa ajili yao ni nyingi mno.  Fedha hizi zingeweza kutumika kwanza kwa kuwalipa madeni yao Walimu na tukishawalipa madeni yao walimu na wale ambao tumewapangia maeneo ya pembezoni wakapata hamu kwa kuongezewa motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazopotea kama hizo zinafikia shilingi milioni 511 kwa mwaka, wale ambao hawaripoti kazini au wanachelewa kufika katika vituo vyao vya kazi, milioni 511.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu ambao ni watoro, pengine kutokana na matatizo hayo hayo ambayo hawezi kufika katika eneo la kazi alilopangiwa kutokana na sababu nyingi ambazo tumekuwa tukizitaja mara nyingi sana.  Mwalimu hana makazi, mwalimu hana posho inayompa hamu ya kwenda kufanya kazi yake, mwalimu hawezi kupata nyumba nzuri, mwalimu hawezi kupata huduma yoyote ambayo inamwezesha kuishi katika eneo lile analopelekwa.  Walimu wanakuwa watoro, hasa katika shule za msingi ni bilioni 47 kwa mwaka zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoro wa walimu wa sekondari bilioni 117.  Hizo ni jumla ya bilioni 119.  Walimu wana madai ya shilingi bilioni 29.  Tuziangalie 119 na 29 hatujaweza kuwasaidia walimu wetu?   *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo hizo zingeweza kutumika ama kwa kuwapandisha madaraja walimu wetu ama kwa kuwapa motisha ama kwa kuwahakikishia kwa kupata nafasi za kuendelea na kupata nafasi ya kujifunza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha, walimu hawa tunafikia mahala tunawatelekeza. Hatuwezi kuzalisha matunda yaliyo bora kwa staili hii ambayo Watanzania tumekuwa tukiidharau taaluma na tunamdharau mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mwaka 1970 kulianzishwa vituo vya Ualimu vipatavyo 600 kama sikosei. Mwaka 2009/2010, Serikali ilipanga kufundisha, kutoa mafunzo kwa walimu kupitia vituo hivyo wapatao 31,250 kama sijakosea. Walimu waliopata mafunzo hayo katika kipindi hicho cha mwaka 2009/2010 ni 270 tu. Kwa msingi huo ukifanya mahesabu utakuta kila kituo kimetoa mafunzo ya walimu wawili au watatu. Tunaelekea wapi? Tutafika? Tunaweza kufika jamani?

**MBUNGE FULANI:** Hatuwezi kufika.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi ikiwa hali ni hiyo, vituo hivi vya ualimu ikiwa bado wafanyakazi wake wanaendelea kulipwa mishahara ni fedha nyingi ambayo inapotea kila mwaka. Namwomba Mheshimiwa Waziri atusawazishie hili. Lakini vituo hivyo hivyo inaonekana vimetelekezwa, vingine vimekuwa ni magofu kabisa, haviridhishi. Kwa mfano, nimesoma katika makabrasha ya Haki Elimu nimekuta kuna kituo kimoja kilichopo Wilaya ya Rufiji, kinaitwa Bungu, ni gofu, ni gofu kabisa. Kinaweza kulala wadudu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nionyeshe kidogo. Hiki ni Kituo cha Ualimu cha Bungu, Wilaya ya Rufiji. Hili ni gofu Waheshimiwa Wabunge. Hili ni gofu, kituo ambacho kingewasaidia walimu wetu na kuweza kupata mafunzo ya mara kwa mara. Lakini vituo hivyo hivyo maktaba zake haziridhishi, utakuta kuna vitabu viwili au vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu hii ni maktaba ya kituo cha Ualimu cha Kisarawe, lakini haina vitabu. Sasa hatujawasaidia walimu, hatujawasaidia wanafunzi wetu. Taifa ambalo tunaliandaa ni Taifa ambalo tukiondoka sisi linatarajiwa likamate nafasi au kabla ya kuondoka sisi linatarajiwa likamate nafasi, sasa tunaandaa Taifa la aina gani? Naomba sana, naiomba sana Serikali. Naujua uchungu wa Mwalimu na uzito wa kazi yake. Naujua uzito wa kazi ya ualimu na nadhani sote tulio humu ndani tunajua uzito wa kazi ya ualimu jinsi anavyoweza kumkamata mkono mtoto mdogo wa miaka minne au mitano na akamwanzisha mpaka leo tunafikia tunapata kiongozi wa nchi, Rais. Tunapata Mawaziri na tunapatikana sisi Wabunge tuliomo ndani humu. Sote tunatokana na mwalimu na ndiyo maana nimesema mwalimu ni mgodi, kila kitu kinatoka kwa mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumefikia mahali vijana wetu wote lazima waende kwenye *tuition classes.* Ni kutokana na kumdharau mwalimu. Mwalimu hafanyi wajibu wake ipasavyo, kwa sababu kile anachopata kwanza hakitoshelezi, mazingira anayofanyia kazi yake ni magumu kuanzia yeye mwenyewe mpaka mwanafunzi ambaye anakwenda kumpa taaluma. Mwanafunzi anakaa chini, mwanafunzi mwingine anamwangalia mwalimu, mwingine kageuka anacheza mdako na mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu ambaye tutamwezesha vizuri basi ataweza kufanya kazi zake vizuri. Wanafunzi wengine ni wajanja sana. Mwanafunzi anakuja darasani anakuja kum-*challenge* mwalimu, kwa hiyo, kama mwalimu hakuandaliwa vizuri atapigwa chini na mwanafunzi. Kuna wanafunzi wengine ni *very intelligent*. Mimi binafsi mwanafunzi alishawahi kunijaribu darasani, kaja kunijaribu kabisa, kaja na *paper* ya mtihani ambayo alihisi kwamba siwezi kuifanya, akaniletea ya *mathematics,* nikamwambia siwezi kukufahamisha peke yako, lazima na wenzako wapate faida katika hili, nikawafundisha darasani. Hakuniletea tena *paper* hiyo na wala hakuwahi kuniletea tena kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mwalimu wetu hatukuwahi kumwandaa ipasavyo, tutamjengea mazingira magumu. Wanafunzi wake pia watamdharau. Sasa hizi *tuition classes* zitatuletea matatizo wakati mwingine kama mwalimu hatatia nia ya kufundisha vizuri darasani. Lakini tukimwezesha vizuri, akafanya kazi yake kwa kuipenda *tuition classes* zitapungua. Zinachangia kutuharibia watoto wa kike. Watoto wa kike wanaitumia fursa hii vibaya sana, fursa ya *tuition classes* wenzangu wazazi wa watoto wa kike naomba mniambie nani ana uhakika kama mtoto wake akitoka usiku kwenda *tuition classes* ana hakika ya kwenda kuhudhuria darasani? *(Makofi)*

Nani ana uhakika? Hakuna mwenye uhakika. Tunamwomba Mungu tu, tunababahatisha tu kwa sababu tunatafuta ile elimu. Lakini kumbe inawezekana mtoto anakudanganya anakuambia anakwenda kusoma kumbe anakwenda kufanya vitu vingine vya ajabu ajabu. Lakini tukiwawezesha walimu wetu vizuri tukawafanya waipende kazi yao, wengi wetu humu ndani hatukusoma kupitia *tuition classes* au siyo? Tumesoma darasani, vitabu vya kutosha vipo, tunachukua vitabu tunakwenda kufanya mazoezi nyumbani. Leo lazima wewe mzazi umnunulie mtoto kitabu. Ni wazazi wangapi wana uwezo wa kununulia watoto wao vitabu? Ni wangapi, ukiacha Waziri, Mbunge na mtu mwingine ambaye ana uwezo wake mwenyewe. Vijijini wazazi wetu wanao uwezo wa kununua vitabu vya watoto wao vya mazoezi. Mtoto anahitaji kufanya mazoezi ya kusoma. Anahitaji kufanya mazoezi ya *mathematics,* anahitaji kufanya mazoezi ya kila somo kwa kutumia vitabu ambavyo wanavipata kule shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia Serikali yetu tujitahidi sana kuiangalia sekta ya elimu kwa kuipa kipaumbele, bado tuna tatizo la kuiboresha elimu yetu. Nashukuru sana Serikali inajitahidi, lakini bado tuna tatizo, walimu hatujawajali, madarasa hatujaweka vizuri. Haiwezekani mwalimu mmoja afundishe watoto 59, au shule moja ina wanafunzi 283, ina mwalimu mmoja. Iko hiyo ina mwalimu mmoja wanafunzi 283. *How are you going to do? (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Inaathiri.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Wewe mwalimu unakwenda kufundishaje darasa hilo lenye wanafunzi 283 mchana kutwa. Kuna shule zimejengwa, kuna wanafunzi wengi mno madarasa manne, sijui matano anafundisha mwalimu mmoja. Mpaka jana ndiyo nimeambiwa kaingia mwalimu wa pili. Madarasa manne anafundisha mwalimu mmoja, anaingia asubuhi na mchana na jioni tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitoe shukrani kwako kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya sekta zote ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wenyeviti wa Mabaraza ya Vyuo Vikuu kwa hotuba hii nzuri sana, ambayo kwa kweli kimsingi imegusa sehemu zote kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari, vyuo vikuu, Vyuo vya Ualimu pamoja na ufundi. Hata hivyo ningependa kutamka jambo ambalo ni wazi kabisa na kwamba kila mmoja analifahamu kwamba, ili kusudi maendeleo yetu yawe endelevu tunahitaji rasilimali watu na si rasilimali watu tu lakini iwe rasilimali watu wenye ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishi katika dunia ya utandawazi. Tunaishi katika karne ya sayansi na teknolojia ambako vile vile ubunifu unahitajika sana. Sisi Tanzania tumejiunga katika shirikisho mbalimbali za Kimataifa ikiwa ni pamoja na Afrika Mashariki, nchi za *SADC* na nyinginezo. Katika ushirikiano wetu na ushindani wetu ili kusudi tuweze kufanikiwa zaidi tunahitaji rasilimali watu na rasilimali ambayo ina ujuzi wa uhakika. Kwa hiyo, Wizara hii kama alivyozungumza aliyemaliza kwa kweli ndiyo kitovu cha maendeleo yetu na nasema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Iwe ni kipaumbele ambacho daima kisiondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu, katika nchi nyingine, ukiuliza je, kipaumbele chenu ni nini? Wanakwambia elimu, elimu, elimu, elimu mpaka tano. Halafu ndiyo vinafuata vitu vingine. Sisi ni mashahidi na wote tulioko humu ndani ni matokeo ya hilo. Kwa hiyo, nasema kwamba Wizara hii ni muhimu na tuunge mkono. Nasema ili tuwe washindani tunahitaji elimu, elimu nzuri na ujuzi. Tuwe na *skills* tunapoelekea katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kutakuwa na ushindani mwingi hasa baada ya kuruhusu *free movement of labour* kutoka nchi moja mpaka nyingine. Wakitangaza kazi Rwanda ama Tanzania watu watakuwa huru kuja huku na kule. Lakini, je, tuko tayari kufanya hivyo? Nina mfano mmoja, mwaka 2000; tukiwa washiriki katika *Inter University Council of East Africa* ilitangazwa nafasi ya *Executive Secretary* ya hii *Inter University Council of East Africa.* Baada ya kutangazwa na sifa kutolewa, walioomba nafasi hiyo Kenya walikuwa ni watu 36 na wana sifa. Uganda walikuwa tisa na Tanzania tulikuwa watatu. Unaweza kuona *opportunities* hapo nyinyi watatu na wale ambao wako 36 na kama ilivyokuwa matokeo yake ni kwamba mtu wa Kenya alipata nafasi hiyo. Huu ni mfano mmoja tu. Kuna sehemu nyingi sana ambazo kwa kweli tunahitaji kujiendeleza zaidi na kuweka mikakati ili kusudi tuweze kunufaika na umoja ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuisifu sana Serikali kwa utekelezaji mzuri wa Mpango wa MMEM ulioanza mwaka 2001 ambao mpaka sasa imefikisha udahili wa wanafunzi milioni nane na nusu. Ukaingia MMES ambao mpaka sasa umefikisha wanafunzi milioni moja na nusu. Haya ni maendeleo, naona tumetumia

muda mwingi sana wa kubeza maendeleo haya. Nakiri kabisa kwamba, kuna mapungufu, lakini lazima pawepo mahali pa kuanzia. Tusingefanya hivyo, hata hawa wachache ni kwamba, wangekuwa ni jeshi linalozurura mitaani. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tumewarudisha watu madarasani na hatimaye tunaangalia yale mapungufu yaliyopo tufanye nini na juhudi za Serikali ziko wazi kabisa katika hili. Vinginevyo tungekuwa na watu wengi ambao wako mitaani. Vyuo Vikuu hivi sasa tuna wanafunzi 118,000, ukilinganisha na mwaka 2005/2006 tulikuwa na wanafunzi takriban 30,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni maendeleo katika upande wa elimu ya juu. Pamoja na hayo ni kwamba, ukiangalia ile *age group* ama *cohort* ya wanafunzi ambao walitakiwa kujiunga na elimu ya juu au Vyuo Vikuu, Tanzania katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, tuko mwisho! Pamoja na kwamba tumepanua, kuna vyuo binafsi, kuna Chuo Kikuu cha Dodoma kimeongezeka, lakini sisi bado tuko mwisho. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, ni lazima tuongeze juhudi zaidi. Kama walivyosema wengine katika maeneo mbalimbali kuna fursa za kuweza kuanzisha vyuo vingine na nilifurahi kusikia kwamba kutaanzishwa Chuo Kikuu Mpanda, Chuo Kikuu kule Musoma, ili kusudi tuweze kudahili wanafunzi wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafunzo haya upande wa udahili, tumepunguza tatizo la wanafunzi wanaomaliza darasa la saba, kujiunga na kidato cha kwanza. Lakini kutoka kidato cha IV kuingia kidato cha V, sasa hivi ni tatizo kubwa! Ni wachache sana wanapata nafasi kuingia kidato cha V na cha VI na hatimaye kwenye elimu ya juu. Nafikiri ni wakati muafaka sasa kwenye Halmashauri zetu na Wizara, iweke mikakati iliyo wazi ili kusudi tuweze kupanua elimu ya kidato cha V na cha VI ili vijana wengi waweze kujiunga. Lisije likatokea tatizo lililotokea huko nyuma la wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wanashindwa kwenda kidato cha kwanza na wao walikuwa wamefaulu lakini nafasi zilikuwa hakuna. Kwa hiyo, kuna haja ya kupanua katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu ya sekondari, kuna upungufu kama wenzangu wengi walivyozungumza na ningependa kuzungumzia mambo ya sayansi kwamba, tuna upungufu wa maabara na vifaa vyake vya kufundishia, hatuna maktaba na kadhalika. Lakini mengine nafikiri ni kuwa wabunifu mathalan, kwa upande wa maabara ningeshauri Wizara iangalie uwezekano wa sisi wenyewe hapa Tanzania kwa kushirikiana na wengine kuweza kuanza kuzalisha vifaa vya maabara hapa hapa nchini. Haiwezekani tukawa tunaagiza *Bunsen burner* kutoka Kenya! Haiwezekani tukaagiza *Test tubes* kutoka Kenya! Haiwezekani tukaagiza vifaa vidogovidogo vingi kutoka nchi jirani. Nafikiri wakati umefika tuanze kubuni mradi huu na tuna madini mengi, hata *chemicals* nyingi tunaweza tukatengeneza hapa badala ya kutegemea kuagiza nje ili kusudi vijana wetu wapate mafunzo kwa vitendo na waweze kuona, maana kuona ni kuamini, kuliko hali tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna masomo mengine kama baolojia; sidhani kama ni tatizo kiasi hicho, tunao vyura wengi sana, tuna panya, tuna *earth worms,* kweli huko kwenye sekondari hata haya tu hatuyawezi! Tunangojea hata haya tuagize kutoka

nje? Kwa hiyo, nafikiri kwamba, ni wakati muafaka vilevile ubunifu katika shule zetu utumike ili kusudi vijana wetu waweze kupata *practicals* yaani *hands on experience.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mpango wa MMEM na MMES nilikuwa nategemea kwamba, sasa mpango wa MMEJU (Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu na Ufundi), ungekuwa umekamilika ili kusudi kuupokea kutoka MMES, maana huku juu hakuna mpango kamili unaojulikana katika elimu ya juu na elimu ya ufundi. Umetajwa tu ukurasa wa 60 wa Hotuba ya Waziri kwamba, mpango unatayarishwa! Nafikiri kwa sababu MMEM ilianza mwaka 2001 na MMES nafikiri mwaka 2004 na hizi zinakwenda katika awamu ya *II* ya *III*, na huu mpango wa MMEJU bado haujaanza. Nafikiri ni vema Wizara ikaharakisha hili ili kuwe na mpango thabiti unaojulikana kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzuie kidogo juu ya mikopo kwa ajili ya wanafunzi. Nilishtuka sana asubuhi niliposikia hapa kwamba, Bodi ya Mikopo ivunjwe. Ingekuwa kila kitu ambacho kinakuwa na kasoro ni kukivunja ama kukiua, basi tungeua vitu vingi sana! Bodi ya Mikopo, ninavyofahamu, imetusaidia sana tena sana. Bodi ya Mikopo ilianza mwaka 2005 na wale watumishi wa kudumu ambao waliajiriwa mwaka 2006. Chombo chochote kinachoanza, mwanzoni ni dhahiri kwamba kinaweza kuwa na matatizo. Lakini tunaweza kujisahihisha na Bodi hiyo ikaendelea kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Bodi ya Mikopo, mwaka 2005/2006, wanafunzi wa Vyuo Vikuu walikuwa ni takriban 30,000 tu, leo hii wako 118,000! Ni kwa sababu wengi wao wamewezeshwa. Hata kama kuna mapungufu yoyote, lakini kusema kweli wanafunzi wamewezeshwa na Bodi ya Mikopo. Naomba tuwe tayari kuisaidia na tungojee ripoti ambayo Rais, alituma Tume ili kusudi waangalie matatizo na kuweza kuyasahihisha ili iendelee kutoa hiyo mikopo. Lakini tunalaumu, mpaka sasa Bodi ya Mikopo imetoa mikopo kwa wanafunzi kiasi cha bilioni 630. Zilizoiva kwa ajili ya kurudishwa ni bilioni 21, mpaka sasa bilioni nane tayari zimesharudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba baada ya mkopo mwanafunzi akishamaliza, anapewa *grace period* ya mwaka mmoja. Kisha baada ya pale anaendelea kulipa mkopo huo kwa kipindi cha miaka kumi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati alipokuwa anachangia Mheshimiwa Riziki, alionesha picha ya kwamba kuna *Cluster Teacher*

*Resource Centre* ya Bungu, ambayo ina hali mbaya sana kimajengo. Nataka kutoa Taarifa kwamba, katika Wilaya ya Rufiji na mimi nikiwa ni mdau wa elimu katika Wilaya ya Rufiji, nilikuwa Mratibu wa kwanza kabisa wa *DBSPE* ambayo ndio iliyoanzisha hizi *cluster, District Bay Support to Primary Education* na katika kujenga kwetu *cluster* katika Wilaya ya Rufiji, tulijenga *cluster* tatu. Ambapo ya kwanza ilikuwa ni Kituo cha Walimu, Ikwiriri, tukajenga Kituo cha Walimu, Chumbi ambacho nilikuwa Mratibu wa Kituo hicho pamoja na Kituo cha Walimu Luaruke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa alipokuwa anaonesha kwamba kuna *Teacher Resource Centre* ya Bungu, kwa kweli nimeshtuka sana! Hatuna *Teacher Resource Centre* ya Bungu. Kwa hiyo, hiyo picha sio ya Wilaya ya Rufiji, labda ni ya Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nakushukuru, Taarifa ameipokea. Kwa hiyo, tunaendelea. Mheshimiwa Pindi Chana!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii adimu ya kuchangia na mimi leo Wizara hii ya Elimu. Nianze kwa kuipongeza sana Wizara, kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati anayeshughulikia Wizara hii kwa kazi kubwa nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya katika Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, imefanya kazi kubwa sana katika Sekta ya Elimu. Mimi naipongeza sana na niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba elimu ndio urithi wa Taifa lolote. Taifa lolote bila elimu ni changamoto kubwa. Baba wa Taifa, mara tulipopata uhuru alisema tutashirikiana kuondoa maadui watatu; ujinga, maradhi na umaskini. Umaskini, leo hii Tanzania inafikia miaka 50 ya Uhuru, inashuhudia kwamba chakula kinapatikana. Tukienda kwenye maradhi, leo hii miaka 50 ya Uhuru, Tanzania tunashuhudia kwamba, katika upande wa maradhi, tumefikia hatua ya kukinga na sio kutibu. Upande wa elimu, tunashukuru sana nchi yetu kwa miaka 50 ya Uhuru, watoto wenye uwezo wa kwenda shule darasa la kwanza mpaka la saba, elimu ni bure. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kutoa rai, kwa kuwa Serikali yetu imejitoa kutoa elimu bure darasa la kwanza mpaka la saba, bado sisi kama wazazi, sisi kama Watanzania, baadhi ya maeneo haturuhusu watoto hawa, maskini ya Mungu, waende shule! Baadhi yetu sisi tumekuwa tunawatumia watoto wenye umri wa kwenda shule, kama watoto wa kazi za majumbani, wakiwa wana umri wa kwenda darasa la kwanza mpaka la saba na sisi ni mashahidi Serikali imeondoa ada. Hivi huo ujasiri wa kumchukua mtoto afanye kazi zako za nyumbani, kufagia, kudeki au kuchunga wakati watoto wako wewe wanakwenda shule! Hicho kiburi kinatoka wapi Watanzania

wenzangu? Hebu tuangalieni sana! Serikali imefuta ada, tuna shule kila kijiji, sisi tushikamane watoto wetu waende shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mkoa wangu wa Iringa na Njombe, nikiwa kama Mbunge wa Viti Maalum kipindi changu cha pili, sisi tumeweka Sera; Mkoa wa Iringa hatuna watoto wa kazi za majumbani na Mkoa wa Njombe. Niombe na mikoa mingine, umri wa kwenda shule, watoto wetu waende shule. Halafu akimaliza darasa la saba, amejua kusoma, amejua kuandika, ndio tuulizane jamani watoto wa kazi wapo? Anayetaka kuchungiwa ng'ombe, anayetaka kudekiwa nyumbani, lakini angalau apate elimu! Kwa hiyo, niwaombe sana Watanzania wenzangu, tusitumie *exploitation of ignorance* za watoto wetu au jamii zetu ambazo ziko pembezoni mwa Mikoa yetu. Watoto wetu wenye umri wa kwenda shule, waende shule. Serikali imefuta ada za shule za msingi, kwa hiyo, tushikamane na tunapotaka watoto wa kazi wanapatikana waliomaliza darasa la saba, tena wengine wamesomea *VETA*, *cleaning* kabisa, vinaeleweka. Lakini tafadhalini sana tutumie nafasi hii ili watoto wetu wapate elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni shida sana watoto wetu wanakwenda kuchunga ng'ombe! Watoto wetu wanakwenda kufanya kazi za nyumbani, hawalipwi ujira! Wanatumika hovyo! Hadidu za rejea za kazi hazieleweki! Anaambiwa hili usipotaka kulifanya utafukuzwa na vitu kama hivyo! Naomba Watanzania tuwalinde watoto wetu. Elimu ya msingi kwa kweli naipongeza sana pamoja na kwamba kuna changamoto, lakini Serikali yetu imejitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuishauri Serikali kwamba, tumekubaliana kuwe na darasa la awali, kila shule ya msingi iwe na darasa la awali. Maana hawa watoto wetu wakiwa hawajapita elimu ya awali, moja kwa moja miaka sita miaka saba anakwenda *standard one,* ndipo mwalimu aanze kumfundisha kushika peni, kuweka daftari lisigeuke juu chini, anakuwa na kazi kubwa. Changamoto za walimu, Wabunge wengi wamezungumza, nisingependa kuzirudia tena. Kwa hiyo, darasa la awali ni kitu ambacho ni agizo la Serikali, lakini shule zetu nyingi sana hazina darasa la awali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nitumie nafasi hii kusema kwamba katika vijiji vyetu vyote Tanzania tuna shule za msingi. Shule hizi za msingi wakati zinaanzishwa, idadi ya watu ilikuwa ni chache ukilinganisha na idadi ya watu leo hii, mwaka 2011. Kwa hiyo, maeneo mengi sana katika vijiji vyetu, katika mitaa yetu, katika Wilaya zetu, tunapaswa tuwe na shule za msingi za ziada licha ya ile moja ambayo ilikuwepo au ipanuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ambayo nimekuwa nikiifanya hivi karibuni katika Wilaya ya Makete, shule ya Msingi ya Makete, ya Bulongwa, ya Kidegembye, Imagye, Kifanya kule Njombe pamoja na shule ya Msingi ya Manga, Kata ya Madilu, shule ya Msingi ya Ludende, Mavanga, Mbugani, Iwela na Nkomang'ombe, shule hizi zote hazikidhi kwa sababu, watoto ni wengi. Kwa hiyo, niiombe Serikali ifanye *school mapping* ya shule za msingi; ikifanya *school mapping* itaona kwamba, idadi ya watoto

wanaotakiwa kujiunga elimu ya shule ya msingi ni kadhaa na *growth rate,* watoto wanazaliwa kiasi hiki kila mwaka na hivyo itafahamu kwamba inatakiwa iongeze kiasi gani Tanzania nzima. Takwimu hizo ziwe tayari ili tuwape fursa watoto wetu waingie elimu ya shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, suala la *capitation grant* kwa shule za msingi imekuwa kidogo inakwenda polepole. Kwa hiyo, *capitation grant* tunaomba *formula* ieleweke! Ni kiasi gani kila shule ilikuwa inapata, hizi ambazo zinapitia Halmashauri za Wilaya! Lakini pia zifike kwa wakati, zitasaidia sana kuongeza shule za msingi mara moja na kukidhi haja ya watoto wetu kwenda shule. Lakini kuna suala la vyakula mashuleni, maeneo mengine tulikubaliana kutakuwa na *milk feeding program.* Hizi ni taratibu ambazo zilikuwa zimeanzishwa na Serikali na utafiti umefanyika vizuri kabisa. Kwa hiyo, ningeomba sana maeneo haya kwa kweli yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masuala haya, ni muhimu sana tukatafakari jinsi ya kushirikisha *stakeholders* mbalimbali katika elimu ya shule za msingi na elimu ya sekondari. Serikali yetu imefanya vizuri sana lakini bado naomba nikiri kwamba, mzigo kwa Serikali bado ni mkubwa. Serikali hiyo hiyo ijenge madarasa! Serikali hiyo hiyo iwalipe walimu! Serikali hiyo hiyo ijenge maabara! Serikali hiyo hiyo iboreshe mazingira yote! Hebu tutafakari jinsi ya kuingia utaratibu wa *public private partnership.* Wapo wadau mbalimbali ambao wapo tayari kuchangia, tunaweza tukapata takwimu zao nchini na watakuwa tayari kuchangia. Maana hizi ni taasisi ambazo wanapata *profit* na katika *prospectus* zao na *memorandum* zao, wamekiri kwamba asilimia fulani ya faida itakayopatikana zitakuwa ni kwa ajili ya masuala ya *community development.* Kwa hiyo, taasisi hizo zikijulikana tutaona ni namna gani ya kushirikiana nazo katika kuendeleza elimu ya shule za msingi pamoja na elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ningeomba elimu ya sekondari *A – Level*, tukubaliane kila Tarafa iwe na *A – Level.* Kwa hiyo, liwe ni jambo ambalo litaingia kwenye vikao vya *RCC* za kila Mkoa. Tukianza na *A–Level* kila Tarafa, itatusaidia sana. Pamoja na hilo, utaratibu wa *exchange program* na kubadilishana walimu kutoka nchi moja na nchi nyingine, katika shule zetu za sekondari tunashindwaje kuwapata walimu wa *English* tu? Sisi wenyewe humu ndani wapo vijana wetu ambao wamemaliza shule vizuri kabisa, wanaweza kufundisha elimu ya sekondari.  Kwa hiyo, tuangalie hata *English* tu, yaani kuna masomo mengine ni changamoto! Sawa bailoji, *physics, chemistry! Language! English* jamani Watanzania, tutakuwa *translators!* Tuwapate hawa walimu hata wa lugha tu, watatusaidia sana sana. Kwa hiyo, ningeomba sana *exchange program* zitumike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sana *dropouts* za shule zetu. Wanafunzi wengi sana hawamalizi shule, kunakuwa na *dropouts* nyingi. Tatizo ni hawa watoto au sisi ambao ni *above 18 years old?* Kwa nini, tunawatumia hawa watoto? Mtoto hajamaliza shule! Ni mtoto wa Jamhuri ya Muungano! *Dropouts* zinakuwa nyingi! Mimba za mashuleni zimezidi Watanzania! Hebu tuangalie, ni muhimu sana tukakabiliana na hili janga, tukubaliane tunawasaidiaje vijana wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu elimu ya Vyuo Vikuu. Niipongeze sana Serikali na nizidi kuishauri kwamba, tukiweza kutumia utaratibu wa *Loans Board* kupitia benki, benki wao ni *professional* wa namna ya kukopesha hela. Zile hela za mikopo ya Vyuo Vikuu ni za Watanzania wote na kama ni za Watanzania wote ni jukumu kuweka utaratibu kuhakikisha kwamba mtoto akisomeshwa kwa *Loans Board* hela ile inarudi na kuwa hakuna masuala ya *lobbying* kwenye mabenki, hakuna *lobbying* na nini. Kwa hiyo, zingepitia kwenye benki ambazo ni *one hundred percent own by Tanzania Government*, tunazo benki zetu za Kitanzania na benki zingine tuzifanyie *scrutinization* mikopo ipitie benki. Lakini pia vyeti vya wale ambao ni *Loans Board beneficially* viwekewe alama, akipata ajira yule mwajiri wake anajua huyu ni *Loans Board beneficially*, kwa hiyo katika mshahara wake kiwango fulani inabidi kirudi Serikalini, ili kesho na kesho kutwa na vijana wengine wanufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu jioni ya leo. Kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Shinyanga kwa kunitia moyo wakati wote na kunitumia meseji za ushauri katika mambo muhimu ya kuchangia Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Waziri wa Elimu kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya bajeti na nimshukuru zaidi kwa kukubali ombi langu la kuweka kipaumbele katika kuboresha Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika cha Moshi, *campus* ya Kizumbi Shinyanga na sasa zaidi ya wanafunzi 4000 watapata nafasi ya kujiunga na masomo ya stashahada pamoja na vyeti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii pia kuwajulisha wananchi wa Shinyanga, ni wakati muafaka sasa kutumia nafasi hiyo waweze kusoma na kupata elimu ya Chuo katika Chuo cha Kizumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza zaidi katika elimu ya juu, nilikuwa napitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, changamoto tulizonazo sasa hivi katika elimu ya juu, idadi ya wanafunzi inakwenda inaongezeka kila siku. Ukiangalia *speed* ya kuongeza idadi ya wanafunzi na miundombinu ya kupata fedha kwa ajili ya ku-*finance* wanafunzi hawa haionekani katika hotuba ya Waziri. Niombe tu kutoa ushauri kwa Waziri kwamba ule mpango sasa wa kuanzisha *education levy* uharakishwe haraka. Ukiangalia takwimu mwaka uliopita tulitumia zaidi ya bilioni 237 katika kulipia mikopo ya elimu ya juu na kipindi kile wanafunzi walikuwa ni wachache. Sasa hivi takwimu zinatuonyesha wanafunzi wamefikia 109,092 wanaopata mikopo na kwenye bajeti inaonyesha watatumia zaidi ya shilingi bilioni 323 kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambao ni asilimia 49 ya bajeti nzima ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu Elimu ya Juu inabeba nusu, wastani wa nusu ya bajeti yote ya Wizara na kuicha idara ya sekondari, shule za msingi ikiwa haina kitu kabisa. Sote tunatambua ili upate elimu bora ya juu ni lazima uwe na

msingi mzuri chini. Ukienda elimu ya juu ukiwa na msingi mbovu ndiyo tutakuwa tuna kazi ya kuzalisha *degree* ambazo hazina uwezo. Ni makusudio yangu kabisa kwamba *level* zote za elimu zina umuhimu katika Taifa letu, *level* ya cheti ina umuhimu wake, *level* ya *diploma* ina umuhimu wake, *level* ya *diploma* ya juu ina umuhimu wake na *level* ya *degree* ina umuhimu wake. Hivyo, Serikali lazima ianze kuangalia vigezo vya wanafunzi kupata elimu ya juu kwa maana ya *degree,* lazima kigezo cha taaluma kiwe ndiyo kigezo namba moja. Leo hii tuna vyuo vingi na imekuwa kama *is like milling of degree, tuna degree* nyingi lakini ukienda kwenye *content* na uwezo wa wanafunzi wale kupokea yale masomo unakuta hautoshi. Kwa hiyo, ni vema Serikali izingatie kabisa elimu ya stashahada ina umuhimu wake na elimu za msingi, sekondari na elimu zingine za kati zina umuhimu mzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu hapa za Wizara, elimu ya msingi inachukua karibu asilimia 72 ya *enrolment* ya wanafunzi wote, elimu ya sekondari *O-level* inachukua asilimia 15, elimu ya sekondari *High School* inachukua asilimia moja, *Teachers College* hapa takwimu inaonyesha ni sifuri *enrolment*, elimu ya vyuo *VETA, Vocation Education* pamoja na elimu ya juu ya Vyuo Vikuu ni asilimia moja moja. Unaona kabisa elimu ya msingi inachukua zaidi ya asilimia 72 ya mzigo wa Wizara ya Elimu, lakini fedha zinazoelekezwa kule ni kidogo sana hazitoshi. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie namna nyingine ya kutafuta fedha hasa kwa kuanzisha hii *education levy*. Hii itasaidia huu mzigo kuwa himilivu siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia *trend* ya ongezeko la wanafunzi elimu ya juu naona kabisa muda si mrefu Mheshimiwa Waziri atakuwa kwenye kiti moto kwa sababu hatoweza kumudu kugharamia wanafunzi wote wanaohitaji mikopo. Pesa ambazo tunatumia sasa hivi ni nyingi zaidi na leo wanafunzi 100,000, pesa ya chakula ya kila siku unatumia zaidi ya bilioni moja kwa siku, sasa wanafunzi wanasoma karibu miezi minane, wastani wa siku 240. Maana yake bilioni 240 zitahitajika kwa ajili ya chakula tu kama utampa kila mwanafunzi 10,000, hapo hujagusa *accommodation*, kwa hiyo, ni mzigo mkubwa, Serikali lazima iangalie namna itakavyobili hali hii inayokuja mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi Jimboni kwangu nizungumzie Chuo cha *Shycom*, miaka ya nyuma, *Shycom* ilikuwa sekondari na Chuo cha Uhasibu kwa ngazi ya vyeti na *Diploma* na wahasibu wengi wa nchi hii wamepita *Shycom*, lakini sielewi kigezo gani kilitumika na Serikali kubadilisha matumizi ya chuo kile na kukifanya kuwa Chuo cha Ualimu na bila kutafuta *High School* nyingi mbadala. Leo tunapoongea Shinyanga Manispaa Makao Makuu ya Mkoa haina *high school* hata moja na Serikali ilipokuwa inafanya maamuzi yale ilitakiwa izingatie mbadala, inatoa *Shycom* kuwa Chuo, je, wanafunzi wanaohitimu kidato cha tano Shinyanga wanakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wilaya ya Shinyanga Mjini Manispaa, ukijumlisha Kishapu na Shinyanga Vijijini ina wastani wa wanafunzi 1700, wanahitimu elimu ya sekondari lakini hawana pa kwenda. Waliomba Serikali na nitaomba Mheshimiwa Waziri, nakushukuru umenisaidia kwenye suala la Chuo cha Kizumbi, lakini naomba na hili unipe majibu, wananchi wa Shinyanga wanaitaka Serikali irudishe shule ya *Shycom*

kuwa *high school,* ili vijana wote wa pale wapate nafasi ya kusoma elimu ya sekondari ya juu. Kile Chuo cha Ualimu hatukikatai, lakini tuna majengo ya chuo cha *campus* ya Kizumbi, Chuo cha Ushirika, anzisheni kitivo cha elimu pale ili wanafunzi wapate fursa ya kusoma ualimu, yapo majengo mengi, uwanja ni mkubwa, mnaweza mkafanya *extension* na mkaanzisha Kitivo cha Elimu katika Chuo cha Kizumbi ili wanafunzi wale wanaosoma ualimu waweze kupata fursa ya kusoma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la madai ya walimu, hili limekuwa ni tatizo sugu, kwenye Jimbo langu la Shinyanga walimu wangu wanadai, wamepandishwa madaraja lakini stahili zao hawalipwi, naiomba Serikali ichukulie kwa uzito mkubwa ilipe madai yote ya walimu, walimu waliohamishwa walipwe madai yao tusiwakope walimu. Lakini pia wapo walimu wanaojitolea, Wizara ya Elimu inajua ina mpango wa wale walimu wanaojitolea kufundisha sehemu zenye shule zilizo na mapungufu, walimu wale hawalipwi pesa zao na leo tunalalamika kwamba walimu hawatoshelezi, lakini ukiangalia wako watu wanajitolea kufundisha lakini hawalipwi, wako walimu wengine wamemaliza vyuo, hawajapata ajira rasmi mpaka sasa hivi na hawana uhakika kama wataajiriwa. Naomba Serikali ilipe umuhimu mzito suala hili ili kuhakikisha walimu wote waliomaliza chuo na ambao wanastahili kuajiriwa wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la maabara ni la muhimu sana, kwenye mpango wa MMEM na MMES tumezungumzia sana ujenzi wa madarasa lakini sasa hivi tuweke kipaumbele chetu kwenye kujenga maabara kwa ajili ya wanafunzi. Ameeleza Profesa Msola hapa kweli ukiwa unasoma sayansi ni lazima ufanye sayansi kwa vitendo, sayansi ya nadharia tutazalisha wataalam ambao atakosea kuchoma sindano, atakosea kuchang'anya kemikali kwa sababu ya msingi mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweke uzito mkubwa katika Wizara hii kuhakikisha kwamba maabara zinajengwa, hata maabara moja ambazo shule za Kata zitashirikiana, siyo lazima kuanza na kujenga maabara katika kila Kata  lakini tunaweza tukachagua shule moja tukajenga maabara iliyokamilika na tukashawishi shule zingine zishirikiane kwenda kufanya mafunzo ya vitendo katika maabara moja. Lakini nyumba za walimu pia ni jambo la msingi sana, wengi wamechangia hapa wamesema walimu wengi wameshindwa kwenda kwenye maeneo ambayo wamepangiwa kwa sababu ya mazingira mabovu.  Naomba Wizara na Waziri, ahakikishe kwamba maeneo magumu kuishi yajengewe nyumba haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda unaniishia nimwombe Waziri anipe majibu na atoe ufafanuzi, wananchi wengi wanashindwa kuelewa unaposema elimu ya msingi inatolewa bure, lakini wanaendelea kuchangishwa pesa nyingi, yapo maeneo pale Shinyanga Ndala, Masekelo, na Kizumbi, wananchi wanauliza je, hii michango kiwango ni kiasi gani? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi hapa ili ieleweke kwa Watanzania wote kwa sababu Kamati za shule zimeshindwa kusimamia hili na inaonekana walimu wakuu ama wakuu wa shule wanafukuza wanafunzi kwa kukosa michango lakini sera ya Serikali wanafunzi wanapaswa wasome bure na mwanafunzi anaposhindwa kulipa mchango siyo kosa lake, kosa hilo ni la mzazi, mwanafunzi aachwe asome asirudishwe nyumba na Serikali lazima itoe maagizo walimu wakuu wasifukuze

wanafunzi shule kwa kushindwa kuchangia michango. Hakuna mwanafunzi anayejisomesha, wanafunzi wote wanasomeshwa na wazazi wao, kwa hiyo, mwenye wajibu wa kulipa ni mzazi. Kwa hiyo, Kamati za shule, walimu wakuu watambue kabisa wa kwenda kuwakaba ni wazazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja*. (Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana kwa nchi yetu. Lakini kabla sijakwenda kwenye hoja, naomba tu niwape taarifa wananchi wa Jimbo langu la Singida Mashariki ambao pengine wananisikiliza kipindi hiki, kwamba, fedha za maendeleo ya Jimbo zimeshatoka na kama ambavyo nimekuwa nawaahidi, nusu ya hizo fedha zitatumika kusomesha watoto wetu. Kwa hiyo, kwa wote wale ambao wamefaulu kidato cha nne, wanakwenda kidato cha tano, wanakwenda kwenye vyuo, wako vyuoni, mwaka huu tutatenga nusu ya hizo fedha kwa ajili ya kuwasaidia gharama za masomo. Maendeleo lazima yanapatikana tukisomesha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba basi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mafunzo na Ufundi. Miaka 20 iliyopita, kabla sijakwenda chuo kikuuu kusoma sheria nilikuwa mwalimu na leo naomba nizungumze habari ya walimu. Hotuba ndefu ya Mheshimiwa Waziri imeeleza pamoja na mambo mengi mengine imeeleza kwamba…

**TAARIFA**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Msemaji anayezungumza hapa ni msemaji ambaye namheshimu sana, mwanasheria mwenzangu na Wakili wa kujitegemea kama mimi. Sasa nimemsikia akisema kwamba fedha ya Mfuko wa Jimbo ambayo amepelekewa Jimboni kwake anakusudia kusomesha wanafunzi. Nataka nimpe taarifa tu kwa faida yake …

**MWENYEKITI**: *Order in the House please.*

**MHE GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa na pengine Waheshimiwa Wabunge wengine watachukua taarifa hii kwa makini kwamba, tuliipitisha Sheria ya Mfuko wa Jimbo hapa. Sheria ya Mfuko wa Jimbo inaeleza kinagaubaga ni shughuli gani ambazo fedha hizo zitafanya. (*Makofi)*

Sheria hiyo haielekezi hata kidogo fedha hiyo kutumika kwa misingi ya kulipia ada za wanafunzi, nataka nimpe taarifa msomi mwenzangu, Wakili mwenzangu asije akateleza na pengine akapata faini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu taarifa imetolewa una hiyari kukubali au kukataa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda niseme tu kwamba, nafahamu sheria inasema nini na pengine Mheshimiwa aliyetoa taarifa asiwe na wasiwasi, nafahamu sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema kwamba, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, moja ya mambo ambayo Mheshimiwa Waziri amesema ni changamoto linalokabili Wizara yake ni uhaba wa nyumba za walimu, wakufunzi na wahadhiri. Uhaba wa nyumba za walimu wetu na ni ukweli kwamba walimu wetu wanaishi katika mazingira duni sana, walimu wetu wanaishi katika nyumba za ajabu sana, wanaishi katika mazingira ambayo hayaendani na mzigo mkubwa ambao tumewakabidhi wa kutusomeshea watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitu ambacho sikielewi na pengine nitaomba Mheshimiwa Waziri alieleze Taifa na Bunge hili ni haya yafutayo: Kwamba katika takwimu zilizoambatana na hotuba ya Waziri Mkuu katika Bunge hili mwaka huu inaonyesha kwamba katika mwaka 2009/2010, shilingi zaidi ya bilioni nne, zilizotengwa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu hazikutumika. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majedwali haya yaliyoambatana na hotuba ya Waziri Mkuu yanaonyesha hicho, shilingi zaidi ya bilioni nne, kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu hazikutumika hadi kufikia mwezi Juni, 2010. Katika sh. 6,218,000,000/= zilizotengwa kwa ajili hiyo hiyo kwa mwaka 2010/2011, sh. 2,333,000,000/= au asilimia 37 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu hazikutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili zaidi ya sh. 6,442,000,000/= zilizotengwa kwa ajili ya kujenga nyumba za walimu nchi hii hazikutumika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini walimu wetu wanaishi katika nyumba duni, kwa nini tuna changamoto ya uhaba wa nyumba za walimu wakati fedha zinazotengwa na Bunge hili ili walimu wetu wajengewe nyumba hazitumiki, au Mheshimiwa Waziri atuambie kama takwimu za Waziri Mkuu ni za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka huu peke yake madai ya walimu ya mishahara ambayo haijalipwa pamoja na madai mengine ni zaidi ya sh. 1,269,000,000/= na ushee. Waziri amesema kwamba, kwa sasa hivi Wizara yake inashughulikia madai ya watumishi 844 ambayo yana thamani ya shilingi milioni 923 na baki. Sasa wakati walimu wetu hawalipwi mishahara yao na posho wanazostahili, kufuatana na majedwali ya Waziri Mkuu mwaka 2008/2009, sh. 12,676,000,000/= zilizotolewa kwa ajili ya uendeshaji wa shule kwa mwaka huo hazikutumika.

Vilevile kufuatana na takwimu hizo hizo ziko kwenye majedwali ya Waziri Mkuu ya mwaka jana, takwimu za mwaka jana zinaonyesha kwamba shilingi bilioni 21, milioni 396 na baki ambazo zilitolewa kwa ajili ya uendeshaji wa shule kwa mwaka 2009/2010 nazo hazikutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu zaidi katika fedha ambazo zilitolewa kwa ajili ya kuendesha shule kwa mwaka jana yaani mwaka wa fedha 2010/2011 jumla ya shilingi bilioni 33 na milioni 590, shilingi bilioni 10 na milioni 637 au 32% ya hizo fedha hazikutumika. Kwa hiyo, wakati walimu wetu hawalipwi mishahara, hawajengewi nyumba, hawalipwi posho na wanahangika, Bunge hili Tukufu linatenga fedha kwa ajili ya walimu na watoto wetu hazitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa fedha ambazo takwimu za Serikali zinaonyesha hazikutumika kwa mwaka 2010/2011 za shilingi bilioni 10, milioni 600 kama 11% ya fedha ambayo haikutumika zingetumika, madeni ya walimu ambayo leo bado hayajalipwa yangeshalipwa yote, walimu wetu wasingekuwa na madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zote maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba walimu wetu wanahangaika siyo kwa sababu hakuna fedha, walimu hawalipwi mishahara na posho zao siyo kwa sababu hakuna fedha, wanaishi katika nyumba duni si kwa sababu hakuna fedha ni kwa sababu fedha ambazo zinatengwa na Bunge hili hazitumiki kwa malengo yaliyoelekezwa na Bunge hili. Walimu wetu ni maskini siyo kwa sababu hakuna fedha, ni kwa sababu fedha zinazotengwa hazitumiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimepitia mafungu yanayopendekezwa na Wizara mwaka huu, na katika fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya walimu wa shule za sekondari na sShule za msingi kwa mwaka huu kwenye *book* hili ni shilingi bilioni moja, milioni 148. Posho ni shilingi milioni 138, ukichanganya posho na mishahara inayopendekezwa kulipa walimu wetu mwaka huu ni shilingi bilioni moja, milioni 287.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu hatutaweza kulipa mishahara ambayo haijalipwa mpaka sasa hivi, hatutaweza kulipa posho ambazo hazijalipwa mpaka sasa hivi na tutakuwa tunazalisha madeni mengine na walimu wetu wataendelea kuishi katika umaskini iwapo Serikali na Wizara haitatenga fedha za kutosha na kama nilivyoonyesha fedha hizo zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, kwa sababu sina muda, hatuwezi tukawa tunaimba miaka 50 ya Uhuru  kwamba umaskini, ujinga na maradhi ndiyo maadui wetu, kama tuko *serious* ni lazima tuhakikishe walimu wetu wanalipwa kwa fedha hizi ambazo Bunge hili limekuwa linatenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho kabisa ni elimu ya juu, mimi niliingia Chuo Kikuu mwaka 1991 badala ya mwaka 1990 na sikuingia mwaka 1990 kwa sababu wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waligoma mwaka 1989 na waligoma kwa

sababu mahitaji yao yalikuwa hayasikilizwi. Tangu mwaka 1989 wanafunzi wamegoma kila mwaka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu nakushukuru sana.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu na niseme tangu mwanzo kwamba mimi ni mwalimu kwa hiyo, kuna baadhi ya mambo ninayafahamu ila niseme tu mengine nashukuru Wizara inaendelea kuyaboresha kuliko hata wakati ambapo mimi nilikuwa mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litaambatana na pongezi kwa Wizara, Waziri na Naibu Waziri na timu nzima kwa kutuandalia angalau maelezo mengi tu yaliyofafanuliwa vizuri lakini kama kawaida basi niwaombee utekelezaji wa haya mliyoyaamua na kujipangia kwamba ndiyo mtayatekeleza kwa mwaka huu wa 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa sababu muda unaweza kuwa mdogo kusema chochote kuhusu elimu kwa watoto wenye ulemavu, wanavyuo wenye ulemavu na walimu wenye ulemavu. Hiyo ndiyo sehemu yangu ambayo kidogo nina ufahamu nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi nimezungumza lakini nitaendelea kuzungumza tu kwa sababu najua kuna siku neema itadondoka. Sisi wenye ulemavu tunahitaji elimu kwa sababu kwa ujumla elimu ni ufunguo wa maisha. Vilevile kwa wenye ulemavu elimu ndiyo ukombozi kabisa kama kweli unaipata. Mwenzenu mimi hapa nilipo ni shule tu ndiyo imeniweka hapa kwani mngenifahamu? Ni shule niliyoipata kwa shida sana tu, lakini katika kupata elimu hii watu wenye ulemavu wa aina zote tuna changamoto nyingi sana. *(Makofi)*

Kwanza mazingira ya shuleni kwenyewe, mazingira ya majengo ya shuleni, mazingira ya mihadhara, nimefika mpaka Chuo Kikuu kwenye mihadhara kule na ninaomba hiyo kwani haihitaji fedha za nje ni Serikali kuamua, wahandisi wa majengo na wa mazingira kuweka haya mambo rahisi kwa wanachuo, wanafunzi, watoto wa chekechea wenye ulemavu wa aina yoyote ile wakifika katika maeneo hayo na wao wakapata bahati ya kupata elimu ambayo wanaweza kuipata, hili halihitaji fedha nyingi na mimi nimechoka kulisema. Lakini inabidi niendeleee kulisemea kama mimi nilipata shida ya kuning’inia kwenye ngazi za Chuo Kikuu na kadhalika wanangu na wajukuu waweze kusema tulikuwa na bibi aliyetusemea kwa mabadiliko chanya, ndiyo ninayoyataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaendana na uhaba wa vitendea kazi na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Ninashukuru katika *level* ya Vyuo Vikuu angalau kuna Vyuo Vikuu vitatu vimeshaanza kuelewa inapaswa kuwasaidia vipi wanachuo wenye ulemavu katika vyuo vyake. Lakini kwenye shule za msingi na sekondari bado matatizo hayo ni makubwa. Mpaka sasa hivi hakuna vitabu vya kutosha vya nukta nundu sijui wenzangu mnajua? Hivi ni kwa watoto wenye ulemavu wa kuona, hawezi kusoma bila hivyo vifaa. Zamani walikuwa wanatumia *tape recorder* wanasikiliza lakini sasa hivi hata sivioni, sijui na teknolojia inavyokwenda, hivi hawa tunawasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi kuna matatizo kwamba hakuna maandalizi ya nyenzo nzuri za kuwafundishia watoto wenye uono hafifu hususani *albino*, wanahitaji *large print* sijui zinaandaliwa namna gani. Hapa ndiyo nataka kuuliza hivi kile kitengo cha Uhuru Mchanganyiko ambacho mashine yake iko pale na wataalamu wako wa kuandaa nyenzo hizi bado kweli kile kituo kinafanya kazi kikamilifu? Maana nilisikia ni watu binafsi tena na sikatai *PPP* tumeipitisha lakini kwa nini Uhuru Mchanganyiko ambacho ni kituo cha Serikali kisitumike *full* ili kusaidia kupunguza gharama? Hapo nitataka kufahamu baadaye mambo yanakwendaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali hata na wanavyuo, mimi hapa nachukua *section* zote tangu shule za awali hata Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundi na *VETA.* Bado kuna haja ya kuwa na idadi ya kutosha ya walimu waliosomea taaluma ya elimu maalum, si kila mwalimu anaweza kumudu kumhudumia mtoto mwenye ulemavu wa aina fulani, kuna chuo sasa hivi *so far* cha Patandi tu ndicho kinachoandaa.

Lakini nishukuru Kanisa la KKKT kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Sekuco kwa madhumuni hayo tu ingawa sasa wanaongeza *degree* nyingine lakini *initial* ilikuwa ni *special education,* nashukuru sana kwani Serikali kwa muda mrefu imetega sana hicho kipengele lakini Kanisa limetusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wengi wanaokwenda Patandi wanakwenda tu kujiendeleza baada ya kuwa mwalimu wa kitu fulani, wakishapata elimu wakirudi Maafisa Elimu wa Wilaya katika Halmashauri hawawapangi katika maeneo ambayo walipaswa kwenda kufundisha, wanabadilishwa kwa hiyo ule upungufu unaendelea kuwepo, sasa lengo ni nini? Wenye ulemavu tubaki bila kusoma au maana yake ni nini? Mheshimiwa Waziri mkishirikiana na TAMISEMI hilo bado ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ili kupunguza upungufu wa walimu ambao unaletwa kwa njia nyingine, mimi nashauri kwa walimu tarajali wote hasa wa shule za msingi na sekondari wapewe dozi ya *special education* ili wanapokwenda kufundisha waweze kukidhi haja na kusaidia halafu tuwangoje na wale wengine ambao wanakwenda kupata *specialisation* ya hiki kitu. *Otherwise* watoto wanakuwa hawana msaada wa kutosha tena ni wale wachache wanaomudu kwenda hata shuleni kwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nashauri wote wanaosomea ualimu wa shule za msingi na sekondari wafundishwe lugha za alama kwa sababu ndiyo lugha pekee ambayo watoto viziwi wanamudu kuzifundisha au kufundishwa nayo. Mwanafunzi anaweza akakuangalia unavyofanya vitendo, utaalamu huo kila mwalimu angalau aujue ili aweze kusaidia watoto kwa sababu hawezi kujua wanakumbana na nani darasani na ninafahamu Serikali inashauri tuwe na elimu jumuishi kwamba darasani humo humo unaweza ukamkuta kiziwi yumo humo, utamsaidiaje? Vinginevyo mwalimu utamaliza kipindi unasema watoto wameelewa sembuse madarasa yenyewe ndiyo hayo, darasa la watoto 100 na viziwi wawili darasani mwalimu utamudu vipi kumsaidia au kuwasaidia hawa wanafunzi wawili ambao hawatakuwa wanaelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba elimu maalumu iko chini ya Ofisi ya Kamisheni. Kama ukaguzi ulivyo, ninaomba *special education* iundiwe Idara yake kabisa. Inashindwa kujitanua na kuchanganua sawasawa changamoto hizi kwa sababu pia ofisi ile ina shughuli nyingi. Ninaomba iundiwe Idara yake ili mambo yafanyike kikamilifu.

Pamoja na kuundiwa Idara yake ninaomba katika Halmashauri zetu tuwe na Maafisa Elimu Maalum, niliomba hilo. Nilishauri na ninashukuru Halmashauri nyingine zinaajiri lakini Halmashauri nyingine bado, nadhani ni kazi ya Wizara kuhakikisha kwamba kila Halmashauri mkishirikiana na TAMISEMI watu hawa wapo ili yale yanayohusu elimu maalum kwa watoto wenye ulemavu katika Halmashauri zao wao ndiyo wanaweza kwa sababu wana utaalamu, wanaweza kusaidia jinsi ya kuchanganua masuala mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kwa sababu hawa Maafisa Elimu Maalum hawapo katika Halmashauri zetu, kunakuwa na fedha zinatoka Serikalini za kusaidia vitengo vya watoto wenye ulemavu kwa chakula na mambo madogo madogo. Lakini fedha hizi hazifiki kwa wakati kiasi kwamba katika maeneo mengine utakuta walimu wanachangishana fedha ili wanunue unga wa uji kwa watoto wenye ulemavu wa akili ambao hawaendi shule bila uji, ni shida tu. Sasa kama wenzangu walivyokwishasema hivi tunamfanyaje mwalimu huyu? Yeye ndiye daktari, ndiye anabeba watoto kwa kweli kazi ya ualimu siyo dhambi jamani kwa sababu kuna wengine walioandikiwa kuwa walimu duniani hapa, alipozaliwa tu akaambiwa na Mungu kwamba wewe utakwenda kuelimisha wengine. Sasa tunapowapa mizigo mingine inakuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwani imeanzisha *system* ya wanafunzi kusoma kwa *TEHAMA*. Mimi nilikuwa nauliza kwa watoto wasioona hapa inakuwaje? Maana *TEHAMA* sijui ni kompyuta au kompyuta za kusema? Naomba baadaye mtanisaidia hilo ili isiwe tu kwamba wanafaidika wachache na wenye ulemavu hawafaidiki na hizi teknolojia mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajua kwa sababu ukichukulia kimahesabu watoto wenye ulemavu ni wachache sana wanaoweza kusoma shule za awali mpaka Vyuo Vikuu. Naendelea kusema kwamba nchi ina pesa, watoto wenye ulemavu wasomeshwe bure kwa *levels* zote yaani bure kabisa. Wazazi wanahangaika nao hebu

muwape nafasi, Serikali sasa inawasaidia bure bila hata senti tano na hakuna kulimpa mkopo. Ninaomba iwe hivyo kwani ni Mungu amewapa huo mzigo tuwasaidie basi waubebe kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu walimu wanaohangaika na wanafunzi na wanachuo wenye ulemavu wapewe posho ya mazingira magumu. Wanawabeba watoto na walimu wengine wana *lighter job* lakini walimu wa watoto wenye ulemavu mpaka wanapomaliza vipindi wanakuwa wameshachoka na hawana budi kwa sababu ndiyo kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja lakini mengine nitayauliza baadaye. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa na sasa namuita Mheshimiwa Henry Shekifu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda sana kukushukuru na kuishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na watendaji wote mimi nawapongeza sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliye na macho haambiwi tazama na aliye na masikio ukimwambia sikiliza basi ana upungufu. Hakuna asiyekiri humu ndani kwamba wote ni kwa utendaji mzuri wa Serikali yetu,kuanzia mwaka 1961 tumeona Mapinduzi makubwa sana katika elimu. Ukizungumzia idadi ya wanafunzi waliopo Chuo Kikuu 100,000 na zaidi kwa leo huwezi hata siku moja ukalinganisha na pale tulipotoka. Mtu asiyepongeza juhudi hizi basi ana tatizo kubwa katika *mind set* yake. Sasa mimi nisingependa sana nijielekeze kama hapo bali nitajielekeza katika mambo ya msingi ambayo kwa ajili ya muda nitajielekeza zaidi kwenye Jimbo langu pengine baadaye nitachangia yale ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na uhaba wa walimu. Tunalo tatizo kubwa katika Wilaya ya Lushoto, walimu ni wachache na tatizo kubwa ni kwamba katika Mkoa wa Tanga wanafunzi wengi wapo Wilaya ya Lushoto. Sasa sina uhakika wa *ratio* ya wanafunzi kwa mwalimu inavyopangwa pengine Waziri baadaye atusaidie. Lakini mimi nieleze tu katika shule za msingi mwaka 2009 tulipangiwa kupewa walimu kama 136, kwa bahati mbaya walimu wale wakafutiwa usajili. Tukaahidiwa kuletewa walimu lakini mpaka leo ninavyozungumza si zaidi ya walimu 20 walioripoti kwa kufidiwa wale ambao walifutiwa usajili. Sasa naomba Waziri aliangalie hili ni pengo kubwa kwa kweli tunahitaji msaada wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la uimarishaji wa elimu yenyewe. Wabunge wengi wamezungumzia suala la kuzingatia mafanikio tuliyopata na sasa tuhakikishe kwamba yale mafanikio tunayalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la ukaguzi. Bila ukaguzi katika shule ni kama nyumba isiyo na mlango, maana huwezi kulinda maslahi, kanuni na taratibu za kufundisha kama huna mtu anayefuatilia nyuma na kuona kinachoendelea. Mimi nashauri sana Idara ya Ukaguzi kwa kweli iwe ni wakala badala ya kuwa ni Idara katika Wizara. Ifanye kazi yake kama *agency* ili ipewe majukumu na ipimwe kama *agency* na mapato yake yajulikane. Kama vile tunavyompa *CAG* fedha ili afanye kazi yake ya ukaguzi, Idara ya Ukaguzi mashuleninayo ipewe fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata katika kitabu cha Waziri hapa kwenye *schedule* ya mwisho hii kwenye ukaguzi wa shule. Shule za Awali zimekaguliwa kwa asilimia 45, halafu Shule/Vitengo vya Elimu Maalum asilimia 28.6 na huko ndiyo kwa kweli tunahitaji wakaguliwe. Vituo vya Elimu Maalum asilimia 29.9 na ukichukua wastani wa vitengo hivi ni asilimia 40.8 tu ya utendaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni wazi na kweli kwamba mafanikio tuliyoyapata kama hayatalindwa shule zilizoanzishwa za sekondari za kata na shule za msingi hazitafanya vizuri. Mimi nashauri sana Idara hii ya Ukaguzi kwa kweli ifanywe Idara Maalum kama vilevile tunavyowapa wale wengine walioko katika maeneo ya ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo eneo la Vyuo Vikuu hasa Chuo Kikuu Huria. Nitangaze maslahi niliyonayo katika Chuo Kikuu Huria; mimi ni Mjumbe wa Baraza, mmeniteua hapa kuwawakilisha. Ukiangalia katika maelezo ya Waziri kuhusu Chuo Kikuu Huria, maeneo mengi yanatamka kwamba Chuo Kikuu Huria kitaendelezwa kwa kujenga nyumba na maeneo ya kusomea. Lakini ninavyoelewa juzi juzi hapa tulikuwa na Kikao cha Baraza, hawakupewa hela za maendeleo. Majukumu yaliyotajwa hapa yatatekelezwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaamini kwa akili zangu kwamba Chuo Kikuu Huria ndiyo mahala ambapo tutapakulia vijana hawa wanaotoka kwenye sekondari za kata, ndiyo mahala pekee tutaegemeza nguvu zetu, vijana hawa wapate pa kwenda. Kwa sasa mafanikio yanaanza kuonekana kwa vijana wengi waliomaliza *form six* kuweza kusoma *degrees* zao kwa miaka mitatu tu badala ya miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Chuo Kikuu Huria ni kwenda mpaka katika Wilaya. Sasa hivi kama walivyotuambia juzi, tunategemea watafungua matawi *(colleges)* kila Mkoa na Wilaya ikipata *college* au *centre* nina hakika tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana. Sikatai maeneo mengine ambayo vyuo hivi vitakaa, lakini kwa utaratibu tuliouchukua kujenga sekondari za kata ambazo mimi naamini ndiyo ukombozi katika nchi yetu hii kwenye nyanja ya elimu, bila kuimarisha Chuo Kikuu Huria vijana wanaosoma katika shule hizo watamaliza tu na watakuwa kama darasa la saba. Watajazana mitaani na *form four* pamoja na *form six* zao kwa sababu hawana pa kwenda na tutaanza kujenga tena tabaka la watu wasio na kazi na wasio na elimu. Mimi nashauri sana, Chuo Kikuu Huria kipewe *priority* na kama tulivyoona kwa kweli waweze kuruhusiwa kufungua maeneo ambayo ni kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri atamke kwa kifupi amekiandalia nini Chuo Kikuu Huria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la mwisho. Hili ni suala la migomo ambalo sikupenda kulizungumza zungumza sana. Mimi ningependa kutamka wazi kwamba mtu yeyote mwenye kuitakia heri nchi hawezi akaamka mbele ya wenzake akasema tutaandamana litakalotokea litajulikana huko huko, mtu huyo atakayefanya hivyo ana kasoro fulani za kuelewa. Hivi wewe umwambie mwanao nenda ukafanye kosa halafu umwambie yatakayokukuta huko utajijua. Hizo ni busara za mzazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema katika dunia yote ni ukweli kwamba wanafunzi wanakwenda shule kwa ajili ya kusoma, si mambo mengine. Niwaombe Wakuu wa Vyuo wawe wakali. Mwanafunzi anayejiingiza katika mambo yasiyohusiana na masomo yake achukuliwe hatua. Wewe umekwenda kusoma, leo unaacha unakwenda kwenye maandamano, tena baya zaidi unachukua kiboko ukamtandike mwenzako ambaye anakataa maandamano.

Mimi nafikiri ni jambo la ajabu sana. Naamini Wakuu wa Vyuo ambao watawaruhusu wanafunzi hao, ningekuwa mimi kwanza nawatandika viboko halafu ndiyo hapo hapo anaikuta barua ya kufukuzwa kwenye geti. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na mwalimu?

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Ni mwalimu, sasa si ameletwa nimfundishe? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri wale wenzangu wenye kutamka kwamba maandamano ndiyo silaha ya mwisho kutafuta haki, inawezekana tukaichukua katika *narrow mind.* Siamini kwamba tumefika mahala mpaka tunaenda kuitisha migomo au tukafanya mambo ambayo ni ya aibu; tukachoma madarasa, tukavunja milango, halafu kesho tena tunatengeneza, kwa kweli si burasa. *(Makofi)*

Sisi Wabunge tuepuke kauli za kuchochea fujo, hilo ndiyo ombi langu. Wabunge wote tuepuke kauli za kuchochea fujo, Mbunge anayechochea fujo mimi nafikiri sasa tubadilishe Kanuni zetu. Unatamka hapa nendeni mkagombane na wewe tutakujadili kwa sababu huitakii heri nchi yetu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kumalizia kwa kusema kwamba suala la kuimarisha shule za sekondari, shule za msingi, shule za kata, ni la msingi sana. Fedha ziongezwe na pia tuangalie sasa hivi kasi ya wazazi kujitolea kwa ajili ya kuimarisha shule za kata, inaonekana kupungua. Hili tusipoliangalia kama Serikali tutajikuta kwenye matatizo. Bado turudishe ari, tuwasihi wananchi wetu wakubali kwamba ukombozi wao katika elimu ni katika shule za kata kwa upande wa sekondari na shule za msingi katika vijiji vyao. Mimi naamini tukienda hivyo tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo basi nashukuru sana na nisisitize moja ambalo wenzangu wamelizungumza. Ningeomba kusema kwamba ukitaka mtu afanye kazi, hata ng’ombe wako ukitaka atoe maziwa mpe majani au pumba.

Wenzangu wengi wamezungumzia kuhusiana na walimu kutopewa haki zao. Hili kwa kweli halina upande na mimi naomba Serikali ilione hili kwamba walimu wanaishi katika mazingira magumu sana huko vijijini, pamoja na watumishi wa Idara nyingine kama wauguzi. Nafikiri tukubaliane wazi na ninapendekeza kwamba ikiwezekana zitolewe posho maalum kwa maeneo ambayo kwa kweli ni ya mateso makubwa. *(Makofi)*

Hili naliomba sana na wala Serikali tusilionee aibu. Kule kwangu mwalimu aliyeko Mboghoi, Mlola ni tofauti sana na mwalimu aliyeko Gare. Huyu wa Mboghoi akiona umeme anashangaa, huyu mwingine angalau anajua kuna umeme katika nyumba yake. Kwa hiyo, huyu nae apewe kamotisha ka kununua betri, ni haki yake na haya mambo tusiyaogope. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mimi naamini ni kilio cha Wabunge wengi na bahati nzuri Serikali yetu ni sikivu na ninyi mmechaguliwa kama chekecheke la Chama cha Mapinduzi, Serikali inayosikiliza matakwa ya watu, hebu hili liangalieni, fedha zitengwe kwa ajili ya kuwapa motisha walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo nashukuru sana, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ninayo shukrani mbele za Mungu na mbele za Bunge lako Tukufu kwa namna ya pekee jinsi Mungu alivyoniponya, nilivyokuwa nimeshikwa na ugonjwa kwa ghafla juzi. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Pia napenda niwashukuru Wanankenge wote kwani waliposikia habari hizi zikitangazwa walishtuka sana. Pamoja na mme na watoto wangu, pia namshukuru sana Mchungaji wangu Askofu Mwakiborwa, kwani alipoomba Bwana alinifungua. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka ku-*declare interest* kwamba ninayo shule kwa hiyo kwa kiwango fulani ninayajua matatizo yanayohusu shule. Napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mambo mengi wanayoyafanya. Pamoja na halisi iliyopo ya upungufu wa fedha, lakini kwa kweli kazi kubwa inafanyika na tunaiona. Kwa hiyo, kwa kweli mnastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niongelee tu kwa namna tofauti suala la walimu kutofika katika vituo vyao vya kazi. Kwa kweli walimu wengi hawafiki katika vituo wanavyopangiwa. Ni kweli kuna matatizo, lakini nadhani pia Serikali iliangalie suala hili na ijiulize ni kwa nini walimu hawafiki kwenye vituo vyao vya kazi wanavyopangiwa? Nitatoa mfano, katika jimbo langu la Nkenge, Serikali ilitupatia walimu wa Stashahada 18, waliofika vituoni ni 13, waliokataa kuja ni walimu watano. Walimu wenye Shahada tulipewa 14, ambao walifika ni saba na wengine saba hawakufika kabisa. Katika Mkoa wa Kagera mzima tulipewa walimu 227, walimu waliofika ni 132 na waliokataa kufika ni 95. Walimu wenye Shahada tulipewa 271, walifika ni walimu 141 na ambao hawakufika

ni walimu 130. Unaweza ukaangalia ni namna gani walimu wengi hawajafika katika vituo vyao vya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri. Mimi kitu ambacho nilikuwa naomba kushauri ni kwamba kuna walimu wengi, tuseme walimu wote hawa 130 Halmashauri zetu zipewe mamlaka ya kutangaza hizo nafasi za walimu ambao hawakufika kwenye vituo vyao vya kazi kwa sababu hizo fedha zinakuwa tayari zimetengwa na Serikali ili tuweze kuziba hizo nafasi za walimu na watoto wapate kufundishwa, kwani tukilifanya hilo kwa sababu kwenye Bajeti fedha inakuwepo tayari, kuna tatizo gani? Kuna mwalimu mwingine angependa kwenda kufundisha kule Kanyigo lakini kwa kuwa Serikali haikumpatia nafasi, amebaki hana pa kwenda. Hebu Halmashauri zipewe mamlaka tuweze kuwalipa walimu na waajiriwe kwa ajili ya kufundisha katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa ninaomba kushauri ni kwamba lazima kuwepo na *incentives.* Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema hapa kwamba tunatakiwa kuwa na motisha, ni namna gani mwalimu anayefundisha kwenye taa na yule anayefundishia kwenye vibatari wapate mshahara unaofanana? Hivyo mimi ningeomba tufanye utaratibu kama nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi nyingi zimefanya hivyo; nitakupatia taarifa labda wewe unayo pia, kuna vitu ambavyo tunaweza kufanya. Tunaweza kutoa *hardship allowance,* tunaweza tukatoa nyumba ili mtu anapokwenda katika eneo lile akute nyumba ipo. Tunaweza tukatoa *transport allowance,* tunaweza tukaweka mapumziko kwa mfano, mwalimu anatakiwa kupumzika mara moja, lakini aliyeko katika *remote areas* akapewa kupumzika labda mara mbili. Tunaweza tukatoa mafunzo, yaani semina, *courses* kwa walimu ambao wanafundisha katika *remote areas. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawa-*motivate* kwa namna tofauti. Mimi nitatoa mfano, mwalimu anayefundisha kwenye wilaya yangu, kule Jimbo la Nkenge katika Kata ya Kakunyu ukampa mshahara sawa sawa na mtu anayefundisha Kyaka, kwa kweli utakuwa huwatendei haki walimu katika maeneo yao. Hivyo ningeomba Serikali iangalie namna gani inaweza ikatoa vitu kama hivyo. Tukifanya hivyo elimu zitalingana kuliko hivi sasa ambapo elimu ya mjini na ile ya vijijini kuna tofauti kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niongelee nchi ambazo zimejaribu kufanya hivyo. Ukienda katika nchi ya Uganda wao wameamua mwalimu aliyeko vijijini wampatie *percent* 30% zaidi ya mshahara wake. Kwa hiyo, mwalimu anaweza akaona ni bora aende kufundisha vijijini kuliko mjini. Tukienda Lesotho, wao wameamua kuongeza mshahara kwa takribani maloti 276 sawa sawa na shilingi za Tanzania 60,000/=. Kwa maana hiyo, mwalimu ataona amejaaliwa na atakwenda kufanya kazi katika maeneo ya vijijini. Ukienda nchini Malawi, wao wameamua kila mwalimu anayekwenda kufundisha sekondari akute nyumba tayari na ina kila kitu ndani. Utakapokwenda Mozambique, wao wameamua kutoa mshahara mara mbili, mwalimu ambaye yupo mjini kama anapata

shilingi 400,000/= yule wa vijijini apate shilingi 800,000/= hiyo ime-*motivate* walimu wanaopangwa vijijini kwenda kufundisha huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija Tanzania utashangaa kuona vipo kwenye maandishi. Walianzisha mkakati huu wa kusema wataweka *incentives* (motisha) mwaka 2009, lakini mpaka leo Tanzania haijatekeleza jambo hilo, matokeo yake walimu wanapopelekwa vijijini wanakataa kwenda. Mimi nilikuwa najiuliza, tatizo ni nini? Kama wenzetu wanafanya, sisi kwa nini tusifanye? Kama tunaona walimu hawaendi maeneo ya vijijini tunaendelea kuimba wimbo walimu wamekataa kwenda vijijini, walimu wamekataa kwenda vijijini, hivi kweli tatizo hatulioni? Mimi naishauri Serikali ikubali kutekeleza kuliko kuongea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni matokeo ya kidato cha nne. Mimi ukiniambia kwamba watoto wengi walishindwa nitakukatalia. Kwa nini nakataa? Ni kwa sababu shule za kidato cha tano hazipo? Hata tungesema wame-*pass* wote wangekwenda wapi? Je, tunazo shule ambazo kama wangekuwa wamefaulu wangeenda? Mimi nimetembea kwenye shule za *A-level*, nilipokwenda hakuna mahali ambapo nilikuta darasa ambalo limepungukiwa watoto. Kwa maana hiyo, tunaweza kusema watoto wamefeli, lakini ni kwamba hatuna pa kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa ni kwamba mwaka huu kwenye Bajeti yetu kama tulikuwa hatukuweka, ningeomba tujenge shule za kidato cha tano kwa kila tarafa haraka iwezekanavyo ili hiki kisingizio cha kusema watoto wamefeli kiweze kuondoka. Si kweli kwamba watoto wote walifeli, lakini kama wange-*pass* mngewapeleka wapi? Maana hakukuwepo na maandalizi ya shule zinazolingana na watoto waliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee elimu ya ufundi. Katika mkoa wetu wa Kagera tunapenda kuishauri Serikali itupatie hata chuo kimoja kwa mkoa mzima kuliko kusubiri ile programu ya kila wilaya ambayo itachukua muda mrefu. Sisi tungependa tupate chuo kikubwa, kizuri, chenye kila kitu, angalau kimoja kwa ajili ya ku-*solve* hii *problem* ya watoto kukosa mahali pa kwenda kuliko kungoja hiyo proramu ya kila Wilaya ambayo nina hakika itachukua muda mrefu na haitakamilika kwa vitu vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukichukua nguvu yote tukaweka kwenye chuo kimoja, tukajikuta kila mkoa una chuo kama kile cha *VETA* iliyopo Dar es Salaam hata kama nimesahau sehemu lakini wote tunajua chuo chetu kizuri kilichoko Chang'ombe. Kwa hiyo, ni vyema tukawa na vyuo kama hivyo katika mkoa huku pole pole tukiandaa kujenga vya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea kwa haraka kwa sababu ninayo mengi lakini ningependa niongelee siasa mashuleni. Mimi kwa kweli ninasikitika sana watoto wetu wanapokuwa badala ya kusoma, ngoja nieleze hivi, unajua siasa ikimuingia mtu anakuwa *addicted*, anakuwa ni kama hana muda wa kuwaza kingine, anawaza *politics* tu, sasa tukiendelea kuwachochea watoto waanze siasa kule vyuoni badala ya kusoma, asubuhi

mpaka jioni watakuwa wanabishana, mimi CHADEMA, mimi CCM, mimi…, matokeo yake hawawezi kusoma vizuri. Hebu tuchague vyuo vya siasa, anayetaka kuongelea siasa akasome kwenye vyuo hivyo ili kwamba vyuo vingine vikae kwa amani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba siasa vyuoni kwa kweli siyo nzuri. Nimesikitishwa na mtoto wa mdogo wangu siku moja amerudi amepigwa, amechubuka, kisa amekataa kuandamana, amekataa kugoma. Kama wanasiasa wangesoma kwenye vyuo vya siasa nakwambia tusingekuwa na matatizo, wangeendelea na siasa huko huko na wakatoka wakiwa wataalamu kuliko labda watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni kwamba katika maongezi yangu yaliyopita niliomba kuwepo *commitment,* wanafunzi wengi au walimu au wanavyuo wanapokuwa vyuoni, akaenda chuoni akamaliza anaweza kuamua kwenda vijijini au akakataa kwa sababu hujam-*commit* katika jambo lolote na hawa watu wanakuwa wamechukua pesa nyingi. Mfano, mtu anakwenda pale anasoma ualimu, amemaliza unamwambia aende Nkenge kule Kakunyu amekataa, utamkamata vipi wakati wewe hujam-*commit?*

Mimi nashauri Serikali, narudia tena nawaomba sana tuweke kipengele cha kumwambia mwanafunzi kama unataka mkopo wetu tutakapokutuma Kakunyu utakwenda angalau kwa miaka mitano, ili aweze kutusaidia huku tukiandaa hali nzuri ya walimu katika sehemu nyingine, kuliko sasa hivi mtu ukimpeleka huko akikataa huna namna ya kumshitaki na wengi wamepotelea kwenye *private schools,* wameenda kwenye mambo mengine. Hebu tuweke *commitment* kwamba atakayekataa kwenda maeneo ya vijijini, mkopo wetu auache ili tusomeshe wale walio tayari kuisaidia Serikali bila kujali mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mishahara ya walimu. Kwa kweli mishahara ya walimu hata kama ni hiyo waliyonayo basi waipate kwa wakati na hasa wakati mwingine kwa nini nilikuwa nasema tuwape posho, kwa mfano usafiri. Mtu anatoka Kakunyu kuja kuchukua mshahara Wilayani kwangu Kyaka ni kilomita 105 hawezi kurudi kule analipa pesa nyingi. Hivyo nilikuwa ninashauri kama wakiwa na maombi yao kwa nini inachukua muda kujibiwa.

Nilipokuwa katika ziara yangu ya jimbo nilitembelea walimu peke yao nikaongea nao. Wakasema kinachotusumbua wala sio kikubwa, tunachohitaji tukiandika hata barua zetu za malalamiko tujibiwe kwa wakati. Mtu hata barua kujibiwa inachukua miezi sita hajaelewa. Mwingine anapandishwa cheo kutoka ngazi moja kwenda nyingine anakaa miezi sita anapata mshahara ule ule wa ngazi ya kwanza hajapata mshahara wake wa ngazi ambayo anastahili. Hivi kuna tatizo gani, maana unapompandisha mtu tayari umeweka kwenye Bajeti ni kitu gani anastahili kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tusiwalaumu sana walimu, hebu tuwasaidie wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maneno niliyoyasema yanatosha ninachoomba sana walimu nao ni watu, tukiwatengenezea mazingira mazuri watakimbilia vijijini na

wataacha mjini kwa sababu wanaona tunajali.  Kwa hayo machache Mungu awabariki sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwa Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza sasa hivi juu ya siasa na wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkosamali hapa alimaliza Chuo Kikuu mwezi uliopita ni mwanasiasa na ni Mheshimiwa Mbunge ni mwanafunzi na hatujaambiwa kwamba Mheshimiwa Mkosamali ameshindwa kusoma kwa sababu ni Mbunge.  Sasa haya maneno ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tundu Lissu taarifa imefika.  Kwa sababu ya kuokoa muda wetu taarifa imefika kwa muhusika, kwa hiyo ataizingatia.  Naomba…

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Siipokei hiyo taarifa. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naomba tusikilizane. Taarifa yako imeshafika sasa naomba nimwite Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Susan Kiwanga ajiandae. Tafadhali.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa maamuzi magumu na mazito ya kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kwa hakika sisi na mimi ni-*declare* tu kwamba kama mtu wa Dodoma, kama Mbunge wa Mkoa wa Dodoma kwamba sisi tutaendelea kuikumbuka Serikali hii ya Awamu ya Nne maisha yetu yote kadri Mungu atakavyotujalia kwa jambo hili kubwa ambalo Serikali imefanya.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimpongeze sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.  Nilipokuwa nasoma ukurasa wa 53 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameainisha changamoto. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi nakupongeza, changamoto hizi ni za kweli na ndizo zipo na kwa kweli kwa maana ya changamoto hizi na ndiyo maana tunaona hata fedha unazoziomba ni kidogo pengine ulipaswa kuomba fedha nyingi zaidi.  Lakini tutafanyaje kwa sababu uwezo wetu pia wa Serikali ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na namna ambavyo nimeisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ninavyojua matatizo ya elimu katika nchi yetu.  Uwanja wa matatizo ya elimu katika nchi yetu pamoja na uainishaji wa ukurasa wa 53 wa hotuba ya Waziri juu ya changamoto hizi bado ni uwanja mpana na hata zile changamoto ni nyingi sana kwa hakika pengine sio rahisi kwa mzungumzaji yeyote humu ndani akaweza katika hotuba ya dakika 15 kueleza matatizo anayoyafahamu ya elimu. *(Makofi)*

Mimi naomba niweke mchango wangu kwa kuzungumzia upungufu wa walimu, lakini upungufu wa walimu ninaotaka kuuzungumzia maana upungufu uliopo katika shule za msingi ni tofauti na upungufu uliopo katika shule za sekondari. Katika shule za msingi upungufu uliopo unatokana na mazingira magumu ambako walimu wengine wakipangiwa katika Wilaya zetu hawapendi kwenda. Hili ni tatizo kubwa ambalo ni kwamba Serikali kwa kweli na hasa sisi Bunge inabidi tufikie hatua ya kufanya maamuzi magumu katika jambo hili. *(Makofi)*

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba tunapitisha Bajeti hii lakini ni vizuri tunapofikiria namna ya kutatua tatizo la walimu na ili watu waweze kuipenda kazi ya ualimu ni kuwaongezea maslahi yao. Jambo pekee ni kuwaongezea maslahi yao. Mwalimu hana marupurupu yoyote, mwalimu hana posho yoyote, kumuacha mwalimu huyu anakwenda kuishi katika kijiji kama vile Gwamungile, Mang'aliza, Kibakwe halafu ukamlipa mshahara kama mtu anayefundisha shule ya msingi Kariakoo, mimi nadhani hatuwatendei haki. Ipo haja ya sisi kama Bunge, mimi niseme kama Bunge kufikiri namna ya kutunga sheria maalum kwa ajili ya walimu hasa kuzingatia maslahi yao. Hili litatusaidia lakini tukibakia tunanung'unika tu hapa na kusema Serikali iongeze, Serikali itaongeza kwa *formula* ya watumishi wa umma. Lakini sisi ndio tunaweza tukasema ije sheria maalum kwa ajili ya kuongeza maslahi ya walimu na Serikali inaweza kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upungufu huu pia unachochewa na mipangilio ambayo kwa hakika pengine Mheshimiwa Waziri achukue huu mchango kwamba kule vijijini na katika maeneo yetu yote kwa sasa tuna wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na wapo tayari kabisa na wanajua maeneo wanayotoka na wana uwezo wa kwenda huko Gwamungile, Igului, Galigali, Mang'aliza au Matonya wanaweza kwenda. Lakini huwezi ukamchukua mtoto aliyekulia hapa Dodoma, Mpwapwa ukasema unampeleka Gwamungile, hawezi kwenda. Nimeshuhudia mwenyewe Afisa Elimu anawapokea walimu, anawapangia kazi, wale wanakwenda stendi kuuliza eti huko basi hili linafika? Wakiambiwa halifiki wanarudi pale wanalia mpaka wanakula mchanga. Mtoto wa kike anauliza kwanza kuna *network* kule, anaambiwa kule hakuna *network* anasema sasa mimi mchumba wangu nitawasiliana naye vipi? Haendi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ipo haja ya kuamua kwa dhati tunazo sekondari zinatoa walimu na mimi juzi nimepelekwa kwa Naibu Waziri nikasema mimi hawa naomba wapelekwe vyuoni maana hawa nitawarudisha waje wafundishe kwenye mazingira haya magumu. Hii habari ya Utaifa tutaizingatia baadae wakifanya kazi miaka mitatu baadae utamhamisha utaleta wengine Utaifa utaendelea kuwepo tu. Lakini tuki-*generalise* hili jambo hakika litatushinda. Lakini upo upungufu wa walimu wa sekondari, niliwahi kusema hapa wakati ule wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Nikasema tumepata walimu waliopata kozi ya muda mfupi na wanatusaidia katika kufundisha sekondari zetu. Ninyi tena mnaanza kutoa vibali waende wakasome hawajamaliza hata mwaka, wakaondoka wote wakaenda kusoma. Kumbe tungewaacha angalau watufundishie watoto wetu kwa miaka hata miwili au mitatu tungekuwa tumewafundisha wakati wale wanaingia na hawa wanakwenda tukashindwa kuwa na

uzalendo wa jambo hilo na waamuzi ni watu wa Wizarani na wataalamu wetu ndio mliokuwa mnaamua. Maana wale nao walikuwa wanakuja na vibali tena hawaagi hata kwa wakuu wao wa shule, hawaagi hata kwa Maafisa Elimu wao wanakurupuka tu unawaambia ameenda kusoma, tukajikuta sekondari zetu zote hazina walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda tumefika mahali, wamekwenda wamesoma wamemaliza, sasa kosa lingine limekuja badala warudi kwenye shule walizokuwa wamepangiwa, badala warejeshwe kule kule waliokoomba ruhusa wakaambiwa nendeni mkasome, sasa mmewapangia sehemu nyingine, mnawa-*allocate* upya kwanza kwa hela ipi. Hawa watu walikuwa na vituo vyao vya kazi kwa nini wasirudi kule kule? *(Makofi)*

Mimi nadhani mnataka kuleta kizaa zaa kingine. Nakumbuka kwenye shule zangu za Jimbo la Kibakwe kuna sekondari 12, kulikuwa kuna walimu wasiopungua nane kila sekondari, lakini wote wamekwenda kusoma. Sasa nilidhani wanarudi kumbe wenzetu mmewa-*allocate* sehemu nyingine. Sasa jamani hivi tutatatua kweli hili tatizo, wangerudi kwenye vituo vyao vya awali. Sasa ndio waanze na hizo digrii zao muanze kufanya *allocation* upya. Sasa hapa mnazalisha tatizo ambalo hakika nawaambieni hamuwezi ku-*solve.* Tatizo la upungufu la walimu litabakia pale pale. Waacheni warudi kule naomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri jambo hili msifanye makosa tena ya mara ya pili, linatuumiza. Suala la upungufu wa walimu ndio siasa. Ukisikia Tundu Lissu amekwenda kule Kibakwe, unasema tayari anakwenda kuzungumzia upungufu wa walimu. Kwa nini iwe Tundu Lissu apate faida, apate urahisi wa kutengeneza siasa nyepesi kama hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ni kumpelekea walimu pale akifika pale akose la kusema. Kwa hiyo, naomba sana tufanye siasa ya mambo mengine makubwa, lakini haya mengine madogo madogo hebu tuyamalize kwa kuweka hiyo hali vizuri na naamini hili linawezekana. Nilikuwa najaribu kuiangalia Bajeti hii, nimeangalia Bajeti pia najua kuna Bajeti za Halmashauri, lakini tulisema hapa kuna suala la kujenga maabara kila sekondari. Ninavyoona maana hii Wizara ya Elimu mara huyu ananyofoa huku, TAMISEMI wamenyofoa huku sasa hatuelewi elewi. Sijui itakuwaje lakini nadhani sijui kama kweli maabara zitajengwa kila sekondari. Sijui fedha zake zipo wapi nitaomba ufafanuzi, nieleweshwe wakati wa majumuisho yako Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la mitaala katika shule zetu za msingi. Hii mitaala sasa vitabu vinavyofundishia tunaweza tukakuta tunatengeneza wanafunzi wenye *levels* tofauti kwa sababu huyu amesoma kitabu cha Nyangwine, huyu amesoma kitabu cha nani, kwa hiyo, kila mtu sasa nchi hii anasoma kitabu chake. Kuna jambo alikuwa amelianzisha Profesa Maghembe, hebu liendelezeni la kwamba vitabu vyote nchi nzima viwe ni vilevile vilivyopitishwa na *EMAC* na hawa *EMAC* mimi nina maneno nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao *EMAC* kazi yao ni ku-*control* na kuangalia vifaa vya kufundishia vitabu na kila mazingira. Lakini sidhani kama wanafanya kazi yao sawasawa maana vitabu tunavyokutana navyo mitaani mpaka unasema hivi hiki kilipitiwa kweli na watu kikaruhusiwa kwenda kufundishiwa au pengine kuna ujanja ujanja hasa katika sekta ya elimu au tukitaka kuua Taifa hili ndugu zetu wa *EMAC* ndio mtakuwa wa kwanza na dhambi hiyo haki ya Mungu, mtahukumiwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu kama mnataka kuua elimu hii ni kuleta *double standard* kwa kukubaliana na vitabu, kukubaliana na vifaa vya kufundishia kiujanja ujanja wala hamnufaiki na dhambi hii itawang'ang'ania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo baya sana mmeaminiwa kufanya kazi ambayo inajenga uhai wa Taifa, lakini namna mnavyoifanya inatutia mashaka kwa sababu vitabu tunavyokutana navyo kule havifai. Maandishi herufi zingine hazipo sawa, jamani hivi kweli tumefikia hatua hiyo? Mimi nadhani ipo haja ya kuona hii *EMAC* na nadhani Wabunge tuna haja ya kuhoji sana hii *EMAC* tunaua Taifa kwa kupitia hawa watu. Kama hawana uwezo basi tuwajengee uwezo wa kutosha. Lakini wao ni watu muhimu sana na umuhimu wao ungejidhihirisha kwa kazi yao nzuri wanayoifanya halafu walalamikie juu ya kujengewa uwezo.

Naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili la *EMAC* na uwezo wao na namna wanavyofanya hatujafurahishwa na kazi yao, tunasoma vitabu hivyo tunakuta vina mapungufu makubwa. Lakini hata vile vifaa vya kufundishia, ile *campus* wanayopelekewa watoto sasa hivi ni *fake.* Zamani unakuta ile *set square* mtu ukipewa unakaa nayo hata miaka mitano utamaliza shule unamwachia na mdogo wako na mdogo wako. Sasa sijui vifaa vinapitishwaje huko. Mimi nadhani kwa kweli ni upungufu mkubwa. *(Makofi)*

Lakini jambo lingine ni namna ambavyo tunachukua wanafunzi wetu kwenye vyuo. Hivi unapompima mwanafunzi aliyesoma sekondari ya Mbuga ambaye ana walimu wawili, unampima sawa sawa, mtihani ule ule na anayesoma Tambaza ambaye ana walimu wote mpaka wanajirudia. Hivi kweli unawapima hawa wanafunzi? Haki iko wapi, elimu ni haki ya kila mmoja. Haki kweli hapa ipo?

Mimi nasema sekondari zingine huku hivi teknolojia sasa hizi zimekuwa hivi lazima watu wafanye mtihani mmoja tuangalie na mazingira yetu. *Division four* ya *Kibakwe secondary* ndio *division one* ya Tambaza au ya Azania. Wakipenya hawa watoto wenye *division three* wakienda *form six* kwenye shule nzuri Mheshimiwa Waziri wanapiga *division one* na mliowaona hapa walio penya. Wale wachache tu wamekuja hapa saba ni ma-*genius* wale.

Sasa hatuwezi tukawahukumu halafu mnatupangia ili aende kozi ya ualimu awe na *division iv* ya pointi 26, jamani mnatuonea. Sisi wenzenu za pointi 30 ndio wenye akili na ndio wamefaulu maana yake wamefundishwa na walimu wawili, maana yake nini? Sisi wenye majimbo ambayo yako vijijini hatutakuwa na wasomi katika nchi hii. Sasa hapa mnawaonea, tutengenezeeni namna ya kuwajaribu kwa namna yoyote ile kwa

kuzingatia hali waliopo, pengine mwanafunzi aseme alifundishwa vipindi vingapi hata kwenye hilo somo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan tuna dakika kumi je, unaweza kuchangia leo ama kesho?

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba iwe kesho.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) isomwe kwa pamoja na Kanuni namba 37.

**MWENYEKITI:** Naomba usome Mheshimiwa…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Kanuni ya 37(1) ambayo inasema kwamba; "Hati inaweza kuwasilishwa Bungeni wakati wa Vikao vya Bunge na Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Kamati yoyote ya Bunge au Mbunge yoyote na Kanuni hiyo ya 37(5) na (6) inaongelea kuhusu hoja itakayowasilishwa kwa kutumia Kanuni hii ya 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kanuni hii ku-*refer* kwa hati ambayo iliwasilishwa jana mezani na Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ambayo ilikuwa ni barua ikitoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Bwana David Jairo ikielezea ukusanywaji wa shilingi 50,000,000 kutoka katika Idara mbalimbali zilizo chini yake kwa makusudio mahsusi ya kutaka kuwa-*facilitate* Wabunge ili waweze kuipitisha Bajeti hiyo bila kipingamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uzito wa suala lenyewe na kwa kuzingatia uwajibikaji wa pamoja…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kabla hujaendelea sana naomba ukae chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge kilichofanyika jana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo hakuwasilisha hati, alichotoa ni kielelezo na kwa vile kimefika kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika atakifanyia kazi, hakuwasilisha hoja jana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba kabla ya kuahirisha Bunge hili nitoe matangazo yafuatayo…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae chini.

Baada ya kipindi cha Maswali na Majibu kesho saa 3.00 asubuhi Wabunge wafuatao watachangia kwa kumalizia ambao ni Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Betty Machangu.

Baada ya tangazo hili naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. Ahsanteni.

*(Saa 1.37 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 20 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*